# Nipashe

Jumatano Februari 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579834

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mashamba ya Sumaye, MO Dewji yaibua neno bungeni

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mapya yaibuka mauaji kanisani

UKURASA 2



Maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), wakiwa wamebeba boksi na sanduku vilivyosheheni nyaraka, katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, jijini Dar es Salaam jana, kusajili kesi ya uhujumu uchumi namba 01.2019, ambapo Mohamed Yusuf Ally, Aloysius Gonzaga na Isaack Sanga wanatuhumiwa kwa makosa ya ukwepaji kodi, utakatishaji wa fedha na kuisababishia serikali hasara ya Shilingi bilioni 2.9. **PICHA: JOHN BADI**

# Kesi mtuhumiwa mil. 7/- kwa dakika yawa gumzo

Asomewa mashtaka 506, nyaraka zabebwa kwenye sanduku na boksi, meneja wa benki aunganishwa, ahamishiwa korti ya mafisadi...*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

### MAGUFULI ASEMA TAIFA LINA MWELEKEO MZURI

RAIS John Magufuli, amewahakikishia Watanzania kuwa taifa linakwenda katika ...

**UKURASA WA 7**

### BEI YA MAFUTA YASHUKA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imetangaza bei kikomo za mafuta ya aina ya petroli, mafuta ya taa na diseli zikiwa...


## King'ora chazua taharuki mjengoni

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA HASIRA ZOTE KWA SINGIDA UNITED UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mapya yaibuka mauaji kanisani

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limedai zaidi ya risasi 10 zilitumika katika tukio la mauaji dhidi ya Isack Petro (28), aliyeuawa kwa kupigwa risasi kisogoni ndani ya Kanisa la Waadventista Wasabato lililoko Kijiji cha Kazikazi, Kata ya Kitaraka, Itigi mkoani Singida.

Tukio hilo lilitokea Jumamosi ndani ya kanisa hilo wakati Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Itigi, Pius Luhende (54), na watu wengine sita wakidaiwa kushiriki mauaji hayo kwa kupiga zaidi ya risasi 10 ndani ya kanisa. Watuhumiwa hao wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Singida.

Mbali na Mkurugenzi huyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, akizungumza na waandishi wa habari jana, aliwataja watuhumiwa ambao wanawashikilia kuwa ni pamoja na askari wawili wa wanyamapori, Rodey Elias (42), Makoye Steven, Ofisa Kilimo, Sylvan Lugwisha (50), Ofisa Sheria, Erick Paul (31), Ofisa Tarafa Itigi, Eliuta Agustino (43) na Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Yusuf John (25).

Akieleza kuhusu tukio hilo, Kamanda Njewike alidai kuwa lilitokea Jumamosi majira ya saa nane mchana, Mkurugenzi Luhende, akiwa na timu ya watu sita, walipokwenda kanisani huko kwa lengo la kuwakamata watuhumiwa.

Alidai kuwa Mkurugenzi Luhende na wenzake walikuwa wanawatafuta watuhumiwa wanaodaiwa kufanya kosa la kuharibu mali katika shamba la Tanganyika Parkers.

Kamanda Njewike alidai kuwa shamba hilo linamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ambako Isack (marehemu) alikuwa anaishi.

Alidai kuwa siku ya tukio, mkurugenzi na wote wanaoshikiliwa, waliamua kuingia mtaani kuwasaka watuhumiwa hao baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Rose Andrew, aliyedai kuharibiwa mali yake shambani humo.

"Wakati wanaendelea kuwasaka, ndipo wakagundua baadhi yao wapo ibadani kwenye kanisa hilo la Wasabato," Kamanda Njewike alidai.

Aliongeza: "Baada ya kufika kwenye kanisa, Mkurugenzi Luhende aliingia ibadani akitaka kuwakamata hao waliokuwa wanadaiwa kuwa ni watuhumiwa wa uharibifu wa mali shambani. Hali hiyo ilisababisha kutokea kwa vurugu kanisani."

Alidai kuwa, wakati vurugu hiyo ikiendelea, mkurugenzi huyo alitoka nje na kufunga mlango wa kuingia kanisani, ndipo askari wanyamapori walioongozana naye wakaanza kufyatua risasi kanisani humo.

"Moja ya risasi zilizofyatuliwa ilimpiga Isack eneo la kisogoni na kufariki dunia hapohapo. Risasi zilizopigwa ni zaidi ya 10 na uchunguzi wa tukio hili unaendelea wakati watuhumiwa wote saba wakiwa mahabusu."

Kamanda Njewike alisema watahakikisha watuhumiwa wanafikishwa mahakamani mapema kujibu tuhuma zinazowakabili.

Taarifa kutoka eneo la tukio zilizofikia Nipashe, zilidai kuwa mmoja wa watuhumiwa hao saba, baada ya kutokea vurugu kanisani, alirudi kwenye gari na kuchukua silaha.

Hata hivyo, Kamanda Njewike, alipoulizwa kuhusu suala hilo alisema hana uhakika nalo.

Nipashe pia ilitaka kujua kutoka kwa kamanda huyo kama watuhumiwa wanayo mamlaka ya kuendesha msako wa aina hiyo na akasema: "Mwenyekiti wa serikali ya mtaa ana mamlaka ya kukamata, lakini kwa tukio lililotokea na nguvu iliyotumika, tunachunguza kama mamlaka hiyo ndivyo inavyomwelekeza Mkurugenzi."

***Imeandikwa na Elisante John (SINGIDA) na Romana Mallya (DAR)***



Rais Dk. John Pombe Magufuli akinywa dafu alilonunua kwa mchuuzi Paschal Sabas, baada ya kukagua ukarabati wa Mradi wa Jengo la Kitega Uchumi la Chama Cha Mapinduzi la (SUKITA), lililopo Mtaa wa Lumumba, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 42 ya CCM, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole. **PICHA: IKULU**

# Kesi mtuhumiwa mil. 7/- kwa dakika yawa gumzo

**Na Waandishi Wetu**

KESI ya tuhuma za kutakatisha Sh. bilioni 24.30 inayomkabili mfanyabiashara Mohammed Yusufali na mwenzake, imeleta gumzo la namna yake mahakamani kutokana na nyaraka zake kubebwa kwenye sanduku na boksi.

Wakati hali ikiwa hiyo, upande wa Jamhuri umemuunganisha Meneja wa Benki ya I&M Tawi la Kariakoo, Sameer Khan, kwenye kesi hiyo.

Watuhumiwa hao walisomewa jana mashtaka 506, likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya mabilioni ya shilingi, huku kesi yao ikisajiliwa kwenye Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi.

Awali, Yusufali aliyedaiwa na Rais John Magufuli kuiba Sh. milioni saba kwa dakika, pamoja na mfanyakazi wake, Arifali Paliwalla, walikuwa wakikabiliwa na mashtaka 601 likiwamo kutakatisha Sh. bilioni 14.

Hata hivyo, Upande wa Jamhuri jana ulibadilisha hati ya mashtaka kutoka mashtaka 601 hadi 506 na kumuunganisha Khan katika kesi hiyo yenye namba za usajili 8/2019 na kusomwa mbele ya

INAENDELEA UK.8

# Magufuli asema taifa lina mwelekeo mzuri

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amewahakikishia Watanzania kuwa taifa linakwenda katika mwelekeo mzuri baada ya serikali kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha uchumi na huduma za jamii.

Alisema hayo jana alipokutana na wananchi katika mtaa wa Zanaki, jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kutembelea kampuni ya Africa Media Group (AMGL) yenye vituo vinne vya televisheni ikiwamo channel Ten na vituo viwili vya redio ikiwamo Magic FM, ambayo kwa sasa inamilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Rais Magufuli alisema pamoja na mafanikio hayo, serikali itaendelea kupambana na dhuluma na matumizi mabaya ya rasilimali za taifa na kutoa wito kwa Watanzania wote kuiunga mkono kwa kuhakikishia wanatanguliza maslahi ya taifa.

Akiwa ndani ya jengo la AMGL, Rais ambaye ni Mwenyekiti CCM, alijionea mitambo, chumba cha habari na studio za kurushia matangazo za kituo cha redio cha Magic FM na kituo cha televisheni cha Channel Ten na kuzungumza na wafanyakazi.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema wafanyakazi hao walimweleza Rais changamoto mbalimbali zikiwamo uhaba na uchakavu wa vitendea kazi, maslahi madogo ya wafanyakazi na uchakavu wa jengo la kituo hicho.

Kutokana na changamoto hizo, taarifa hiyo ilisema Rais Magufuli aliahidi kutoa Sh. milioni 200 ndani ya siku mbili kwa ajili ya kununulia vitendea kazi vya kituo hicho na kuwataka wafanyakazi wa AMGL kumpelekea mapendekezo ya jengo lolote la CCM lenye hadhi nzuri ili kuhamishiwa kituo hicho.

Aidha, Rais Magufuli aliwapongeza wafanyakazi hao kwa kazi nzuri wanazozifanya na kwamba dhamira yake ni kuhakikisha kituo hicho kinaboreshwa, matangazo yake yanafika maeneo mengi ya ndani na nje ya nchi na kinakuwa cha mfano kwa vituo vingine nchini.

"Nataka Africa Media Group Ltd iwe na vyombo vyenye nguvu, vinavyotazamwa kila mahali hapa nchini hadi nje ya nchi. Tanzania haiwezi kuwa soko la kuangalia vyombo vya habari vya kutoka nje ya nchi. Watu waangalie vyombo vya habari vya nje lakini vyombo vyetu viwe ndio mwongozo wa maisha ya Watanzania zaidi ya Milioni 50.

"Na hii natoa wito kwa vyombo vyote vya Tanzania, mna wajibu wa kuzungumzia mazuri ya Tanzania, lakini pia muendelee kutoa elimu kwa Watanzania, Watanzania karibu asilimia 75 ni wakulima, toeni vipindi vya kuonyesha kilimo bora, ufugaji bora, na kadhalika," alisema kama alivyokaririwa na taarifa hiyo.

Baada ya kutoka AMGL, Mhe. Rais Magufuli amekagua mradi wa ukarabati mkubwa wa jengo la kitega uchumi la CCM (Sukita) lililoko mtaa wa Lumumba Jijini Dar es Salaam ambalo litakamilika Juni, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# King'ora chazua taharuki bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MILIO ya king'ora cha kuashiria kuwapo hatari ndani ya jengo la Bunge, jana viliwafanya wabunge, mawaziri na wafanyakazi wa taasisi hiyo kutoka ndani ya jengo wakitimua mbio.

Hali hiyo pia iliulazimu uongozi wa Bunge kusitisha shughuli za chombo hicho cha kutunga sheria kwa takribani saa moja ili kupisha uchunguzi wa kiini cha milio hiyo ya king'ora, ambao baadaye ilielezwa kuwa hapakuwa na tatizo lolote.

Milio hiyo ilianza kusikika kwenye jengo la Ukumbi wa Bunge saa 5:02 asubuhi, wakati wa kipindi cha 'Maswali', Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Bernadeta Mushashu (CCM).

Kutokana na ishara hiyo ya hatari wabunge, mawaziri na watumishi wa Bunge walianza kutoka kwenye jengo hilo kwa kutimua mbio, baadhi wakipita mlango wa dharura, mkabala na eneo maalum la kurushia matangazo ya televisheni.

Dakika moja baadaye (saa 5:03 asubuhi), Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, alitangaza kusitisha shughuli za Bunge kwa muda.

Milio ya ving'ora hivyo ilidumu kwa dakika nane, kisha ikasikika tena saa 5:17 asubuhi, jambo ambalo lilizusha taharuki iliyowafanya wawakilishi hao wa wananchi kujikusanya vikundi vikundi wakijadili hatari hiyo.

**KAMANDA MUROTO**

Saa 5:20 asubuhi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akiwa ameongozana na maofisa mbalimbali wa vikosi vya ulinzi, aliwasili kwenye Viwanja vya Bunge kufuatilia kilichotokea.

Baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kiini cha milio ya king'ora hicho, Muroto alisema: "Tusubiri, bado vyombo vya usalama pamoja na Kikosi cha Uokoaji na Zimamoto wanafuatilia tatizo kujua ni nini kimetokea."

Gari la Zimamoto lenye namba za usajili ZT 0045 liliwasili kwenye Viwanja vya Bunge likiwa na askari na maofisa kadhaa kufuatilia tukio hilo.

Kazi hiyo iliendelea kwa muda na saa 5:50 asubuhi, baadhi ya maofisa wa Bunge walianza ku-

INAENDELEA UK. 8



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Charles Kichere (aliyechuchumaa), akiangalia vifaa vya kutengeneza risiti bandia za kielektroniki, baada ya watu wanne kukamatwa nazo katika eneo la Nzunguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# IGP Sirro apangua makamanda polisi

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amefanya mabadiliko ya makamanda kadhaa, ikiwamo kumhamisha Kamanda wa Mkoa wa Mwanza, Jonathan Shana ambaye amerejeshwa Makao Makuu ya Polisi.

Taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Jeshi la Polisi, Ahmed Msangi, ilieleza kuwa mabadiliko hayo yamewahusisha makamanda wa polisi wa mikoa ya Kinondoni na Mwanza.

Ilieleza kuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Jumanne Muliro, amehamishiwa Mwanza kuchukua nafasi ya Kamanda Shana.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Mussa Taibu, anakuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni.

Aidha, ilifafanua kuwa mabadiliko hayo ni ya kawaida katika utendaji kazi kwa Jeshi la Polisi.

# Mashamba ya Sumaye, MO Dewji yaibua gumzo

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SAKATA la Waziri Mkuu mstaafu, Fedrick Sumaye na mfanyabiashara maarufu nchini, Mohamed Dewji (MO) la kufutiwa umiliki wa mashamba yao kutokana na kushindwa kuyaendeleza, limewavuruga wabunge wa pande zote mbili na kuibua gumzo bungeni.

Wabunge wa Upinzani na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliingia katika mvutano na gumzo kuhusu taratibu zilizotumika kuyafuta, huku Spika wa Bunge, Job Ndugai, akilazimika kuzima mjadala huo, akisema anadhani suala la Sumaye liko mahakamani, hivyo si jambo jema kuendelea kulijadili bungeni.

Kabla ya Spika Ndugai kuzima mjadala huo usiendelee, Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Peter Msigwa, alisema haoni shida ya unyang'anywaji wa mashamba hayo, lakini taratibu zinazofanyika siyo sahihi.

Sumaye na Mohamed Dewji walitajwa mara kadhaa na wabunge hao wakati walipokuwa wakichangia taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya Januari 2018 hadi Januari 2019.

Taarifa hiyo iliwasilishwa bungeni na mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Dk. Stephen Kiruswa.

Akichangia, Msigwa alisema pamoja na mambo mengine, kamati haikuweka baadhi ya mapendekezo yake katika taarifa ambayo ni kuitaka serikali kuunda kamati ya kuchunguza unyang'anywaji wa mashamba hayo.

Kutokana na kauli hiyo ya Msigwa, Mbunge wa Simanjiro (CCM), James Ole Millya, alisimama na kuomba kumpa taarifa mzungumzaji huyo akisema: "Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mbunge, mimi natoka Jimbo la Simanjiro, takribani mwezi mmoja uliopita, Waziri alifuta mashamba zaidi ya 200 na nina hakika mashamba haya yote yalikuwa hayajafuata utaratibu na wala asipende kumchafua waziri."

Alipomaliza kutoa taarifa hiyo, Msigwa alimshangaa Millya akisema: "Mimi nadhani unaenda haraka, mimi sijamchafua sasa ni wapi namchafua, nimezungumza, nimesema sina tatizo kabisa na mashamba makubwa kunyang'anywa kwa mujibu wa sheria na kufuatwa utaratibu."

"Nimetoa mfano moja, Mheshimiwa Sumaye alikuwa na shamba lake, alilipata kihalali na ameliendeleza mpaka wanachukua shamba lake, alikuwa na ng'ombe 200 kwenye shamba lake, alikuwa na kondoo 350, nyumba kubwa ya umwagiliaji, kisima

INAENDELEA UK.8




Energy and Water Utilities Regulatory Authority

ISO 9001:2015 Certified

***KUMB: PPR/19 - 02/1***

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 FEBRUARI 2019

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Februari 2019.** Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Januari 2018. Kwa mwezi Februari 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 175/lita (sawa na asilimia 7.61), Shilingi 144/lita (sawa na asilimia 6.48) na Shilingi 156/lita (sawa na asilimia 7.08), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 174.03/lita (sawa na asilimia 8.02), Shilingi 143.65/lita (sawa na asilimia 6.84) na Shilingi 155.32/lita (sawa na asilimia 7.47), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, kupungua kwa bei za mafuta katika soko la ndani kunatokana na kuendelea kushuka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia kama inavyoonekana katika Jedwali C.

(b) Kwa Mikoa ya Kaskazini, bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zitaendelea kuwa zile zile za mwezi Januari 2019. Hii inatokana na ukweli kwamba, pamoja na kuwa kuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini mwezi Januari 2019 kupitia bandari ya Tanga, mafuta hayo ni kidogo na hayatoshelezi mahitaji ya mafuta kwa mikoa yote ya Kaskazini. Hata hivyo, ghala ya kuhifadhia mafuta mkoani Tanga bado ina kiwango kikubwa cha mafuta yaliyopokelewa mwezi Desemba 2018 ambayo yatatosheleza mahitaji ya mafuta kwa mikoa ya Kaskazini. Kwahiyo, bei hizi za kuanzia tarehe 6 Februari 2019 zimezingatia gharama za mafuta yaliyoingizwa nchini mwezi Desemba 2018 kupitia bandari ya Tanga.

(c) Vilevile, itakumbukwa kuwa, kuanzia tarehe 2 Januari 2019, bei za mafuta kwa Mikoa ya Kusini zilikokotolewa kulingana na gharama za mafuta yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi Mikoa ya Kusini. Hata hivyo, kutokana na kupokelewa kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika maghala ya mafuta yaliyopo mkoani Mtwara katika wiki ya pili ya Januari 2019, kuanzia tarehe 25 Januari 2019, wamiliki wa vituo vya mafuta katika Mikoa ya Kusini ya Mtwara, Lindi na Ruvuma walishauriwa kununua mafuta hayo kutoka katika ghala za mafuta zilizopo katika mkoa wa Mtwara.

(d) Hivyo, kuanzia tarehe 25 Januari 2019, bei ya rejareja ya mafuta ya Petroli na Dizeli katika Mikoa ya Kusini zilikokotolewa kulingana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara. Bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mikoa hiyo ya Kusini zitaendelea kuwa zile za kuanzia tarehe 25 Januari 2019. Hata hivyo kuna punguzo la Shilingi 0.68/lita ya Petroli na Shilingi 0.74/lita ya Dizeli kutokana na marekebisho ya gharama za ucheleweshwaji wa meli bandarini. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(e) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo *(price cap)*** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na **Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

## JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **2,120** | **2,080** | **2,046** |
| **Arusha** | **2,255** | **2,299** | **2,286** |
| Arumeru (Usa West) | 2,255 | 2,299 | 2,286 |
| Karatu | 2,273 | 2,318 | 2,304 |
| Longido | 2,266 | 2,310 | 2,297 |
| Monduli | 2,260 | 2,305 | 2,291 |
| Monduli-Makuyuni | 2,265 | 2,309 | 2,296 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,340 | 2,384 | 2,371 |
| **Pwani (Kibaha)** | **2,125** | **2,084** | **2,050** |
| Bagamoyo | 2,132 | 2,091 | 2,057 |
| Chalinze Junction | 2,135 | 2,094 | 2,060 |
| Chalinze (Msata) | 2,139 | 2,098 | 2,064 |
| Kibiti | 2,141 | 2,100 | 2,066 |
| Kisarawe | 2,128 | 2,087 | 2,053 |
| Mkuranga | 2,130 | 2,090 | 2,056 |
| Rufiji | 2,148 | 2,107 | 2,074 |
| **Dodoma** | **2,179** | **2,139** | **2,105** |
| Bahi | 2,187 | 2,146 | 2,112 |
| Chamwino | 2,175 | 2,134 | 2,100 |
| Chemba | 2,206 | 2,165 | 2,131 |
| Kondoa | 2,212 | 2,171 | 2,138 |
| Kongwa | 2,177 | 2,136 | 2,102 |
| Mpwapwa | 2,180 | 2,140 | 2,106 |
| Mtera (Makatopora) | 2,198 | 2,158 | 2,124 |
| **Geita** | **2,286** | **2,245** | **2,211** |
| Bukombe | 2,275 | 2,234 | 2,200 |
| Chato | 2,307 | 2,266 | 2,232 |
| Mbogwe | 2,324 | 2,283 | 2,250 |
| Nyang'hwale | 2,301 | 2,260 | 2,226 |

25047102

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Iringa** | **2,185** | **2,144** | **2,110** |
| Ismani | 2,190 | 2,149 | 2,115 |
| Kilolo | 2,189 | 2,148 | 2,114 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,195 | 2,154 | 2,120 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,336** | **2,295** | **2,261** |
| Biharamulo | 2,310 | 2,270 | 2,236 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,352 | 2,312 | 2,278 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,358 | 2,318 | 2,284 |
| Muleba | 2,336 | 2,295 | 2,261 |
| Ngara | 2,324 | 2,283 | 2,249 |
| Misenyi | 2,345 | 2,304 | 2,270 |
| **Katavi (Mpanda)** | 2,329 | 2,288 | 2,254 |
| Mlele (Inyonga) | 2,310 | 2,270 | 2,236 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,321 | 2,280 | 2,246 |
| **Kigoma** | **2,352** | **2,311** | **2,277** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,364 | 2,324 | 2,290 |
| Buhigwe | 2,341 | 2,300 | 2,267 |
| Kakonko | 2,309 | 2,268 | 2,234 |
| Kasulu | 2,338 | 2,297 | 2,263 |
| Kibondo | 2,316 | 2,276 | 2,242 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,245** | **2,289** | **2,276** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,248 | 2,292 | 2,279 |
| Mwanga | 2,238 | 2,282 | 2,269 |
| Rombo (Mkuu) | 2,261 | 2,306 | 2,292 |
| Same | 2,231 | 2,275 | 2,262 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,251 | 2,295 | 2,282 |
| **Lindi** | **2,110** | **2,089** | **2,105** |
| Lindi-Mtama | 2,114 | 2,093 | 2,123 |
| Kilwa Masoko | 2,133 | 2,112 | 2,080 |
| Liwale | 2,145 | 2,124 | 2,126 |
| Nachingwea | 2,130 | 2,109 | 2,134 |
| Ruangwa | 2,136 | 2,115 | 2,136 |
| **Manyara (Babati)** | **2,289** | **2,333** | **2,320** |
| Hanang (Katesh) | 2,300 | 2,344 | 2,331 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,304 | 2,349 | 2,335 |
| Mbulu | 2,302 | 2,346 | 2,333 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,321 | 2,365 | 2,352 |
| **Mara (Musoma)** | **2,299** | **2,258** | **2,225** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,340 | 2,299 | 2,265 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,308 | 2,267 | 2,233 |
| Rorya (Shirati) | 2,343 | 2,302 | 2,268 |
| Bunda | 2,290 | 2,250 | 2,216 |
| Butiama | 2,296 | 2,255 | 2,221 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,345 | 2,304 | 2,270 |
| Tarime | 2,310 | 2,270 | 2,236 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,315 | 2,274 | 2,240 |
| **Mbeya** | **2,228** | **2,187** | **2,153** |
| Chunya | 2,237 | 2,196 | 2,163 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,251 | 2,211 | 2,177 |
| Kyela | 2,243 | 2,203 | 2,169 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,212 | 2,171 | 2,137 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,237 | 2,196 | 2,162 |
| **Morogoro** | **2,146** | **2,105** | **2,071** |
| Mikumi | 2,161 | 2,120 | 2,087 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,183 | 2,143 | 2,109 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,206 | 2,165 | 2,131 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,195 | 2,154 | 2,120 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,194 | 2,153 | 2,119 |
| Malinyi | 2,204 | 2,164 | 2,130 |
| Kilosa | 2,164 | 2,123 | 2,089 |
| Gairo | 2,164 | 2,123 | 2,089 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,156 | 2,115 | 2,081 |
| Turiani | 2,171 | 2,130 | 2,096 |
| **Mtwara** | **2,096** | **2,075** | **2,118** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,132 | 2,111 | 2,167 |
| Masasi | 2,112 | 2,091 | 2,144 |
| Newala | 2,117 | 2,096 | 2,150 |
| Tandahimba | 2,110 | 2,089 | 2,144 |
| Nanyamba | 2,110 | 2,089 | 2,144 |
| **Mwanza** | **2,271** | **2,230** | **2,196** |
| Kwimba | 2,289 | 2,248 | 2,214 |
| Magu | 2,279 | 2,238 | 2,204 |
| Misungwi | 2,265 | 2,224 | 2,190 |
| Sengerema | 2,303 | 2,262 | 2,229 |
| Ukerewe | 2,330 | 2,290 | 2,256 |
| **Njombe** | **2,213** | **2,172** | **2,138** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,234 | 2,193 | 2,159 |
| Ludewa | 2,251 | 2,210 | 2,176 |
| Makambako | 2,205 | 2,165 | 2,131 |
| Makete | 2,244 | 2,203 | 2,169 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,211 | 2,170 | 2,136 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,294** | **2,253** | **2,219** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,294 | 2,253 | 2,219 |
| Kalambo (Matai) | 2,301 | 2,260 | 2,226 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,307 | 2,266 | 2,232 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,182** | **2,161** | **2,169** |
| Mbinga | 2,194 | 2,173 | 2,203 |
| Namtumbo | 2,173 | 2,152 | 2,199 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,220 | 2,199 | 2,213 |
| Tunduru | 2,147 | 2,126 | 2,228 |
| **Shinyanga** | **2,249** | **2,209** | **2,175** |
| Kahama | 2,263 | 2,222 | 2,189 |
| Kishapu | 2,278 | 2,237 | 2,203 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,281 | 2,240 | 2,206 |
| Simiyu (Bariadi) | 2,291 | 2,250 | 2,216 |
| Busega (Nyashimo) | 2,284 | 2,243 | 2,209 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,294 | 2,253 | 2,219 |
| Maswa | 2,282 | 2,242 | 2,208 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,289 | 2,249 | 2,215 |
| **Singida** | **2,211** | **2,171** | **2,137** |
| Iramba | 2,223 | 2,183 | 2,149 |
| Manyoni | 2,196 | 2,155 | 2,121 |
| Ikungi | 2,207 | 2,166 | 2,132 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,236 | 2,195 | 2,161 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,237** | **2,196** | **2,162** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,244 | 2,203 | 2,169 |
| Ileje | 2,241 | 2,200 | 2,166 |
| Momba (Chitete) | 2,246 | 2,205 | 2,171 |
| Tunduma | 2,241 | 2,200 | 2,167 |
| **Tabora** | **2,275** | **2,234** | **2,200** |
| Igunga | 2,229 | 2,188 | 2,154 |
| Kaliua | 2,294 | 2,253 | 2,219 |
| Ulyankulu | 2,288 | 2,247 | 2,213 |
| Nzega | 2,239 | 2,199 | 2,165 |
| Sikonge | 2,287 | 2,246 | 2,212 |
| Urambo | 2,288 | 2,247 | 2,213 |
| Uyui | 2,276 | 2,235 | 2,201 |
| **Tanga** | **2,198** | **2,243** | **2,229** |
| Handeni | 2,219 | 2,263 | 2,250 |
| Kilindi | 2,234 | 2,278 | 2,265 |
| Korogwe | 2,210 | 2,255 | 2,241 |
| Lushoto | 2,220 | 2,264 | 2,251 |
| Mkinga (Maramba) | 2,205 | 2,250 | 2,236 |
| Muheza | 2,203 | 2,247 | 2,234 |
| Pangani | 2,205 | 2,249 | 2,236 |

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

| **Bei za Jumla - DSM** | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta ya Taa (Shs/Lita)** |
|---|---|---|---|
| **Bei Kikomo** | **1,996.85** | **1,955.90** | **1,922.73** |

| **Bei za Jumla - TANGA** | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta ya Taa (Shs/Lita)** |
|---|---|---|---|
| **Bei Kikomo** | **2,074.48** | **2,118.21** | **2,105.56** |

| **Bei za Jumla - MTWARA** | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta ya Taa (Shs/Lita)** |
|---|---|---|---|
| **Bei Kikomo** | **1,972.49** | **1,951.12** | **----** |

**JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

**BANDARI YA DAR ES SALAAM**

| | **Petroli** | **Dizeli** | **Mafuta ya Taa** |
|---|---|---|---|
| Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Punguzo la Dola 115.352/Tani | Punguzo la Dola 104.947/Tani | Punguzo la Dola 102.194/Tani |

**JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

| | **Bandari** | **Petroli** | **Dizeli** | **Mafuta ya Taa** |
|---|---|---|---|---|
| **Mafuta yalipokelewa mwezi wa:** | **DSM** | Januari 2019 | Januari 2019! | Januari 2019! |
| | **Tanga** | Desemba 2018 | Desemba 2018 | Desemba 2018 |
| | **Mtwara** | Januari 2019 | Januari 2019! | ----! |
| **Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:** | **DSM** | Desemba 2018 | Desemba 2018 | Desemba 2018 |
| | **Tanga** | Novemba 2018 | Novemba 2018 | Novemba 2018 |
| | **Mtwara** | Desemba 2018 | Desemba 2018 | ---- |

**Nzinyangwa E. Mchany**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

215047702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni sahihi kabisa bandari kuachiwa makusanyo zaidi

**BANDARI** ni uti wa mgongo kwa taifa, kwa sababu inachangia asilimia kubwa ya mapato. Ni eneo ambalo serikali kujielekeza zaidi kupata fedha za kujiendesha pamoja na kutoa huduma nyingine muhimu kwa jamii.

Pamoja na jukumu la bandari la kutoa ushuru na kodi mbalimbali kwa bidhaa zinazosafirishwa nje na zinazoingizwa nchini, hayo inahitaji fedha kwa ajili ya kujiendesha na kutekeleza miradi kadhaa ya kuiboresha.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na kujihusisha na ukusanyaji wa mapato kwa taifa, imekuwa ikitelekeza miradi kadhaa husussan ya kujenga bandari mpya pamoja na kuboresha bandari zilizopo, ukiwamo upanuzi na ukarabati.

Kimsingi, utekelezaji wa miradi hii unahitaji fedha za kutosha, vinginevyo malengo ya mamlaka hiyo hayawezi kufikiwa. Tunasema TPA inahitaji fedha nyingi kwa kuwa Tanzania ina maeneo mengi ya maji ambayo yanahitaji bandari hususan bahari na maziwa makuu ya Victoria, Nyasa na Tanganyika.

Hata hivyo, kutokana na kutokuwapo utaratibu au mfumo wa serikali kuu kuiachia mamlaka hiyo sehemu ya makusanyo kwa ajili ya utejelezaji wa miradi yake, hali hiyo inaonekana kuiathiri kifedha.

Baadhi ya wabunge huko nyuma walikuwa wanalizungumzia suala hili na kupendekeza kwamba serikali iweke utaratibu wa kuiachia mamlaka hiyo sehemu ya makusanyo ili pamoja na mambo mengine izitumie kutekeleza baadhi ya miradi yake.

Katika msisitizo wa jambo hilo, Bunge limeitaka serikali kuibakishia angalau asilimia 40 ya makusanyo yake TPA, ili iweze kuendeleza baadhi ya miradi ya kimkakati, badala ya kuchukua makusanyo yote.

Kwa sasa TPA inatekeleza miradi ya ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara ambayo inaigharimu takribani Sh. bilioni 20, wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni Sh. bilioni 270.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu juzi, Mwenyekiti wake, Seleman Kokoso, alisema kamati yake imependekeza jambo hilo ili kuipa ahueni mamlaka hiyo.

Alisema kwamba moja ya malengo makuu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ni kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya kila mwezi.

Alieleza kuwa kwa kuwa mamlaka inayo miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa bandari na kwa sasa TPA ipo katika hatua ya kuboresha kwa kufanya ukarabati kama vile Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara, kamati inashauri kubakishwa angalau asilimia 40 ya makusanyo ya mamlaka ili iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake.

Mwenyekiti huyo aliliambia Bunge kuwa miradi kama vile ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara ambayo inagharimu takribani shilingi bilioni 20 wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni shilingi bilioni 270.

Alisema kutokana na hali ilivyo, kamati inaishauri serikali kufanya ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Ziwa Nyasa.

Kutokana na idadi kubwa ya miradi iliyotajwa kuwa katika utekelezaji, tunaona kuwa hoja ya Bunge ya kuiachia mamlaka hiyo asilimia kama hiyo ya makusanyo ina mantiki, kwa kuzingatia kuwa kiasi cha fedha kinachotakiwa katika utekelezaji ni kikubwa.

Bila shaka serikali italizingatia pendekezo hilo mapema iwezekanavyo, kwa kuwa kuipa TPA kiasi hicho cha fedha ni sawa na kuwekeza kwa kuwa miradi ya bandari inayotekelezwa ikikamilika itazalisha fedha zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

**BUSARA**

**VIJIKO SI LESENI YA KUTONAWA MIKONO**
MIONGONI MWA MAELEKEZO YANAYOTOLEWA NA MABWANA AFYA NI PAMOJA NA KUNAWA MIKONO KABLA YA KULA. HATA UKITUMIA UMA NA VIJIKO BADO UTATAKIWA KUNAWA MIKONO YAKO. TUSISAHAU USAFI NI TABIA TENA KINGA DHIDI YA MARADHI. TUSICHOKE KUKUMBUSHANA.
**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni aibu wanafunzi kusomea chini ya mti jamii inaisubiri serikali



Na Sabato Kasika

**SEKTA** ya elimu imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali, ambazo kwa namna moja au nyingine, zinachangia kushusha na kukwamisha maendeleo ya sekta hiyo muhimu nchini.

Hata hivyo, baadhi ya changamoto ziko ndani ya uwezo wa jamii.

Hivyo basi, inashangaza kuona zikiendelea kuwapo bila ya jamii husika kuchukua hatua ya kuzitatua!

Muungwana amekuwa akijiuliza nini shida, je ni kukosekana kwa ubunifu, au elimu ya uraia?

Siku hizi imekuwa kama jambo la kawaida kukuta vyoo vya shule vimebomoka na kusababisha wanafunzi wajisaidie vichakani au katika vyoo vya nyumba za jirani na shule, bila jamii kuchukua hatua ya kujenga vipya.

Wakati shule zikiwa na changamoto hizo, viongozi wa serikali za vitongoji, vijiji, mitaa, kata wakiwamo madiwani na wale wa halmashauri wapo.

Kwa mfano wiki iliyopita, gazeti hili liliandika habari kuhusu wanafunzi 108 wa darasa la pili na la tatu wa Shule Msingi Nakalola, wilayani Masasi, mkoani Mtwara, kusomea chini ya miti ya miembe.

Wanafunzi hao wanasomea katika mazingira hayo kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa, hali inayosababisha hata uelewa wao wa masomo kuwa mdogo.

Shule hiyo ilianzishwa mwaka 1946, ina chumba kimoja cha ofisi ya walimu ambacho kinatumiwa pia na mkuu wao.

Muungwana anaona jamii haitakiwi kusubiri mazingira ya shule kuwa katika hali hiyo na badala yake ichukue hatua za kuyaboresha.

Wazazi na jamii ndio wenye jukumu la kusimamia shule kupitia kamati za shule ili kuhakikisha zinakuwa na miundombinu inayotakiwa, tena iliyo bora.

Inasikitisha kuona watoto wakisomea katika mazingira kama hayo wakati wananchi na viongozi wa maeneo husika hawachukui hatua, kana kwamba hawahusiki katika maendeleo ya shule yao.

Serikali inatoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne, kwanini jamii isiunge mkono juhudi hizo kwa kuchangia michango ya hali na mali kuboresha mazingira ya shule zao?

Hivi ni sahihi kuiachia serikali ifanye kila kitu, ubunifu wa viongozi wa maeneo husika uko wapi?

Umefika wakati sasa jamii na viongozi wa maeneo ambayo yana shule zenye changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa, vyoo na nyingine kutambua kwamba wana wajibu wa kushiriki kwenye utatuzi wa changamoto hizo.

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya watu ambao wamekuwa hawataki kuchangia maendeleo ya shule na hasa baada ya serikali kuja na utaratibu wa kutoa elimu bure.

Kwamba maadam serikali imetangaza elimu bure, hivyo hawawezi kuchangia chochote hata kama ni chakula shuleni kwa ajili ya watoto wao! Haya ni mawazo potofu, ambayo yanapaswa kuachwa.

Hebu fikiria, mzazi anaombwa kuchangia unga, maharage au chakula chochote kwa ajili ya mtoto wake ili asome vizuri, halafu anasema elimu ni bure, atakuwa yuko sahihi kweli kama si kupotosha?

Serikali imewapunguzia wazazi gharama kwa kuondoa ada, sasa kwanini wakatae kuchangia chakula?

Ninadhani haohao ndio, ambao hawaoni umuhimu wa kuchangia ujenzi wa miundombinu ya shule inapoharibika au ile mipya.

Kwa mtindo huo wa jamii kutojali au kutotambua kuwa inahusika, matokeo yake ndio hayo ya watoto kusomea chini ya miti na kukosa chakula kana kwamba shule hazina wenyewe.

Muungwana anaona wakati wa jamii kuelimishwa ni huu, lakini pia ni wakati kwa viongozi wa maeneo husika kuwa na ubunifu, kutobweteka huku mambo yakienda vibaya.

Kwa mfano shule inapokuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa, viongozi wanatakiwa kuhamasisha jamii kujitolea kwa hali na mali, isombe mawe, mchanga na maji ili kufanikisha ujenzi vyumba vipya.

Utaratibu huu ukitumiwa vizuri unaweza kusaidia kumaliza changamoto zinazozikabili shule mbalimbali nchini na hasa zile zilizo chini ya uwezo wa jamii za maeneo husika, badala ya kuendelea kuisubiri serikali kuu.

HABARI KITAIFA

# Wanaswa na risiti feki za TRA

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imewakamata wakazi wanne jijini Dodoma, ikiwatuhumu kujihusisha na utengenezaji wa risiti bandia za mashine za kielektroniki (EFD).

Vijana hao walikamatwa jana katika msako uliondeshwa na timu ya TRA uliongozwa na Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo, Charles Kichere.

Kamishna mkuu huyo aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa jana, kuwa walifanikiwa kuwanasa watuhumiwa hao wakiendelea na kazi ya kuzalisha risiti bandia.

Alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao kulitokana na taarifa za kiintelijensia ambazo mamlaka ilizipata.

Aliyataja majina ya watuhumiwa hao kuwa Jarome Julius, Saidi Julius (wote wakazi wa Kisasa Nyumba 300), Darif Saidi (23), mkazi wa Nzuguni C na Awadhi Suleiman, mfanyakazi na Meneja wa Kampuni ya Mafuta ya Lake Oil Kituo cha Kisasa.

Kichere alisema katika eneo la Kisasa Nyumba 300, watuhumiwa wawili wanaoishi huko, walikutwa na kompyuta moja, mashine ya kuskani na risiti mbalimbali za bandia.

Alisema kwenye eneo la Nzuguni, mtuhumiwa Saidi alikamatwa na mashine ya kutolea risiti za elektroniki moja, kompyuta moja na mashine ya kuskani moja.

Aliongeza kuwa mamlaka imebaini kuwa, wateja wakubwa wa risiti hizo za bandia ni madereva wa magari ya serikali ambao hununua risiti hizo za mafuta na huzipeleka kwa mwajiri wao ili kulipwa fedha.

"Mtandao huu wa wahalifu hawa ulikuwa Dar es Salaam, wamekuja Dodoma baada ya kuona tumewakamata wengine, na huku makao makuu wateja wao wengi wamehamia huku na wao wakaendelea na kuibia serikali, tumewakamata na tutaendelea kuwakamata," alisema Kichere.

Alidai kuwa moja ya mashine walizozikamata ni mali ya Kituo cha Mafuta cha Lake Oil cha Ilula na imekuwa ikitumika kila siku kutolea risiti za uuzaji wa mafuta.

"Watuhumiwa imeonekana kuwa hutengeneza risiti za bidhaa mbalimbali wakishirikiana na watu wenye nia mbaya ya kuibia serikali kwa kukwepa kodi," alisema.

Mamlaka hiyo ilishapiga marufuku vituo vya mafuta kutumia mashine ndogo za mkononi kuuza mafuta, ikivitaka kutumia mashine zilizounganishwa na pampu za mafuta.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na wafadhili wa mradi wa Kulijengea Bunge Uwezo, walipomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma jana. Wapili kulia ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson na (kulia) ni Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Kesi kigogo Takukuru kusikilizwa mfululizo

**Na Hellen Mwango**

KESI inayomkabili Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai, na wenzake ya kutakatisha fedha imepangwa kuendelea kusikilizwa mfululizo ushahidi wa Jamhuri Februari 19 mpaka 21, mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Awali, Wakili wa Serikali, Vitulis Peter, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri, lakini Jamhuri haikuwa na taarifa kama hakimu amemaliza likizo au la.

Alidai siku 14 zilizopita kesi hiyo ilipofikishwa mahakamani hakimu alikwenda likizo na mashahidi wanaotarajiwa kuitwa wanatoka mikoani.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, aliiomba mahakama kutoa ahirisho fupi ili kesi iendelee na pande zote mbili zijue hatima yake.

Hakimu Simba alisema upande wa Jamhuri upeleke mashahidi ili usikilizwaji uende kwa wakati.

Alisema itasikilizwa mfululizo Februari 19 mpaka 21, huku washtakiwa wakiendelea kukaa mahabusu.

Upande wa Jamhuri umeshaita mashahidi akiwamo Msajili wa Hati Msaidizi, kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Joanitha Kazinja na Msaidizi wa Hati Kanda ya Kaskazini wa wizara hiyo, Emmanuel Bundala.

Gugai na mwenzake watatu wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo, makosa 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Gugai anakabiliwa na kosa la kumiliki mali kinyume na kipato chake, ambapo alitenda kosa hilo kati ya Januari 2005 na Desemba 2015.

Inadaiwa akiwa Takukuru Dar es Salaam, Gugai alikuwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake, huku akishindwa kuzitolea maelezo.

# Bei ya mafuta yashuka tena

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imetangaza bei kikomo za mafuta ya aina ya petroli, mafuta ya taa na diseli zikiwa zimepungua kulinganisha na zile za mwezi uliopita.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany, ilieleza kuwa bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimepungua.

"Kwa mwezi Februari, bei za rejareja za petroli, dizeli na mafuta ya taa, zimepungua kwa Sh. 175/lita, Sh. 144/lita na Sh. 156/lita, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za mafuta hayo kwa Sh. 174.03/lita, Sh. 143.65/lita na Sh. 155.32/lita," alisema Mchany.

Alisema kupungua kwa bei katika soko la ndani kumetokana na kuendelea kushuka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa mikoa ya kaskazini, bei za mafuta zitaendelea kubaki kama ilivyo kabla ya mabadiliko hayo.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa kuanzia Januari 25, bei za rejareja ya petroli na dizeli katika mikoa ya kusini zilikokotolewa kulingana na gharama za mafuta yaliyopokewa katika bandari ya Mtwara.

Kutokana na hali hiyo, taarifa ilieleza kuwa bei za petroli na dizeli kwa mikoa hiyo ya kusini zitaendelea kuwa za kuanzia Januari 25.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. Ewura itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta," alisema Mchany.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika.

# Handeni yapata mwenyekiti mpya

**Na Boniface Gideon,** HANDENI

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, limemchagua Diwani wa Kwamatuku, Mustapha Beleko (CCM), kuwa mwenyekiti mpya wa halmashauri hiyo.

Uchaguzi huo wa mwenyekiti mpya ulifanyika jana, katika ukumbi wa halmshauri hiyo baada ya aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Ramadhani Diliwa, kujiuzulu udiwani Novemba 6, mwaka jana.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, msimamizi wa uchaguzi huo ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Handeni, William Makufwe, alisema Beleko alipata kura 22 kati ya 22 zilizopigwa na hakuna kura ya hapana.

Mafuwe aliongeza kuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) hakikusimamisha mgombea katika uchaguzi huo.

Mkurugenzi huyo alisema ilibidi kufanya uchaguzi huo kwa kuwa ni miezi mitatu nafasi hiyo imekuwa wazi tangu kujiuzulu kwa mwenyekiti huyo.

Baada ya kuchaguliwa, Beleko aliwashukuru madiwani wenzake kwa kumwamini na kumpa nafasi hiyo na kuwaahidi kutoa ushirikiano kwa kuwa tayari ameshapata uzoefu wa kuongoza baraza hilo akiwa kaimu mwenyekiti kwa kipindi cha miezi mitatu.

Alisema halmashauri hiyo ina changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa maji na miundombinu kwa baadhi ya maeneo na kuahidi kuhakikisha wanatekeleza mipango waliyojiwekea na kuwataka madiwani wenzake kushirikiana naye katika kutimiza azima hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo alijiuzulu nafasi hiyo kutokana na shinikizo kutoka kwa madiwani na wananchi baada ya kutangaza kipengele cha muhtasari kinachosema "uamuzi uliofanywa na Baraza la Madiwani ni makao makuu ya halmashauri kuwa Kabuku hayakuwa sahihi".

Hali hiyo ilisababisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, kuingilia kati na kutoa uamuzi kuwa makao makuu ya halmashauri yatakuwa Mkata.

# King'ora chazua taharuki bungeni

INATOKA UK.3

waita wabunge na kuwaomba kuingia katika ukumbi wa Bunge na baadaye saa 6:04 mchana, Bunge likarejea chini ya Spika Job Ndugai.

Kabla ya kuendelea na uwasilishaji wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na ile ya Kilimo, Mifugo na Maji, Spika Ndugai alisimama na kueleza kwamba mpaka wakati huo kulikuwa hakuna sababu ya wazi juu ya ving'ora hivyo kulia kwa kiasi hicho.

**NJE YA BUNGE**

Nje ya viwanja vya Bunge, Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Awesso, alisema: "Hiyo alamu (king'ora) inaashiria kama kuna moto lakini kikubwa tunaambiwa kama hujui kifo chungulia kaburi. Tumejifunza inahitajika elimu ya majanga si tu kwa wabunge hata maeneo mbalimbali kwa sababu moto ni jambo la dharura," alisema.

Aweso alisema bado kunahitajika elimu kwamba inapotokea hali hiyo ni kwa namna gani wanaweza kujiokoa, mfano mzuri ni wabunge na watu waliokuwa nje, hakuna utaratibu na hawajui wakae sehemu gani.

"Kwa kweli kunahitajika sana elimu ili kukabiliana na majanga yanapotokea, kwa hiyo sisi tulivyofundishwa linapotokea jambo kama hili, hamtakiwi kuwapo eneo hilo lazima mtoke," alisisitiza.

Mbunge wa Mtera (CCM), Livingstone Lusinde, alisema neno hatari kila mtu anajua namna ya kulitafsiri ndiyo wabunge wote walisimama wakaanza kukimbia.

"Wabunge wote wamezagaa eneo hili (viwanja vya Bunge) na hawajakimbilia Assembly Point (eneo la kukusanyikia wakati wa dharura). Kwa hiyo ningeshauri kuwekwe vibao vinavyoonyesha kukitokea hatari wabunge wakimbilie wapi.

"Kwanza mpaka sasa hivi, bado hatujaelezwa kilichosababisha alamu ilie na mpaka sasa hivi inalia lazima tusubiri watu wa zimamoto na majanga kutazama halafu baadaye watatuambia nini kimetokea," alisema Lusinde

Naye Mbunge wa Viti Maalumu (Chadema), Lucy Owenya, alisema: "Bado haijajulikana nini chanzo, kama kuna hitilafu ya umeme au vipi. Bado hatujaambiwa lakini ni jambo ambalo si la kawaida kutokea na hiyo imeleta taharuki ndiyo maana wabunge wote tuko nje."

**TAARIFA YA BUNGE**

Baadaye, Kitengo cha Habari na Mawasiliano cha Bunge kilitoa taarifa juu ya taharuki hiyo.

Katika taarifa hiyo, Bunge lilisema wataalamu walifuatilia na kujiridhisha kuwa hakukuwa na tatizo la moto ndiyo maana Bunge lilirejea na kuendelea na kikao kama kawaida.



Mafundi wa kampuni ya Estim, wakiendelea na kazi ya awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani, yenye urefu wa kilomita 19, ikiwamo ujenzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kesi mtuhumiwa mil. 7/- kwa dakika

INATOKA UK.2

Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile.

Katika kesi hiyo, Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Patrick Mwita akisaidiana na Mawakili wa Serikali, Esther Martin na Leornad Swai.

Wakili Mwita alidai kuwa, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 506, yakiwamo ya utakatishaji fedha, kuisababishia serikali hasara, kula njama, kutoa taarifa za uongo Mamlaka ya Mapato (TRA) na kughushi.

Kati ya mashtaka hayo, la kuisababishia serikali hasara linawakabili Yusufali na Paliwalla, ambao wanadaiwa kuwa, kati ya Januari 2008 na 2016, wakiwa ndani ya Jiji la Dar es Salaam, kwa makusudi waliwasilisha nyaraka za uongo TRA na kitendo hicho kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 24.30.

Khan anakabiliwa na mashtaka ya kutakatisha fedha 12; kwamba kati ya Januari 2008 na Januari 2016, anadaiwa kufanya miamala ya kuhamisha fedha haramu kutoka katika akaunti za Yusufali Sh. bilioni 24.30 huku akijua fedha hizo ni zao la kutakatisha.

Pia Yusufali anakabiliwa na kosa la kukwepa kodi TRA ya Sh. bilioni 24.30 kati ya Januari 2008 na Januari 2016 kupitia kampuni zake.

Mshtakiwa Yusufali na Paliwalla wanatuhumiwa kwa makosa 293 ya kughushi, kutoa taarifa za uongo 132, kutakatisha fedha 50.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Wakili Mwita alidai kuwa upelelezi umekamilika na wapo katika hatua ya mwisho ya kuwasilisha taarifa Mahakama Kuu Divisheni Maalum ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Hakimu Rwizile alisema kesi hiyo itatajwa Februari 28, mwaka huu na washtakiwa wote wapelekwe mahabusu.

**KORTI YA MAFISADI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) iliisajili kesi hiyo katika Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi.

Maofisa wa taasisi hiyo walifika kwenye mahakama hiyo jana mchana wakiwa na sanduku na mabokisi yenye nyaraka za kesi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari mahakamani hapo jana, Mkuu wa Sheria na Mashtaka wa Takukuru, Donasian Kessy, alisema wamefanikiwa kusajili kesi hiyo katika mahakama.

Alisema kusajiliwa kwa kesi hiyo katika mahakama hiyo kunafanya idadi ya kesi za aina hiyo kufika tatu tangu ilipoanzishwa na serikali ya awamu ya tano.

***Imeandikwa na Hellen Mwango, Enock Charles na Beatrice Shayo.***

# Mashamba ya Sumaye, MO Dewji

INATOKA UK.3

na ghala la mazao, anaambiwa hajaendeleza, mimi nasema unyang'anyaji huu siyo sahihi."

Alisema anafahamu kwamba Rais kubadilisha hati, anayo mamlaka hiyo na kwamba mpaka sasa ukiangalia hali ilivyo, ukiangalia akina Mo (Mohamed Dewji) wamenyanganywa mashamba yao ni lazima kamati ya uchunguzi iundwe ili kuangalia unyang'anywaji unavyoenda.

Suala hilo lilimwinua kitini Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, na kutoa taarifa kwa mzungumzaji huyo kwamba kinachoonekana kupigiwa kelele ni shamba la Sumaye.

Mlingwa amesema: "Hapa linalopigiwa kelele ni suala la shamba la Mheshimiwa Sumaye, ambaye taarifa zake ni hizi, alikuwa na shamba la ekari 326, amekaa nalo miaka 15, ameendeleza ekari sita, amejenga kibanda kimoja kina watu watatu.

"Katika shamba la Sumaye, kulikuwa na miembe mitatu, miche ya mahindi 76, mnazi mmoja, ng'ombe watatu, mbuzi 11, bata sita na kuku tisa."

Naye, Mbunge wa Mbozi (Chadema), Pascal Haonga, aliomba kutoa taarifa kwa mchangiaji ambaye ni Msigwa, akisema licha ya kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo ilikuwa ikiongozwa na Nape Nauye (Mtama-CCM) kuisifia, lakini imekuwa na utendaji mbovu, ndiyo maana Nape ameshinikizwa kujiuzulu.

Hoja ya Haonga, haikumpendeza Spika Ndugai na kumtaka kuthibitisha kama ni kweli Nape amejiuzulu kutokana na kushinikizwa na ameshinikizwa na nani.

Haonga alisema hana uthibitisho kwamba Nape ameshinikizwa kujiuzulu, lakini amedhani kuwa inaweza kuwa ni sababu; na kwa kuwa hawezi kuthibitisha, anafuta kauli yake.

Shamba la Sumaye lililofutiwa hati ni la ekari 426 ambalo liko Mvomero, mkoani Morogoro.

**NAPE: WEKENI AKIBA YA MANENO**

SIKU moja Nape kudaiwa kujiuzulu nafasi yake ya kamati, ameibuka na kuwataka wabunge wote kujifunza kuweka akiba ya maneno.

"Nataka niwaombe wenzangu, kwanza nimshukuru Waziri (Lukuvi) na nimshukuru Rais (Magufuli) kwa kulifuta (shamba namba 37 lililoko Maumbika, Mtama mkoani Lindi), hili shamba kwa niaba ya wakulima, sasa tutakwenda kuligawa vizuri.

Zaidi Nape akasema: "Kwa hiyo wakati mwingine tunapolishwa maneno na kuanza kusema, wekeni akiba ya maneno juu ya nani anapinga nini, na nani anasema nini, itatusaidia sana wanasiasa, ni vizuri tukiweka akiba ya maneno."

Nape alimshukuru Rais John Magufuli, huku akieleza kuwa anataka wabunge wajifunze kidogo kuweka akiba ya maneno hasa wanaposhutumiana bila sababu.

"Mheshimiwa Spika, wakati wa uchaguzi, sisi wa Jimbo la Mtama tulipeleka maombi ya kufuta baadhi ya mashamba makubwa yaliyotelekezwa. Namshukuru Rais, namshukuru Waziri wa Ardhi (Lukuvi), moja ya shamba lililofutwa ni shamba namba 37 liko Maumbika, Mtama Mkoa wa Lindi.

"Aliyelipeleka kuomba lifutwe ni mimi mbunge, nilimpelekea waziri, waziri akapeleka kwa Rais, Rais akafuta. Nataka niwaombe wenzangu, kwanza nimshukuru waziri na nimshukuru Rais kwa kulifuta hili shamba kwa niaba ya wakulima, sasa tutakwenda kuligawa vizuri,"alisema Nape.

# CRDB yawafuata wateja wake Mwanza

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATEJA wa benki ya CRDB Mkoa wa Mwanza, wameishauri benki hiyo kupanua na kuboresha huduma zake za kifedha kwa kuhakikisha zinawafikia wananchi wengi walioko vijijini, kwa kuwapatia mikopo yenye riba nafuu.

Ushauri huo ulitolewa wakati wa hafla iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya kumtambulisha rasmi Mkurugenzi Mtendaji mpya wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, kwa wateja wake wa Mwanza ikiwa ni kuhakikisha lengo la benki hiyo linakidhi na kuwasaidia wajasiriamali kuongeza mzunguko wa kipato chao pamoja na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Ally Hussen, alisema: "Benki hii ilianzishwa ikiwa na mtaji wa Shilingi milioni 54, lakini hadi Dk. Kimei anaondoka ameicha ikiwa na Shilingi trilioni 6."

Alisema benki hiyo chini ya Dk. Kimei imekuwa ni chachu ya kuongeza pato la taifa, ambapo hadi mwaka 2015, kodi yake kwa serikali ilifikisha Sh. bilioni 44 nje na kodi ya wafanyakazi, hivyo kuifanya CRDB kuwa ni ya kwanza kulipa kodi kubwa.

Kwa upande wake Nsekela alisema Mwanza ni kitovu cha uchumi wa nchi, hivyo benki hiyo inatambua umuhimu wa mkoa huo kwa wateja wake wakiwamo wafanyabiashara wakubwa na wadogo.

Aidha, Nsekela alisema CRDB ina matawi yasiyopungua 265, inamitandao isiyopungua 550, pia inatoa huduma mbalimbali kupitia mawakala zaidi ya 5,000,huduma zote zinawalenga wateja wa mijini na vijijini na benki hiyo imeendelea kupanua wigo wa kutoa huduma kwa jamii pamoja na kuanzisha kampuni tatu, ikiwamo inayotoa huduma ya bima kwa Watanzania.

ITV Daima
Kwa matangazo na Burudani saa 24

# Mahakama yaanzisha mpango kulea wanafunzi

**Na Lydia Churi,** MAHAKAMA

MAHAKAMA ya Tanzania imeanzisha mpango wa kushirikiana na vyuo na shule za sekondari katika kuwalea na kuwatambua wanafunzi wenye vipawa, tabia na maadili mema, ambapo huwafuatilia na kuwafanyia tathmini ili baadaye waje kufanya kazi na mahakama.

Lengo lingine ni baadaye kufanyakazi maeneo mengine katika sekta ya sheria katika Wiki ya Utoaji wa Elimu ya Sheria inayoendelea jijini Dodoma, wanafunzi kutoka baadhi ya vyuo vikuu na shule za sekondari nchini wanashiriki kwa kujifunza masuala ya mbambali yanayohusu sheria pamoja na taratibu za kimahakama jijini.

Akizungumza na wanafunzi, walimu na washauri wa wanafunzi hao, kwa niaba ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Latifa Mansoor, alisema kupitia mpango huo wa Mahakama, watumishi watakaoajiriwa na Mahakama ni wale tu wenye tabia na maadili mema na wenye uwezo uliothibitika ili waweze kutoa huduma bora hapo baadaye.

**Tunawaalika katika maadhimisho haya ili kubadilishana uzoefu na pia mjifunze masuala mbalimbali ya sheria ili muwe na ufahamu zaidi.**

Jaji Mansoor alisema baadhi ya mambo ambayo Mahakama inashirikiana na vyuo na shule hizo ni kuwa na uhusiano wa karibu na kuwa na fomu za ufuatiliaji wa mienendo ya maadili na taaluma za wanafunzi ambazo hujazwa na kutumwa kwa Mahakama ya Tanzania mara mbili kwa mwaka.

Aliyataja mambo mengine ya ushirikiano ni pamoja na uanzishwaji wa klabu na utoaji wa elimu ya sheria shuleni pamoja na mpango wa kuwazawadia fursa za masomo na zawadi nyingine wanafunzi wenye vipaji na maadili mema.

Aidha, Jaji Mansoor aliwataka walimu na washauri wa shule hizo kuwalea na kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanakuwa na ubora katika taaluma, tabia na maadili. Aliongeza kuwa wanafunzi wa vyuo hufuatiliwa na kumbukumbu zao huhifadhiwa kwa mahitaji ya baadaye ikiwamo ajira kwa watumishi wa Mahakama na Sekta ya Sheria kwa ujumla.

Aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii na kuwa na tabia na maadili mema kwa manufaa yao na ya taifa kwa ujumla." Tunawaalika katika maadhimisho haya ili kubadilishana uzoefu na pia mjifunze masuala mbalimbali ya sheria ili muwe na ufahamu zaidi," alisema.

Kufuatia mpango huu wa ushirikiano, Mahakama ya Tanzania inatarajia kuwa na huduma zilizoimarika, watumishi kufanya kazi kwa ubora wa hali ya juu na kwa kuzingatia utawala wa sheria, na vitendo vya rushwa na ukiukwaji wa maadili kupungua.

Vyuo ambavyo mpaka sasa vimeingia kwenye ushirikiano na Mahakama ya Tanzania ni vyuo vikuu vya Dar es Salaam, Mzumbe, Dodoma, Ruaha, Iringa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.



Mfanyabiashara mdogo akinadi bidhaa zake kwa abiria katika makutano ya Barabara ya Morogoro na Mandela, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# RC: Bodaboda atakayebeba mwanafunzi wa kike kukiona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI mkoani Shinyanga imepiga marufuku waendesha pikipiki (bodaboda) kubeba wanafunzi hasa wa kike wa shule za msingi na sekondari.

Katazo hilo limetolewa baada ya kubainika wao ndio chanzo kikubwa cha mimba kwa wanafunzi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellack, ndiye aliyetoa tangazo hilo kwenye maadhimisho ya miaka 42 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) yaliyoandaliwa na Jumuiya ya Wanawake (UWT) Mkoa wa Shinyanga.

Alisema kila dereva wa bodaboda anatakiwa kuacha mara moja kuwabeba wanafunzi hao wa kike, ili serikali ijiridhishe ni chanzo gani kingine ambacho kimekuwa kikisababisha wanafunzi wa kike kubeba mimba wakiwa masomoni.

Tellack alisema kama bodaboda atabainika au kukutwa akiwa amembeba mwanafunzi, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake, nakuongeza kama kutakuwa na changamoto nyingine inayosababisha wanafunzi hao kukubeshwa mimba, serikali itakabiliana nayo.


"Marufuku waendesha pikipiki mkoani hapa kuwabeba wanafunzi katika vyombo vyao, kwa kuwa inaonyesha kuwa ndio chanzo kikubwa cha wanafunzi na watoto wa kike kubeba mimba, tunataka kujua mara baada ya bodaboda kutowabeba wanafunzi chanzo kingine kitakuwa ni nini," alisema Tellack.

Hata hivyo, alisema pia wazazi nao wamekuwa wakichangia kuwa na ongezeko la mimba za ututoni kutokana na kutokuwa wakweli kwa watoto wao juu ya kutoa elimu ya uhusiano.

Pia alisema kuwa, anachukizwa na wazazi pamoja na mashirika yanayotoa huduma za kiafya za kuwahamasisha watoto kutumia mipira ya kiume (kondomu) na sindano za kuzuia mimba kwa kuwa wanafunzi na watoto wadogo wamekuwa wakifanya ngono wakijua kuwa watatumia vifaa vya kuzuia mimba.

Aidha, aliwataka kutoa elimu ya madhara ya vijana ama watoto wadogo kujihusisha au kushiriki kwenye mapenzi katika umri mdogo kuwa ni hatari kwa maisha yao kwa sababu wanaweza kupoteza maisha.

# Mbunge alia kero ya maji jimboni kwake




Habari na Augusta Njoji

MBUNGE wa Mbarali (CCM), Haroon Pirmohamed, amehoji serikali lini itapeleka huduma ya maji katika maeneo ya jimbo hilo kutokana na mradi wa Bwawani kusuasua kujengwa.

Akiuliza swali hilo jana bungeni, Mbunge huyo alisema maeneo ya kata za Mahogole, Mwatenga, Kongoro, Utengule-usangu, Luhanga, Itambo, Chimala, Ihahi, Imalilo, Igaua, Miyombweni, Mapogoro na mji wa Rujewa hayana maji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema Halmashauri ya Wilaya Mbarali kupitia programu ya maji vijijini tangu mwaka 2012 imefanya usanifu katika vijiji 16 na kujenga miradi ya maji katika vijiji vya jimbo hilo.

**Hadi sasa mradi huu umegharimu Sh. bilioni 2.9, taratibu za kutangaza awamu ya tatu zinaendelea na awamu ya nne na ya tano zitatangazwa baada ya awamu tatu kukamilika.**

Alitaja vijiji hivyo kuwa ni Simike, Udindilwa, Igurusi, Chimala, Mkunywa na Ubaruku.

"Pamoja na kukamilisha miradi hiyo, halmashauri inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya Luduga-Mawindi, ambao hadi utakapokamilika utagharimu Sh. bilioni tisa na utahudumia vijiji sita vya kata za Mawindi na Ipwani," alisema.

Alifafanua kuwa mradi huo utatekelezwa kwa awamu tano na kwa sasa utekelezaji unaendelea katika awamu ya kwanza ambayo imefikia asilimia 98 na awamu ya pili imefikia asilimia 75.

"Hadi sasa mradi huu umegharimu Sh. bilioni 2.9, taratibu za kutangaza awamu ya tatu zinaendelea na awamu ya nne na ya tano zitatangazwa baada ya awamu tatu kukamilika," alisema.

Aweso alisema kwa lengo la kuboresha huduma ya maji, mji wa Rujewa pia umejumuishwa katika miji itakayonufaika kupitia fedha za mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 500 kutoka serikali ya India ambazo zitatumika katika ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akiteta jambo na Spika wa Bunge, Job Ndugai, jijini Dodoma. **PICHA: OWM**

## Serikali kufunga migodi hatarishi

SERIKALI imesema haitasita kuyafunga maeneo ya migodi yatakayobainika kuwa ni hatarishi na yanakiuka kanuni za usalama.

Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, alisema hayo jana Bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Maryam Msabaha.

Katika swali lake, Msabaha alitaka kujua ni lini serikali itawapatia zana za kisasa na elimu ya kutosha wachimbaji wadogo.

Akijibu swali hilo, Nyongo alisema katika kuhakikisha uchimbaji wa madini nchini unafuata taratibu za usalama, afya na utunzaji wa mazingira, serikali imeanzisha Tume ya Madini ambayo ina ofisi za Ofisa Madini Wakazi (RMO) mikoa yote na kila eneo lenye shughuli za uchimbaji.

"Wachimbaji wengi katika migodi ya wachimbaji wadogo amekuwa hawazingatii tahadhari za usalama wakati wa shughuli za uchimbaji," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali itazidi kuweka msisitizo kwa wachimbaji hao kuzingatia Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira wakati wa uchimbaji.

Pia alisema Wizara ya Madini ilikuwa ikitoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo wa madini lakini ilibainika kuwa baadhi ya wachimbaji waliopatiwa ruzuku walitumia kinyume cha maelekezo na makubaliano.

Alisema serikali inaangalia utaratibu mzuri wa kuwasaidia wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuzishawishi taasisi za fedha kuwakopesha wachimbaji wadogo.

Aliwashauri wachimbaji kutunza kumbukumbu za uzalishaji na mauzo ya madini ili kuzishawishi taasisi za fedha kuwakopesha.

# Mwongozo kubadilishana wafungwa wabainishwa

BUNGE limeelezwa kuwa suala la kubadilishana wafungwa baina ya nchi moja na nyingine huongozwa na mkataba wa makubaliano ulioingiwa baina ya nchi husika.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Hamad Masauni alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kasulu Mjini (CCM), Daniel Nsanzugwanko.

Nsanzugwanko katika swali lake, alisema wafungwa wakimbizi toka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo wamekuwa wakijaza mahabusu na magereza nchini.

"Je, kwa nini serikali isikubaliane na nchi za Burundi na DRC kubadilishana wafungwa ili wakimbizi hao wafungwe katika nchi zao?" alihoji.

Mbunge huyo pia alihoji kuwa wafungwa wa aina hiyo wanapokuwa mahabusu na Magereza Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) linachangia gharama kwa kiasi gani.

"Je, UNHCR imechangia fedha kiasi gani kwa wafungwa wakimbizi waliofungwa au kuwekwa mahabusu nchini kuanzia mwaka 2017/18?" alihoji Nsanzugwanko.

Akijibu maswali hayo, Masauni alisema lengo la mkataba huo ni kumpa fursa mfungwa anayetumikia kifungo chake gerezani kutumikia sehemu ya kifungo chake kilichobaki katika nchi yake.

"Ieleweke kuwa ni utamaduni wa kisheria duniani kwamba mahabusu na mfungwa bila kujali kama ana hadhi ya ukimbizi, wanapopokelewa na kuhifadhiwa katika magereza, jukumu la kuwatunza hufanywa na serikali ya nchi husika," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa kufuata sheria na kanuni za magereza zilizopo ambazo kimsingi zimeipa serikali jukumu hilo. Aidha alisema kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Magereza hakuna mahabusu au mfungwa mkimbizi kwa kuwa wahalifu wote hupokewa kwa hati kutoka mahakama zenye utambulisho wa hadhi ya mahabusu au mfungwa tu.

Hata hivyo, alisema suala la UNHCR kuchangia gharama za kuwatunza wafungwa na mahabusu wanaodaiwa kuwa wakimbizi huwa halipo na halifanyiki.

"Kwa sababu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za magereza zilizopo hazijaainisha kumtambua mahabusu au mfungwa mkimbizi katika magereza zetu,"alisema.

# Ubelgiji yatoa bil. 3/- utafiti wa ndizi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI ya Ubelgiji imetoa zaidi ya Sh. bilioni 3 kwa Chuo cha Afrika cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, (NM-AIST), zitakazotumika kujenga kituo kikubwa mahiri cha utafiti wa ndizi mshale.

Kituo hicho kitatumiwa na wakulima kuomba ushauri na kubadilisha kilimo chao cha mazoea.

Mradi wa ujenzi wa kituo hicho ni wa pili wa kuwezesha mradi wa matumizi endelevu ya rasilimali kwa maendeleo ya jamii Kanda ya Kaskazini (VRIL).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo jana, Makamu Mkuu wa NM-AIST, Profesa Emmanuel Luoga, alishukuru serikali ya Ubelgiji kwa kuwaamini na kuwapatia fedha hizo zitakazonufaisha wananchi wa kanda hiyo hasa nyanja ya uzalishaji wa ndizi mshale.

Alisema mradi huo ulianza miaka sita nyuma na sasa baada ya tathimini ya awamu ya kwanza wameona kuna haja kuendelea kusaidia mradi ili wananchi wapelekewe matokeo ya utafiti uliofanyika nyanja mbalimbali na kutumia kwa ajili ya kuzalisha kwa tija.

Alitaja baadhi ya tafiti zilizofanyika awamu ya kwanza na kugusa jamii ni teknolojia ya kutibu maji taka na kuyatumia kwa matumizi mengine na kwa upande wa sekta ya kilimo, utafiti ulijikita katika uzalishaji wenye tija wa zao la ndizi mshale ambazo ni chakula kikuu kwa wakazi wa Kanda ya Kaskazini.

"Kupitia awamu hii ya pili ya mradi uliowezesha tafiti za masuala mbalimbali, wananchi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini hasa Arusha na Kilimanjaro wategemee kunufaika na kituo kikubwa kitakachojengwa chuoni hapa ambacho kitafanya utafiti mahiri wa zao hili na kutoa ushauri kwa magonjwa ya ndizi na uzalishaji wake," alisema.

Naye Mratibu wa Mradi wa VRIL, Profesa Karoli Njau, alisema mradi huo awamu ya kwanza ulianza mwaka 2013 hadi 2018 na ulijikita maeneo matatu ya kilimo, uchafuzi wa mazingira, maji na matumizi ya maji.

Alisema katika awamu hiyo zaidi ya Sh. bilioni 3.5 zilitumika kuendesha tafiti katika maeneo hayo na kujenga uwezo kwa walimu wa ngazi ya uzamivu ambao walipelekwa kusoma nchini Ubelgiji na kufanya utafiti wao nchini kupitia chuo hicho.

# UWT yahimiza wanawake kugombea nafasi uongozi

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WANAWAKE wilayani Longido, wametakiwa kujitokeza kuwania nafasi za uongozi kwa uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu na uchaguzi mkuu wa mwakani, ili kuepukana na mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke kuwania nafasi ndani ya jamii.

Katibu wa UWT Wilaya ya Longido, Judith Laizer, alisema hayo wakati akizungumza na wanawake waliokuwa wakifanya usafi wa mazingira katika Shule ya Sekondari ya Longido juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho miaka 42 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi.

Alisema jumuiya hiyo ilitenga siku ya juzi kufanya usafi ndani ya jamii ikiwamo taasisi mbalimbali kama vile shule, hospitali na hata maeneo ya stendi.

Alisema kumekuwa na mila kandamizi kwa jamii kumdharau mtoto wa kike au mwanamke katika kuongoza jamii na kuwataka wanawake kuchukua fomu za kugombea fursa za uongozi katika Serikali za Mitaa mwaka huu, na mwakani wagombee nafasi za ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu.

**Nikiwa kama Mkurugenzi wa Uchaguzi upande wa chama, nasema hivi, nitapitisha majina, chukueni fomu, jazeni muone.**

"Kwa kweli nitafurahi kuona mnakuwa wenyeviti wa vijiji na madiwani wa kata pamoja na ubunge. Lakini pia naomba msiwaangushe wanawake wenzenu pale wanapochukua fomu za kuwania nafasi, wapigieni kura na kubwa zaidi hakikisheni mnasimamisha viongozi wanaokubalika na jamii," alisema.

Mkazi wa Kata ya Longido, Namnyaki Saibulu, alisema wanawake wengi wanajaza fomu kwa lengo la kuwania nafasi ndani ya jamii, lakini cha kushangaza majina yao yanakatwa.

"Tunajaza fomu, tunakubalika na jamii lakini bado majina yetu yanakatwa," alidai.

Alisema wanawake wengi kwa sasa wamekata tamaa kuwania nafasi kutokana na majina yao kutopitishwa kuwania fursa za uongozi, hivyo wanaiomba serikali kutenda haki sawa kwa jamii.

"Tupeni nafasi za uongozi tunaweza, msitutumie kwenye kupiga kura tu, na sisi tunahitaji nafasi, sasa tukiomba mtupe jamani," alieleza.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Longido, Simba Gaddaf, alisema awamu hii atahakikisha wanawake wanaochukua fomu majina yao hayatakatwa na watapewa nafasi za uongozi.

"Nikiwa kama Mkurugenzi wa Uchaguzi upande wa chama, nasema hivi, nitapitisha majina, chukueni fomu, jazeni muone," alisema.

Alieleza anatambua mila za jamii ya Kimasai hawapendi kuwapa wanawake na vijana nafasi za uongozi na wanaopinga asilimia kubwa ni wazee wa kimila Malaigwanani, lakini na sisi tunafuata katiba inasemaje.

"Ifike pahali mila kandamizi kwa wanawake na vijana zipuuzwe na wahakikishia hadi niondoke Longido tutakuwa na madiwani, wenyeviti na hata wabunge wanawake," alisisitiza.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Boay, mkoani Manyara, wakibeba saruji iliyotolewa juzi na Mbunge wa Babati Vijijini, Vrajlal Jituson ambaye aligawa mifuko 3,000 kwa ajili ya shule zote za jimboni. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC awataka watendaji kutanguliza maslahi ya taifa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewataka maofisa watendaji wa kata na vijiji kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na kuweka mbele maslahi ya taifa ya kuwahudumia wananchi.

Alitoa rai hiyo wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha maofisa tarafa na maofisa watendaji wa kata na vijiji wa halmashauri za Arusha Dc na Meru zote za wilayani humo.

Kikao hicho kililenga kuwakumbusha na kuwajengea uwezo wataalamu katika utekelezaji majukumu yao ya kuwahudumia wananchi.

Aliongeza katika wilaya hiyo wamekubaliana kuanzisha programu maalumu ya mafunzo kwa watendaji kwa kushirikiana na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilichoko wilayani humo, ambapo mafunzo hayo yatawaongezea ujuzi wa kazi.

Alisema maofisa wanaajiriwa kutoka kwenye kada tofauti, jambo ambalo wakati mwingine, linasababisha changamoto ya kukwamisha baadhi ya kazi.

Aidha, alieleza kupitia mafunzo hayo yatawajengea uelewa wa pamoja na kufahamu majukumu yao na mipaka ya kazi kwa kuwa na uadilifu, kujiamini, kuongeza morali ya kazi, pamoja na kuweka mbele uzalendo kwa maslahi ya taifa.

"Tumegundua kuna umuhimu kupata mafunzo kwa watendaji wote, yatakayowakumbusha na kuwawezesha kutambua namna sahihi ya utekelezaji wa kazi zetu za kila siku, hii imetokana na baadhi ya watendaji kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa usahihi," alisema.

Alisisitiza watendaji wa serikali wanatakiwa kusimamia hali ya usalama katika maeneo yao ya kazi kwa kutambua wageni wanaoingia na kutoka katika maeneo yao ya kazi, sambamba na kuhamasisha wananchi kushiriki kuchangia maendeleo katika maeneo kwenye jamii husika.

"Kazi kubwa ya mwaka huu ni kujenga vyumba vya madarasa, ninawaomba maofisa watendaji, tuelekeze nguvu zetu kuhamasisha jamii kujikita zaidi katika kujenga madarasa na mimi nataka nione kila tarafa ina kuwa na shule ya kidato cha tano na sita na kila kata kuwa na kidato cha kwanza hadi cha nne," aliongeza.

Kwa upande wa wakurugenzi wa halmashauri hizo, (Meru), Emanuel Mkongo, (Arusha Dc), Dk. Wilson Mahera, waliwataka maofisa watendaji kusimamia shughuli za maendeleo kwa kuendana na kasi ya serikali, kuwa waadilifu katika kutekeleza kazi kwa kutoa huduma sawa kwa wananchi na kusimamia haki.

# CCM waadhimisha miaka 42 kusafisha eneo la hospitali

**Na Paul William,** ROMBO

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Rombo, kimeadhimisha sherehe za miaka 42 tokea kuzaliwa kwake kwa kufanya usafi katika eneo litapojengwa Hospitali ya Wilaya itakayogharimu Sh. bilioni 7.5.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alisema ujenzi wa hospitali hiyo ya wilaya ilikuwa ni ndoto ya muda mrefu kwa wananchi wa Rombo, lakini kwa kutambua umuhimu wa afya na kutekeleza kwa vitendo ilani ya uchaguzi serikali imeamua kutimiza ndoto hiyo ya wananchi.

**CCM imejizatiti kuhakikisha inafanya vizuri na kuwataka wanachama na wananchi kuhakikisha pale walipokosea mwaka 2014 na 2015 hawarudii makosa.**

"Leo tumezindua sherehe za miaka 42 ya kuzaliwa kwa chama wilayani Rombo kwa kufanya usafi eneo hili litakalojengwa hospitali ya wilaya wanachama na wananchi wa Rombo mnapaswa kutambua hospitali hii itakuwa na faida kubwa kwenu, hivyo mnapaswa kutoa ushirikiano unapohitajika ili kuhakikisha ujenzi huu unakamilika mapema," alisema Mabihya.

Akizungumzia uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, aliwataka wanachama kuondoa ubinafsi pamoja na kuepuka makundi.

Alisema kuwa CCM imejizatiti kuhakikisha inafanya vizuri na kuwataka wanachama na wananchi kuhakikisha pale walipokosea mwaka 2014 na 2015 hawarudii makosa.

Mabihya alisema wananchi wanawajibu wa kuchagua kiongozi atakayewatumikia na kuwaletea maendeleo kupitia chama ambacho kikiahidi kinatekeleza kwa vitendo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rombo, Anthony Tesha, aliwataka Wanaccm kujijengea tabia ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akining'inia kwenye bajaj, iliyoko kwenye mwendo, katika eneo la Mbezi Mwisho, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake na uvunjifu wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**






# Serikali yaipa Rombo bil. 1.5/- ujenzi hospitali

**Na Mary Mosha,** ROMBO

SERIKALI imetoa Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Rombo, itayosaidia kuondoa changamoto za huduma ya afya katika wilaya hiyo.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, jana wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa hospitali hiyo, ambapo alisema hadi kukamilika kwake hospitali hiyo itagharimu Sh. bilioni 7.5.

Alisema kwa awamu ya kwanza serikali imeshatoa Sh. bilioni 1.5 ambazo zitatumika kujenga majengo saba muhimu likiwamo la mama na mtoto pamoja na wodi ya kinamama ili kuruhusu hospitali hiyo kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

"Tunatambua wananchi mmekuwa mkilazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya, lakini kukamilika kwa hospitali hii ambayo tunategemea mwakani ianze kutoa huduma itaondoa adha ya kutembea umbali mrefu," alisema Dk. Mghwira.

Alisema hospitali hiyo inayojengwa Kata ya Kirongo Samanga, serikali imeshaanza kuaandaa wataalamu wa afya watakaoanza kutoa huduma mara moja itakapokamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, aliwataka wananchi wa Rombo kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuwaletea maendeleo.

# Hai wamwomba Magufuli kufuta hati

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI wilayani Hai, imemwomba Rais John Magufuli, kufuta hati za matumizi ya eneo la Mashine Tools lenye vitalu 52 kutokana na maeneo hayo kutoendelezwa wala kulipiwa kodi.

Eneo la Mashine Tools lilitengwa na serikali kwa ajili ya viwanda, lakini halijaendelezwa wala kulipia kodi licha ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kutoa agizo hilo.

Akisoma utekelezaji wa ilani ya CCM kwa miaka mitatu, Mkuu wa Wilaya, Lengae ole Sabaya, alisema ni vyema ikiwa itampendeza Rais Magufuli kufuta hati hizo, na kukabidhi Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Alisema serikali imefikia uamuzi huo baada ya baadhi ya wamiliki wa maeneo hayo kukaidi agizo la Waziri Lukuvi lililowataka kulipia kodi, ambapo hadi kufikia sasa viwanja vitatu kati ya 52 ndivyo vilivyolipiwa kodi.

"Serikali haitawavumilia tena... tunataka kila mmoja awajibike kwa namna anavyoweza ili kulikomboa taifa katika kulipa kodi...tutaandika ombi maalumu kwa rais kutusaidia kufuta hati na kurudisha kwa TIC," alisema.

Sabaya alisema kwa kiwango kikubwa serikali imetekeleza jukumu la kuwahudumia wananchi kwa kufuata miongozo ya ilani ya chama ya mwaka 2015/20.


Alisema katika sekta ya afya, serikali imeboresha huduma za afya kwa kujenga na kukarabati vituo vya afya na zahati pamoja na kununua dawa.

Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, alisema kuwa halmashauri ya wilaya hiyo, imeongeza ukusanyaji wa mapato kwa kasi ukilinganisha miaka ya nyuma.

"Wilaya ya Hai imekuwa miongoni wa wilaya zilizopo kwenye nafasi ya 10 bora hapa nchi, kwa kukusanya mapato kwa wingi," alisema Sabaya.

Nao baadhi ya wananchi wakazi wa wilaya hiyo, wakizungumzia uamuzi wa serikali hiyo, Elinas Msao na Hawa Hamis, walisema ikiwa maeneo hayo yatapatiwa wawekezaji watapata ajira sambamba na kukuza uchumi wa nchi.

"Kituo hiki kinaweza kuwa msaada kwa jamii inayoizunguka, hivyo ni vyema ikimpendeza Rais kulifanyia kazi na kufuta hati hizo au kuwaburuza mahakamani," alisema Hawa.



Ukurasa 19

**RAIS TSHISEKEDI KUFANIKISHA MAZISHI YA TSHISEKEDI DRC**

**MAKALA:**

Venezuela; Rais Maduro ajipanga kwa uchaguzi mpya wa Bunge



Ukurasa 18

**KIMATAIFA:**



**Mkataba wa kimataifa makombora masafa ya kati wasambaratika rasmi**

Ukurasa 20

siasa

JUMATANO FEBRUARI 6, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



**Salamu za Dk. Bashiru kwa wanasiasa zisibezwe**

Ukurasa 14

# EAC na changamoto ya mgogoro wa wanachama Rwanda, Burundi

**Na Mashaka Mgeta**

NI rahisi kusema ya kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yenye nchi sita zilizo wanachama, inahitaji kutatua changamoto zinazoikabili wakati ikijielekeza kuwa shirikisho, miongoni mwa hizo ni mgogoro wa kidiplomasia unaozikabili Rwanda na Burundi.

Mbali na Rwanda na Burundi, EAC inaundwa pia na Tanzania, Kenya, Uganda na Sudani Kusini.

Lakini kwa takribani miaka minne sasa, uhusiano wa kidiplomasia kati ya Burundi na Rwanda umedhoofika kiasi cha kutotambuana kuwa washirika wa maendeleo.

Mzozo wa kidiplomasia kati ya nchi hizo umekuwa changamoto kwa kigezo kwamba, dira ya EAC inaeleza kuwa ni

ENDELEA UK 16



Rais Pierre Nkurunziza

UCHAMBUZI

# MAADHIMISHO YA MIAKA 42 YA CCM

## ■ Salamu za Dk. Bashiru kwa wanasiasa zisibezwe

**Na Sabato Kasika**

HISTORIA inaonyesha kuwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kilizaliwa Februari 5, 1977 baada ya kuvunjwa kwa vyama vya Tanganyika African National Union (TANU) na Afro-Shirazi Party (ASP).

Hatua hiyo inatokana na Katiba ya CCM, katika Azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa wa Pamoja wa TANU na ASP wa Januari 21 mwaka 1977, ambapo kwa kauli moja ilitamkwa kuvunjwa kwa Tanganyika African Union (TANU) na Afro-Shirazi Party (ASP) Februari 5 mwaka 1977 na kuundwa kwa chama kipya chenye uwezo wa mwisho katika mambo yote kwa mujibu wa Katiba.

Lengo la kuunganisha vyama hivyo na kuzaliwa CCM lilikuwa ni kuendeleza utamaduni uliokuwa umeanza huko nyuma wa kuunganisha nguvu kwa ajili ya kujiimarisha katika mapambano.

Chama cha ASP kwa upande wa Zanzibar kilitokana na muungano wa African Association (AA) na Shirazi Association (SA), ikiwa ni kuunganisha nguvu za wanyonge katika mapambano ya kuuondoa usultani na utawala wa kikoloni wa Kiingereza.

Kwa upande wa Tanzania Bara, TANU ilizaliwa kutokana na kujibadilisha kwa Tanganyika African Association (TAA) kutoka jumuiya ya kutetea maslahi ya kijamii na kuwa chama cha siasa.

Uhuru wa Tanganyika wa Desemba 9 mwaka 1961 na Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964, kulifanya TANU na ASP vikamilishe kazi ya ukombozi wa nchi hizi mbili kutoka katika makucha ya ukoloni mkongwe na usultani.

Muungano wa TANU na ASP ndio uliowezesha CCM kuwa chama chenye nguvu, imara na madhubuti, hivyo kuwa chenye uwezo wa hali ya juu wa kuwaunganisha Watanzania.

Aidha, CCM kimeweza kuwaongoza wananchi katika mapambano ya kitaifa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kufuatana na mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza ndani na nje ya nchi.

Kimeendelea kupewa dhamana ya kuunda serikali na kushika dola tangu 1977 chini ya mfumo wa demokrasia ya chama kimoja hadi sasa katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, kufuatia mageuzi yaliyoidhinishwa na marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1992.

Aidha, tangu kuanzishwa kwa CCM, Februari 5 ya kila mwaka, chama hicho kimekuwa kikiadhimisha kumbukumbu ya kuzaliwa kwake, ambapo jana kilitimiza miaka 42 tangu kianzishwe mwaka 1977.

Maadhimisho ya miaka 42 ya CCM yalianza tangu wiki iliyopita kwa wanachama kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo usafi na nyingine nyingi, ambapo safari hii yamefanyika kila mkoa, tofauti na miaka mingine.

Mwaka huu maadhimisho hayo yana kaulimbiu isemayo: 'Tujipange kwa Pamoja ili Kuleta Ufanisi Katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa,' ambapo Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally alitoa salamu.

**SALAMU**

Katika salamu zake za maadhimisho ya mwaka huu, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Ally anawatahadharisha wanasiasa kuwa makini na kauli wanazotoa zenye lengo la kuchonganisha vyombo vya ulinzi na usalama na kwamba hakuna atakayewavumilia.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

> Miongoni mwa mambo yanayotajwa kama kikwazo kwa amani ni kutoheshimiwa kwa utawala wa sheria, katiba na kubadili sheria kwa maslahi binafsi.

Aliitoa kauli hii mkoani Dodoma katika uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 42 ya kuzaliwa kwa chama hicho yaliyofanyika katika Kata ya Nzali, jimbo la Chilonwa Wilaya ya Chamwino.

Akizindua maadhimisho hayo ambayo yamepangwa kufanyika katika kipindi chote cha mwezi huu, Dk. Ally anasema:

"Wapo baadhi ya wanasiasa wanaotumia matukio yenye utata ili kuvichonganisha vyombo vya ulinzi na usalama ndani na nje ya nchi... ni vyema wanasiasa hao wakaacha kuyatumia matukio hayo kutafuta umaarufu wa kisiasa," anasema.

Kauli hiyo inalenga kuhimiza amani ili Watanzania waweze kufanya shughuli zao za maendeleo bila hofu, hivyo wanasiasa hawana budi kuzingatia hilo kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Ni kauli ambayo inaendana na ile aliyoitoa mwenyekiti wa chama hicho Dk. John Magufuli katika maadhimisho ya miaka 41ya CCM.

Katika maadhimidho hayo, Rais Magufuli aliwapongeza viongozi, wanachama na wapenzi wote wa CCM na kuwahimiza kutunza amani na umoja, kuchapa kazi kwa maslahi ya nchi yao na serikali inayoongozwa na CCM.

Kupitia ukurasa wake Twitter President JPM aliaandika: "Nawapongeza viongozi, wanachama na wapenzi wa wote wa CCM kwa kutimiza miaka 41. Tunaposherehekea mafanikio yetu tuendelee kutunza amani na umoja wetu, tuchape kazi kwa maslahi ya nchi yetu na serikali inayoongozwa na CCM."

CCM ndio iliyopewa ridhaa ya kuongoza nchi, hivyo viongozi wake hawana budi kuhimiza amani kama wanavyofanya katibu mkuu na mwenyekiti wa taifa kwa nyakati tofauti.

**UMUHIMU WA AMANI**

Kwanza kabisa jamii imejengwa na wafuasi wa itikadi, imani na mitazamo tofauti katika nyanja za siasa, dini na fikra, kwa hiyo kutofautiana kupo.

Lakini bado tutabaki kuwa ni watu wa jamii moja kwani kuna mambo yanayotuunganisha, ambayo hatupingani hasa amani na utulivu katika jamii, ambavyo vikiwapo watu wanaweza kufanya shughuli za maendeleo vizuri.

Amani na utulivu vikiwapo, wanasiasa, wanafanyakazi, wafanyiabiashara na watu wa kada nyingine wanaendelea na shughuli zao kama kawaida tena kwa uhuru, lakini bila hilo hakuna chochote cha maendeleo kitakachofanyika.

Wakati viongozi wakihimiza amani, kila mmoja wetu hana budi kulinda amani ya nchi ikiwamo kutetea ulinzi na uhifadhi wa haki za binadamu kwa kuunganisha nguvu na wadau katika kulinda haki hizo.

Kumekuwa kukidaiwa kuwapo kwa viashiria vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani, na sasa moja ya mambo ya msingi ambayo rais amekuwa akihimiza katika mikutano yake ni amani.

Miongoni mwa mambo yanayotajwa kama kikwazo kwa amani ni kutoheshimiwa kwa utawala wa sheria, katiba na kubadili sheria kwa maslahi binafsi.

Viashiria vingine vinavyotajwa ni kulegalega katika usimamizi wa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi na kukosekana kwa uadilifu kwa viongozi wa umma, wanaodaiwa kupindisha sheria kwa makusudi.



Rais Felix Tshesekedi wa DRC, na mpinzani wake Martine Fayulu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Fayulu akataa kujiunga serikalini, aanza kampeni aina ya Lumumba

**Na Ani Jozeni**

MGOMBEA wa pamoja wa awali wa iliyokuwa kambi ya upinzani nchini Congo, Martin Fayulu, amekataa kuwa sehemu ya serikali ya umoja wa kitaifa itakayoongozwa na Rais Felix Tshisekedi ambaye ushindi wake ulitiliwa shaka na vyombo vya ndani na nje ya DRC.

Fayulu ametoa hotuba ya kwanza mwishoni mwa wiki tangu Rais Tshesekedi alipoapishwa katikati ya wiki, ambako alitoa rai kuwa 'ndugu yetu Martin Fayulu' ajiunge na utawala mpya kujenga nchi.

Lakini kiongozi huyo wa upinzani amekataa, akisema kuwa ndiye rais halali.

Ila tofauti na jinsi ilivyokuwa Kenya mwaka jana au hivi karibuni huko Venezuela, hajatoa rai ya 'kula kiapo' kivyake, ashindane.

Katika matamshi yake Fayulu alitaka kuwe na upinzani wa amani hasa kwa maandamano kutetea ushindi wake lakini haielekei kuwa wafuasi wake ni kundi la kisiasa lenye mwelekeo mmoja, au linalotaka kwa nguvu zote kuwa mgombea huyo wa pamoja hapo awali ni budi aingizwe madarakani.

Hata Kanisa Katoliki ambalo tangu mwanzo limekuwa mstari wa mbele kutoa ushuhuda kuwa uangalizi wao wa uchaguzi kupitia waangalizi takriban 40,000 waliosambazwa nchini kote ulionyesha kuwa Fayulu alishinda tena kwa kura nyingi pia halijaonyesha shauku ya kufuatilia kwa nguvu kuwekwa wazi mtiririko wa kupiga kura, kuhesabu na kutangaza.

Ni kama kuna aina fulani ya kuridhika kuwa upinzani umeshinda na kutangazwa, bila kujali ni mpinzani yupi hasa aliyeshinda.

Aliwaambia mamia ya wafuasi wake jijini Kinshasa kuwa 'ukipewa mkono halafu ukaona mkono huo ni mchafu, unaukataa' na ndiyo maana ataendelea kudai haki itendeke kuhusiana na uchaguzi huo na siyo kumtii "mtu huyo ambaye hatujamchagua."

Mpango wake wa sasa ni kufanya ziara kuzunguka pande tofauti za nchi hiyo kueleza jinsi uchaguzi huo ulivyokwenda na matokeo yalivyopokonywa, pia kupeleka madai yake mbele ya Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Mataifa (UN).

> Walisimamiwa na shirika la ujasusi la Marekani CIA na kuwa chini ya Kanali Joseph Mobutu kwa idhini ya waziri mkuu wa Katanga, Moise Tshombe, akauawa kikatili.

Ni hatua ya ziada baada ya juhudi zake kupeleka madai ya kutolewa matokeo potofu kukataliwa na Mahakama ya Katiba ya nchi hiyo, ambayo pia iliteuliwa na rais aliyepita, Joseph Kabila.

Tatizo ambalo Fayulu anaelekea kukabiliana nalo kila atakapokwenda ni kuwa anachotaka kueleza si habari, kuwa hakuna jipya kwani hali hiyo inafahamika kila mahali, lakini nchi mbalimbali duniani pamoja na wengi kati ya raia wa DRC wamekubali kuiunga mkono mamlaka hiyo mpya ili amani irejee.

Suala la msingi ni kuwa ni upinzani ndiyo umeshinda na siyo utawala wa Rais Kabila kujiendeleza kupitia mgombea wa chama chake, Emmanuel Shadary.

Haitakuwa rahisi kwa makundi ya kisiasa nchini humo kuondoka kwenye msimamo wa 'mwanzo mpya' kwenda katika ule wa 'mshindi halisi' ambao anautaka Fayulu, kwani inatosha kuwa ni upinzani.

Pamoja na kuwa kuna ushahidi usiopingika kuwa Fayulu aliungwa mkono na watu wengi zaidi kama mgombea kwa nafasi ya urais, hakuna vielelezo vya kutosha kuwa anao msingi imara wa kufuatilia madai yake kwa mfano kupitia wingi wa wabunge.

Taarifa zilizotolewa baada ya uchaguzi zinasema kuwa wafuasi wa rais aliyepita ndiyo wenye wingi wa viti bungeni, hali inayompa nguvu Shadary na kumkandamiza Fayulu katika kusukuma maswali, hoja au maazimio ya Bunge kuhusu kilichofanywa na taasisi tofauti kuhusiana na uchaguzi mkuu.

Kwa maana hiyo Fayulu atakuwa anategemea kuungwa mkono na wapiga kura wake, na hawataanza mapema kufanya hivyo.

Mwelekeo wa Fayulu wa kuzunguka Congo nzima kueleza kilichotokea ni marudio kiaina ya historia, ambako Congo Leopoldville ilifikia uhuru wake mwaka 1960 katika hali ya ushindani kati ya vyama na viongozi wa kikabila wanaoungwa mkono na Ubelgjiji na Ufaransa.

Upande wa pili ulikuwa wa viongozi halisi wa kutafuta uhuru wa nchi hiyo wakipingwa na utawala wa kikoloni, hivyo wahafidhina wakapewa madaraka nusu, chini ya Rais Joseph Kasavubu, na wazalendo wakapewa nafasi ya uwaziri mkuu, aliyekuwa Patrice Lumumba. Muda si mrefu Kasavubu akamfukuza kazi Lumumba, ambaye alianza kuzunguka nchini kote kueleza kilichotokea, na alipofika Katanga akakamatwa na askari wa kukodiwa.

Walisimamiwa na shirika la ujasusi la Marekani CIA na kuwa chini ya Kanali Joseph Mobutu kwa idhini ya waziri mkuu wa Katanga, Moise Tshombe, akauawa kikatili.

Ila kwa vile dunia ni mviringo, ni Felix Tshisekedi ambaye amefaidi historia hiyo hadi kumfikisha madarakani, hasa kwa kivuli cha baba yake, hayati Etienne Tshisekedi wa Mulumba, aliyefikia pia uwaziri mkuu chini ya Kasavubu na baadaye, Mobutu.

Ni heshima hiyo ya kuwa mwana wa mpinzani wa jadi iliyomwezesha Felix Tshisekedi awe ndiye mtu ambaye Rais Kabila angeweza kuongea naye kupanga 'dili' la nini kifanyike, kwani asingeweza kushinda kiti hicho kivyake, na angechangamkia wazo la 'kufanya biashara' kuhusu suala hilo.

Na kama Lumumba alivyoshindwa kukusanya nguvu akihutubia watu majimboni, ndivyo Fayulu atakavyoona ugumu wa kuwaambia watu waendelee na maandamano, wasitulizane na kuanza upya, ambayo ndiyo njia sasa.

Ila kuna tofauti kubwa kati ya Congo ya 1960 na hii ya 2019 pamoja na kufanana katika maeneo kadhaa, na siyo madogo. kwa mfano tishio la kujitenga ambalo lilikuwa Katanga wakati ule sasa linaonekana bayana upande wa Mashariki wa nchi hiyo.

Kama ilivyokuwa miaka ya 1960, bado kuna vikosi vya Umoja wa Mataifa vya kulinda amani, kwani haijawahi kuwepo kikamilifu licha ya utulivu uliokuwepo wakati wa utawala wa kidikteta kiasi wa Mobutu, na alipopinduliwa na kina Kabila wakitokea Rwanda na majeshi yasiyo ya kukodiwa lakini ya kivamizi, vita ikafumuka upya nchini humo.

Ndiyo maana hoja za Fayulu ni nzito lakini tishio lake sio kubwa kivile kwani yeye si kiongozi wa kijeshi kama Kabila aliyeondoka madarakani.

Ni mwanasiasa ajuaye uvumilivu, si kupiga tu.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# EAC na changamoto ya mgogoro wa wanachama Rwanda, Burundi

kutanua wigo wa ushirikiano kati ya nchi wanachama, pamoja na mambo mengine, masuala ya siasa, uchumi na kijamii kwa maslahi ya pande zote.

Kwa hiyo nchi mbili kama Rwanda na Burundi zinapoweka wazi kuhusu mgogoro wao, ni wazi kwamba azma ya 'kutembea njia moja' itakwama na hivyo kuwa vigumu kulifikia kusudio la kuwa na jumuiya yenye nguvu.

Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza, amekuwa akimshutumu Rais Paul Kagame wa Rwanda na utawala wake kwa kuihujumu Burundi, kwamba hali hiyo inachochea kukosekana kwa amani na utulivu nchini humo.

Hata hivyo, serikali ya Rwanda imekuwa ikakanusha madai hayo mara kwa mara.

Uhasama kati ya utawala wa Rais Kagame wenye Makao Makuu yake jijini Kigali na ule wa Rais Nkurunziza wenye Makao Makuu aliyoyahamisha kutoka Bujumbura kwenda Gitega, ulikolea zaidi mwaka 2015.

Wakati huo, Rais Nkurunziza alikuwa katika mchakato wa kuingia katika awamu ya tatu ya utawala, hivyo kuzua utata kiasi cha kusababisha maandamano nchini mwake, na baadaye kunusurika katika mapinduzi ya kijeshi yaliyozimwa.

Mapinduzi hayo yalifanyika Mei, 2015 wakati Rais Nkurunziza akiwa jijini Dar es Salaam, kushiriki kikao cha usuluhishi wa mzozo wa kisiasa uliohusu kutaka kuongeza muda wa kuiongoza Burundi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Usalama wa Burundi 'aliyetumbuliwa' na Rais Nkurunziza Februari, 2015, Meja Jenerali Godefroid Niyombare, alitangaza mapinduzi hayo kupitia kituo binafsi cha redio cha Bonesha FM.

Ikulu ya Rais Nkurunziza ilijibu baadaye kwamba mapinduzi hayakufanikiwa na mhusika alikuwa akisakwa kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Pia, kumewahi kutokea mapigano ya kutumia silaha za moto kufuatia mauaji ya raia na wapiganaji kwenye maeneo ya mpakani mwa nchi hizo.

Shutuma zote kuhusu matukio hayo na mengine yenye taswira ya kuvunja amani ya Burundi, yakadaiwa kupata usaidizi wa karibu kutokea Rwanda.

Kwa hali hiyo, Rais Nkurunziza akatangaza kwamba Rwanda imekosa sifa za kuendelea kuwa mshirika wa Burundi.

Ndipo serikali ya Burundi ilipotoa rai kwa EAC, kuitisha kikao cha dharura kwa lengo la kupata suluhu ya mzozo huo ambao hata hivyo, Rwanda imekuwa ikikanusha madai hayo mara kwa mara.

Ulipoitishwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za EAC Februari Mosi mwaka huu jijini Arusha, ilitarajiwa kwamba wakuu wa nchi mbili hizo wasingefika.

Mikutano kama huo ilipangwa kufanyika Novemba 30 na baadaye Desemba 27, mwaka jana lakini ilishindikana kufanyika.

Kabla ya mkutano wa Arusha, Waziri wa Masuala ya EAC wa Burundi, Isabelle Ndahayo, aliliambia gazeti la The East African jijini Bujumbura, kuwa nchi hiyo itashiriki mkutano wa Arusha na kwamba watajadili mzozo huo ikiwa tu utawekwa kwenye ratiba.

Rais Kagame alishiriki mkutano wa Arusha na kukabidhiwa Uenyekiti wa EAC kutoka kwa Rais Yoweri Museveni wa Uganda na Burundi ikawakilishwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Gaston Sindimwo.

Sindimwo amekuwa akimwakilisha Rais Nkurunziza tangu kutokea kwa mapinduzi yaliyoshindikana, isipokuwa Julai, 2017 alipokutana na Rais Joseph Magufuli wilayani Ngara mkoa wa Kagera.

Kwa hali ilivyokuwa, haikutarajiwa sana kwa Rais Nkurunziza kuhudhuria mkutano wa Arusha ambao pia ulilenga kuangazia uondoaji vikwazo visivyokuwa vya kodi kwa biashara katika ukanda wa EAC na azma ya kuingia jumuiya hiyo katika shirikisho la kisiasa.

> "Sasa hapa sijajua EAC watasimama wapi ama labda wana ujuzi wa ziada, lakini ninavyojua mimi wao ndio wasuluhishi ambao Burundi imewakimbilia, kisha Mwenyekiti akawa ni kiongozi wa nchi inayolalamikiwa...tuwape nafasi kwa maana lazima mgogoro huo utatuliwe,"




Wakuu wa nchi za EAC, Kutoka kushoto, Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, Paul Kagame wa Rwanda, Yoweri Museveni wa Uganda na John Magufuli wa Tanzania. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Liberat Mfumukeko

Naye Rais Kagame ilitarajiwa asingefika jijini Arusha kuhudhuria mkutano huo, kwa sababu ya kuwa na siku ya kumbukumbu ya mashujaa nchini kwake, lakini alishiriki.

Hoja nyingine katika mkutano huo ilihusu namna ya kuharakisha mchakato wa kuiwezesha Sudan Kusini kushiriki shughuli za EAC na kuyapitia maombi ya Somalia kuwa mwanachama wa jumuiya hiyo.

## KUTEULIWA KWA KAGAME KUIONGOZA EAC

Wakati mgogoro kati ya Rwanda na Burundi ukizidi 'kutokota', Rais Kagame ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa EAC, akichukua nafasi hiyo kutoka kwa mtangulizi wake, Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda.

Vyanzo vya uhakika kutoka katika sekretarieti ya EAC vimekaririwa na gazeti la East African kuwa uteuzi wa Rais Kagame ulipitishwa 'kwa mbinde' kutokana na pingamizi lililowekwa na Burundi.

Inaelezwa kwamba Burundi ilihofia kwamba kuwapo kwa Rais Kagame katika wadhifa wakati huu ambapo nchi hizo zipo kwenye mgogoro wa kidiplomasia, hakutakuwa na tija.

Lakini katika kile kinachoonekana kukwepa mgogoro huo kuwa 'ajenda kubwa' kuhusu kuchukua kwake nafasi hiyo, Rais Kagame akasema EAC ni taasisi ya wananchi wa mataifa yaliyo wanachama na kwamba mafanikio yake yatapimwa kwa idadi ya watu wanaonufaika kutokana na program zake.

Mchambuzi wa masuala ya migogoro ya kijamii, Silvanus Isdory anasema ni vigumu kupata suluhu ya mzozo unaohusisha mmoja wa upande kuwa na nguvu za kiutawala na uongozi.

"Katika utatuzi wa mgogoro wowote, ili upate suluhu nzuri ya kudumu, pande zinazopingana zisiwe katika mamlaka ya utawala ama uongozi, na ndio maana hata kiongozi anaposhutumiwa, ni vema akajiuzulu kupisha uchunguzi, ndivyo ilivyo katika migogoro pia," anasema.

Anasema ingawa EAC inaweza kuwa na mifumo ya kitaasisi inayoweza kukabiliana na kuwapo katika uongozi kwa Rais Kagame na kushughulikia mzozo ambao serikali yake inashutumiwa, lakini mazingira ya kupata suluhu ya kudumu hayatakuwa na wigo mpana kufikia lengo.

Naye mtaalamu wa migogoro katika mawasiliano, Flora Protas anasema ili kupata suluhu ya kudumu, ni lazima msuluhishi akubaliwe na pande mbili, inayolalamika na ile inayolalamikiwa.

"Sasa hapa sijajua EAC watasimama wapi ama labda wana ujuzi wa ziada, lakini ninavyojua mimi wao ndio wasuluhishi ambao Burundi imewakimbilia, kisha Mwenyekiti akawa ni kiongozi wa nchi inayolalamikiwa...tuwape nafasi kwa maana lazima mgogoro huo utatuliwe," amesema.

Vyanzo vingine vimekaririwa na vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano vikieleza kuwa kutokana na mzozo unaoendelea kati ya Burundi na Rwanda, kuna uwezekano kuvunjika kwa EAC kama ilivyotokea mwaka 1977.

## KATIBU MKUU

Lakini Katibu Mkuu wa EAC, Libérat Mfumukeko, anasema kuvunjika kwa jumuiya hakuwezi kutokea tena na kufafanua kuwa awali (1977) ilikuwa 'nyakati za giza' tofauti na sasa ambapo jumuiya imepiga hatua kubwa katika kujiimarisha kwake.

Jambo la maana katika EAC ni kutambua kwamba jumuiya hiyo ipo kwa ajili ya raia wake, kama alivyoelezea Rais Kagame baada ya kukabidhiwa uenyekiti na Rais Museveni.

Hivyo ipo haja ya kushirikisha stadi na mbinu zisizoathiri utendaji, misingi na mipango ya EAC, ili mgogoro huo upate suluhu ya kudumu na ukanda wa Afrika Mashariki uwe salama kwa maslahi ya wananchi wake.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540**



Rais Donald Trump akiwa katika moja ya Makumbusho ya Kitaifa ya Historia ya Waafrika Weusi na Utamaduni wao, katika uwanja maarufu wa National Mall. Picha ndogo ni Gavana Ralph Northam. **PICHA: MTANDAO**

# UBAGUZI MAREKANI:

## Shinikizo la Gavana kujiuzulu laongezeka

GAVANA wa Jimbo la Virginia anashinikizwa kujiuzulu, baada ya kudhihirika kuwa aliweka picha ya ubaguzi wa rangi aliyohifadhi katika kitabu chake cha picha za kumbukumbu cha chuo cha udaktari zaidi ya miaka 30 iliyopita.

Ralph Northam ameomba msamaha Ijumaa kwa "ubaguzi na matusi", hayo katika mavazi yaliyowekwa ndani ya kitabu hicho. Katika tamko alilolitoa kupitia picha ya video, Northam amesema picha hiyo haiendani na yeye alivyo hivi leo.

"Siwezi kubadilisha maamuzi niliyofanya, wala kurekebisha madhara yaliyoletwa na tabia yangu ya wakati huo na hivi leo," ameeleza zaidi.

"Lakini nakubali kuwajibika kwa vitendo vyangu vilivyopita, na niko tayari kufanya bidii kurejesha imani yenu kwangu."

Kurasa ya kitabu hicho ipo picha ya mtu mwenye uso mweusi na mwingine amevaa mavazi ya kikundi cha ubaguzi wa rangi kilichokuwa na mavazi ya kutisha na kuficha utambulisho wao maarufu kama Ku Klux Klan garb.

Gavana ameeleza kuwa yeye ni mmoja wao katika hiyo picha lakini hajajitambulisha ni yupi kati yao.

Kikundi cha Wabunge Wamarekani Weusi na cha Baraza la Wawakilishi Weusi la Virginia vimemtaka mara moja ajiuzulu.

"Ralph Northam alikuwa na karne tatu za kujitambua zaidi, lakini ni hivi sasa anakiri kitendo hiki cha ubaguzi wa rangi,". Kikundi cha Wabunge Weusi walituma ujumbe wa Twitter. "Kuomba msamaha hivi sasa haitoshi. Ni lazima ajiuzulu."

Kikundi cha Baraza la Wawakilishi Wamarekani Weusi Virginia limeposti tamko kupitia ujumbe wa Twitter ambao unasema kwa Northam: " Tunashukuru sana yote ambayo amechangia katika maslahi yetu ya pamoja. Lakini kufuatia kile kilichodhihirika leo, ni wazi kuwa hawezi tena kututumikia kwa ufanisi kama Gavana. Ni wakati wa yeye kujiuzulu, ili Virginia ianze mchakato wa kuponya maradhi haya."

### ALICHOWAHI KUTAMKA TRUMP KUHUSU UBAGUZI:

Rais Donald Trump amewahi kulaani sera za ubaguzi wa rangi zilizopelekea tukio la kinyama katika maandamano ya watu wenye itikadi hizo waliokusanyika huko Charlottesville, Virginia, mwaka juzi akisema kuwa "ubaguzi ni dhambi."

Kwa mara ya kwanza tangu machafuko hayo yatokee, Trump ametaja kwa jina sera za kinazi, Kikundi cha Ku Klux Klan, na ubaguzi wa rangi ni "wahalifu na wezi... ambayo ni kinyume cha kila maadili tunayoyafuata nchini Marekani."

Aliahidi kuwa mtu yoyote aliyefanya "vitendo vya ubaguzi wa uvunjifu wa amani" katika eneo la Charlottesville atawajibishwa. "Haki itatendeka," alisisitiza.

Trump alisema kile kilichotokea Charlottesville ni "uovu wa hali ya juu uliosababishwa na chuki, ubaguzi na uvunjifu wa amani."

"Alisema hilo halina nafasi nchini Marekani na kama nilivyosema mara nyingi hapo awali, bila ya kuangalia rangi za ngozi zetu, sote tunaishi chini ya utawala wa sheria," amesema.

Matamko ya Trump yalifuatiwa na lawama kutoka makundi mbalimbali ya kisiasa kwa kushindwa siku mbili kutumia maneno ya ubaguzi na sera za kinazi kulaani vitendo hivyo vya uvunjifu wa amani.

Wamarekani weusi wasio na hatia waombwa radhi baada ya miaka 70:

Wamarekani weusi wanne waliokuwa hawana hatia ambao walituhumiwa kwa kosa la kumbaka msichana wa kizungu mwenye umri wa miaka 17 kusini mwa jimbo la Florida, Marekani miaka 70 iliyopita familia zao ziliombwa radhi kwa niaba yao Ijumaa.

Charles Greenlee, Walter Irvin, Samuel Shepherd na Ernest Thomas walikuja kujulikana kwa jina la Groveland Four. Wote wanne ni marehemu. Lakini ndugu wa familia hizo bado wako hai.

Familia hizo zilihudhuria usikilizwaji wa shauri hilo ili kuwasafisha watu hao kutokana na tuhuma hizo, huko Tallahassee Ijumaa ambapo maafisa walipiga kura ya pamoja kuwaomba radhi watu hao wanne.

Inaendelea Uk. 18

# Venezuela; Rais Maduro ajipanga kwa uchaguzi mpya wa Bunge

**Na Michael Eneza**

HALI ya kisiasa ya Venezuela inaelekea kupata aina fulani ya ufumbuzi baada ya nchi za Magharibi kuunga mkono jaribio la kumwondoa kwa nguvu Rais Nicolas Maduro madarakani, kumbadilisha kwa Spika wa Bunge Juan Guaido, aliyejitangaza kuwa rais wa muda.

Kiongozi huo wa Bunge kijana aliapishwa na kundi la wafuasi wake wakati maandamano na ghasia yakiendelea jijini Caracas, kutokana na mvutano kati ya Bunge na utawala wa Rais Maduro, ambaye bado ameendelea kuungwa mkono na jeshi la nchi hiyo.

Tatizo la msingi ni hali mbaya ya uchumi wa nchi hiyo ambako bajeti ya serikali hutegemea mauzo ya mafuta nje, ambako bei inashuka.

Wachunguzi wa habari wanasema ili Venezuela itulizane chini ya utawala wa kimapinduzi ulioko madarakani, inabidi bei ya mafuta ipande na kufikia dola 100 kwa pipa, wakati imekuwa ikishuka hadi dola 45 na kupanda tena hadi dola 60 wiki iliyopita.

Ila kinachopiganiwa mitaani na bungeni ni uhalali wa serikali iliyoko madarakani kwani iliingia au kurudi tena madarakani wakati wa kipindi cha hayati Hugo Chavez aliyerithiwa na Maduro, kwa kutumia kura ya maoni yenye mvutano mkubwa na maswali mengi.

Sehemu kubwa ya wafuasi wa awali wa chama cha kimapinduzi cha ki--Bolivar kama Spika huyo wamekihasi chama kujiunga na madai, maandamano.

Ni mvutano huo wa kikatiba unaoendelea tangu 2016 ambao ulimpa nguvu Guaido na wafuasi wake kutangaza kutokumtambua Maduro kama rais, huku wakiungwa mkono na nchi kadhaa za Magharibi, hasa Canada na Marekani.

Baadaye Bunge la Umoja wa Ulaya (EU) lilipitisha azimio kuitambua serikali ya muda ya Guaido, hivyo kumweka Maduro mtegoni endapo ataanza kutumia jeshi kuwaondoa waandamanaji kwa risasi, kwani hapo sasa angeweza kushtakiwa kwa kukiuka haki za binadamu.

Hata hivyo, machafuko yakizidi au jeshi kutumika Maduro hawezi kufikishwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai huko The Hague kwa veto za Russia na China.

Kabla ya kutangazwa kuwa utawala wa Maduro unafikiria kuandaa uchaguzi mwingine wa Bunge, wachunguzi walikuwa wanahofia uwezekano wa uingiliaji kijeshi kutoka nje, hasa Brazil na Colombia dhidi ya utawala wa Maduro.

Ni kwa maelezo kuwa unasababisha wimbi kubwa la wakimbizi na kuhatarisha mshikamano kijamii kwani nchi zinazozunguka Venezuela hazijajiandaa kupokea wakimbizi lukuki kutoka nchini humo, halafu pia serikali hiyo



Rais wa Venezuela Nicolas Maduro. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Kiongozi wa upinzani aliyejitangaza kuwa rais wa mpitio wa Venezuela Juan Guaido.

> “ Ila ilikuwa tahadhari ya wazi kuwa utawala wa Rais Maduro hauwezi kutegemea jeshi kuendelea kuunga mkono serikali hiyo machafuko yakiendelea, na likazidi kuondoa mezani ndoto za kutumia jeshi kuzuia mabadiliko.

imekosa uhalali kwani ipo serikali ya muda inayoungwa mkono na maelfu ya waandamanaji.

Kwa njia hiyo upinzani umemzidi kete Rais Maduro katika propaganda, kuwa amewekwa na jeshi, si watu au Bunge.

Kubadili msimamo kwa Rais Maduro kutoka kuwa ‘ngangari kinoma’ na kukubali kufanyika uchaguzi wa Bunge mapema zaidi ya ilivyopangwa kikatiba kulifuata baada ya ofisa wa ngazi za juu wa jeshi la anga, cheo cha meja jenerali, kuuasi utawala wa Maduro na kujiunga upinzani.

Kujitoa kwa ofisa huyo kuliashiria kuwa hata katika jeshi la nchi hiyo hakuna uhakika wa kuendelea kuungwa mkono kwa utawala wa Maduro endapo hali ya uchumi itaendelea kuzorota, na haiwezi kupumua bila bei ya mafuta kupanda, tena kwa kiwango cha kutosha.

Ni jambo ambalo haliwezekani kwani Rais Donald Trump wa Marekani anafanya kila awezalo kuzuia isipande.

Guiado alianza kuonyesha kuwa anaweza kuteka kikamilifu mamlaka ya nchi alipotangaza kuwa misaada ya kibinadamu itaanza kuingia kutoka nje kupitia mji wa Cucuta, ulio mpakani na Colombia, moja ya nchi zenye serikali za mrengo wa kulia zinazounga mkono jitihada za kumuondoa Rais Maduro.

Bado utawala wa Maduro ulikuwa haujasema lolote kuhusu uwezekano wa misaada hiyo, wakati juhudi zake za kujiweka karibu zaidi na utawala wa Rais Vladimir Putin wa Russia zilikuwa zinaelekea kukwama.

Juhudi hizo zingekuwa na umuhimu endapo ingekuwa ni suala la kutishiwa na Marekani kama Maduro na wenzake wanavyodai, bila maandamano.

Kugeuzwa kwa haraka kwa mgogoro huo kuwa wa kimataifa umempa nguvu kiongozi wa upinzani, kwani jeshi sasa linamuunga mkono Rais Maduro kama kundi la kijamii, lakini likitumia mtutu wa bunduki inaweza kuwa janga kwa utawala huo.

Licha ya kuwa hakuna nchi zenye uchu wa kuingilia kati nchini humo, uharaka wa kumtambua rais wa muda Guaido ulionyesha kuwa wana dhamira ya kujitosa zaidi katika suala hilo hali ikileta hitaji hilo, na kwa vile Venezuela siyo nchi ya kahawa ila mafuta, uwezekano wa kuangaliwa kwa ‘jicho la tatu’ ni mkubwa zaidi.

Ni kama ilivyokuwa Libya au Iraq, kuwa nchi tajiri kwa mafuta ikiparaganyika inavuta uingiliaji.

Taarifa aliyoitoa Jenerali Francisco Yanez alipojitoa katika mshikamano na serikali ya Rais Maduro na kutangaza utii wake kwa Guaido ulimpa nguvu zisizo za kawaida kiongozi huyo wa upinzani, kwa njia ya kupewa heshima halisi na ofisa mwandamizi wa jeshi kuwa ndiye mkuu halali wa nchi hiyo.

Jenerali Yanez alisema urejeshwaji wa demokrasia umakaribia, akaongeza kuwa hatatoa taarifa nyingine zozote “hadi atakaporuhusiwa na amiri jeshi mkuu wa jeshi halali la Venezuela, Rais Juan Guaido.”

Ni taarifa ambayo kwa hali yoyote ilikuwa ni changamoto kwa Maduro kuweza kusimama mbele ya kadamnasi, au hata vyombo vya habari, kuipuuzia kuwa haina maana yoyote. Ilikuwa ni kama deraya imetobolewa na mishale ya adui inaweza kupita kirahisi tu.

Alithubutu hata kutangaza katika hotuba iliyoingizwa kuwa mkanda wa video kuwa ‘asilimia 90 ya jeshi la Venezuela ‘ wanamuunga mkono Guaido, dai ambalo wengi kati ya wachambuzi habari walilitilia mashaka kwani ingekuwa rahisi kwa upande huo kujitokeza maofisa zaidi wa jeshi kuunga mkono uasi huo.

Ila ilikuwa tahadhari ya wazi kuwa utawala wa Rais Maduro hauwezi kutegemea jeshi kuendelea kuunga mkono serikali hiyo machafuko yakiendelea, na likazidi kuondoa mezani ndoto za kutumia jeshi kuzuia mabadiliko.

Ni katika hali hiyo mazungumzo ya kupata msaada wa Russia yakaanza kufifia na matayarisho ya uchaguzi wa Bunge kuanza kikamilifu, wafuasi wa Maduro walipogundua kuwa kwa hali yoyote ile, wamekalia kuti kavu, kuzingirwa.

# Shinikizo la Gavana kujiuzulu laongezeka

**Inatoka Uk.17**

“Kitendo hiki sahihi cha kuwaomba radhi hakijachelewa kabisa,” Gavana Ron DeSantis amesema katika tamko lake. “Naamini kuwa utawala wa sheria ndio jambo tukufu linalounganisha jamii. Wakati sheria inapokanyagwa, sote tunaathirika. Kwa hawa vijana wanne maarufu kama Groveland Four, ukweli ulikuwa umefichwa.”

Thomas aliuliwa na kundi lenye mhemuko muda mfupi baada ya tukio hilo 1949.

Wengine watatu waliteswa na hatimaye kukiri makosa na kuhukumiwa na washauri wa mahakama ambao wote walikuwa ni wazungu.

Shepherd alipigwa risasi na kuuliwa na mkuu wa polisi wa eneo ambaye alikuwa anampeleka kuhudhuria kesi iliyokuwa inarudiwa tena. Greenlee na Irvin walihukumiwa kifungo cha maisha.

Norma Padgett ambaye ilikuwa inadaiwa amebakwa, bado yuko hai. Yeye pia alihudhuria siku ya Ijumaa kikao hicho.

“Mimi siyo muongo,” amesema kukiambia kikao hicho.

Wachunguzi wa kujitegemea wamethibitisha kuwa watu hao ambao walihukumiwa bila ya ushahidi, wakati wa zama za uovu wa nadharia iliyojulikana kama Jim Crow nchini Marekani, walikuwa hawana hatia kutokana na tuhuma hizo. Zama hizo zilikuwa ni zenye sera za ubaguzi na ukandamizaji na pia kuendeleza utumwa.

Devil In The Grove, ni kitabu kilichoandikwa juu ya kesi ya Groveland Four, na kushinda tuzo ya Pulitzer Prize mwaka 2013.

**CHANZO: Sauti ya Amerika-VoA**



Kiongozi wa muda mrefu wa upinzani DRC, marehemu Etienne Tshisekedi ambaye ni baba mzazi wa Rais wa sasa wa DRC, Felix Tshisekedi. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Tshisekedi kufanikisha mazishi ya Tshisekedi DRC

**Na Mwandishi Wetu**

Ni takribani miaka miwili sasa tangu aliyekuwa kiongozi mkuu wa upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Étienne Tshisekedi wa Mulumba' kufariki dunia nchini Ubelgiji, lakini mwili wake bado haujazikwa.

Etienne Tshisekedi aliyezaliwa Desemba 14, 1932, ndiye baba mzazi wa Rais wa sasa wa DRC, Felix Tshisekedi. Wakati wa uhai wake, aliwahi kuwa Waziri Mkuu mwaka 1997.

Mwili wa Tshisekedi hivi sasa unaendelea kutunzwa jijini Brussels, Ubelgiji na si kwenye ardhi ya DRC, taifa 'alilolipigania' katika kipindi kirefu cha maisha yake.

Miongoni mwa vyanzo vikuu vilivyosababisha mwili huo kutozikwa kwa muda wote, ni mzozo wa kuhusu mahali panapofaa kuuzika.

Familia ya Tshisekedi na chama cha UDPS walitaka kiongozi wao azikwe kwenye eneo la makumbusho katika Makao Makuu ya chama hicho jijini Kinshasa, lakini mamlaka ya DRC (kwa wakati huo) ilikataa, ikitumia sheria ya mkoloni iliyozuia mazishi kufanyika kwenye maeneo yenye makazi ya watu.

Uongozi wa jijini Kinshasa, ukaelekeza kwamba mazishi ya Tshisekedi yanapaswa kufanyika kwenye maeneo ya makaburi kama inavyofanyika kwa raia wengine wa jijini humo na kwamba (mamlaka hiyo) ndiyo ingesimamia mazishi hayo.

Kama Tshisekedi angezikwa jijini humo, ilitarajiwa kwamba Moise Katumbi aliyekuwa mpinzani mkuu wa Rais aliyemaliza muda wake, Joseph Kabila, angeshiriki mazishi kutokea uhamishoni alipokuwa anaishi.

Kwa vijana, Katumbi anapoonekana jijini Kinshasa huibua shamrashamra na shangwe ambazo zingeweza 'kutibua' maombolezo ya msiba wa Etienne Tshisekedi.

**UMAHIRI WAKE**

Étienne Tshisekedi wa Mulumba alikuwa mwanasiasa mashuhuri wa upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), muasisi na kiongozi wa chama cha upinzani cha Union for Democracy and Social Progress (UDPS).

Alikuwa mkosoaji na mpinzani mkubwa wa kiraia kwa kiongozi anayedaiwa kuitawala nchi hiyo kwa misingi ya kidikteta, Mobutu Sese Seko.

Mobutu alitawala nchi hiyo ikijulikana kama Zaire kwa zaidi ya miongo mitatu kabla ya kung'olewa kwa msaada wa majeshi ya nje yakiwamo ya Rwanda na Uganda.

Pia alimpinga kiongozi wa utawala wa kijeshi Laurent Kabila aliyeingia madarakani kwa njia ya mapinduzi mwaka 1997, na mwanaye, Joseph Kabila `aliyerithi' kiti hicho mwaka 2001 baada ya baba yake (Laurent) kuuawa.

Hata afya yake ilipoanza kudhoofika, Etienne Tshisekedi aliendelea kuwa 'kinara wa upinzani' nchini DRC.

Aliyewahi kuwa Msemaji wa upinzani, Jean-Raymond Muyumba, alikaririwa akisema "wamekataa tusiuzike mwili wa marehemu". Muyumba aliamini kwamba hata baada ya kifo chake, Etienne Tshisekedi aliendelea kuwa tishio kwa utawala wa Rais Kabila.

"Ndio anaiongoza nchi (Kabila), ana nguvu kubwa za dola lakini nguvu zenye mamlaka ya juu katika nchi zipo mtaani (kwa raia)," akasema.

Kabla ya kifo chake, Tshisekedi aliongoza muungano wa vyama vya upinzani na 'kuapa' kuwa Uchaguzi Mkuu wa Rais na wabunge nchini humo ungefanyika mwaka 2017.

Maelfu ya raia wa DRC walikuwa wakiamini kwamba kufanyika uchaguzi huo, kungeibua matokeo ambayo yangempa Etienne ushindi wa kishindo, ikiwa ni baada ya kuisaka nafasi hiyo kwa takribani miongo minne.

**KUKIMBIA NCHI**

Etienne Tshisekedi alipitia mikiki-mikiki mingi ya kisiasa DRC, ikiwamo kukimbilia na kuishi nje ya nchi hiyo.

Mathalani, Julai mwaka 2016, Etienne Tshisekedi alirejea DRC na kupata mapokezi makubwa alipotoka kwenye matibabu na 'ukimbizi wa kisiasa'. Alikuwa nje kwa takribani miaka miwili.

**BAADA YA KIFO CHAKE**

Baada ya taarifa kuhusu kifo chake kuthibitishwa, maelfu ya wafuasi wake waliandamana barabarani, wakafika karibu na makazi yake yaliyopo wilaya ya Limete, huku wakiwatupia mawe askari waliokuwa wakiwazuia na askari `wakijibu mapigo' kwa mabomu ya machozi na wengine wakikamatwa.

Wakati wa utawala wa Mobutu, Etienne Tshisekedi aliwahi kuitumikia serikali yake akiwa Waziri kabla ya kuunda UDPS mwaka 1982.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2001, Etienne Tshisekedi alishika nafasi ya pili nyuma ya Rais Kabila (wakati huo), lakini uchaguzi huo ulidaiwa kughubikwa na udanganyifu mkubwa.

"Mbuyu umeanguka…watu kama hawa si rahisi kuwapo kwenye jamii zetu," alisema Albert Moleka, aliyewahi kuwa Ofisa Mkuu wa Tshisekedi katika uchaguzi wa mwaka 2011.

**DALILI NJEMA ZA MAZISHI**

Mwaka jana, kuliibuka taarifa za kuwapo makubaliano kati ya serikali iliyoongozwa na Joseph Kabila na familia ya Tshisekedi, kuhusu kufanyika mazishi yake.

Familia hiyo, chama cha UDPS na serikali, wakatangaza kamati ya watu tisa kushiriki mazungumzo na kukubaliana mipango ili ipatikane ndege binafsi itakayogharamiwa na serikali, iende Ubelgiji kuchukua mwili wa Tshisekedi.

Mwili wa Etienne Tshisekedi ulipangwa kuwekwa kwenye Jengo la Bunge kwa ajili ya maombolezo ya kitaifa kabla ya kuzikwa kwenye makazi ya familia nje ya jiji la Kinshasa.

Hata hivyo, haikutangazwa tarehe ya siku ya kuurejesha mwili huo. Awali, mwili ya Tshisekedi ulitarajiwa kurejeshwa DRC Machi, 17, 2017, baadaye ikasogezwa kuwa Mei halafu Agosti, lakini haikufanikiwa, kutokana na mzozo uliohusu mahali atakapozikwa.

Bila shaka baada ya kuchaguliwa kwa Felix Tshisekedi, mtoto wa marehemu Etienne Tshisekedi kuwa Rais wa DRC, ni dhahiri kwamba kigingi kilichosababisha mwili huo kuendelea kuwa nchini Ubelgiji kitaondoka na mwanasiasa huyo kupata heshima ya kuzikwa nchini kwake.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu +255 754 691540.**

MAKALA

# Mkataba wa kimataifa makombora masafa ya kati wasambaratika rasmi

Na Nimi Mweta



Rais Ronald Reagan wa Marekani (Kulia) na Katibu Mkuu na Kiongozi wa Urusi, Mikhail Gorbachev, walipotia saini mkataba wa kupunguza silaha za nyuklia za masafa ya kati, Desemba 8, mwaka 1987. Picha ndogo ni moja ya magari ya kurusha makombora ya masafa ya kati. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

MALALAMIKO ya Marekani kuwa Russia haitekelezi matakwa ya Mkataba wa Kimataifa wa Makombora ya Nyuklia ya Masafa ya Kati (INF-Intermediate Nuclear Forces Treaty) wa mwaka 1987, yameifanya nchi hiyo ifikie uamuzi wa kujitoa katika mkataba huo.

Hata hivyo, Russia ilikataa shutuma hizo na kuitaka Marekani iendelee kuheshimu mkataba huo jinsi ulivyo.

Matokeo yake, Russia nayo imetangaza kuwa hautambui mkataba huo mradi Marekani imetoa tangazo la dhamira ya kujitoa rasmi ndani ya miezi sita (kwa mujibu wa maangalizo katika mkataba huo, ili kutoa nafasi kwa jumuiya ya kimataifa kufanya juhudi zinazowezekana kutatua hali hiyo).

Hapakuwa na hata haja ya kungoja miezi sita kuthibitisha kuwa mkataba huo sasa umeparaganyika, Russia ilipokataa madai ya Marekani.

Isitoshe, wakati hali hiyo inajitokeza, hali ya kimataifa ni tofauti kwa kina na ile ambako mkataba huo ulitiwa saini mwaka 1987, wakati uthabiti wa hali ya usalama duniani ulikuwa unaweza kuhakikishwa na mkataba kati ya Marekani na iliyokuwa Urusi peke yao.

Sasa kuna taifa jingine kubwa lenye uwezo wa kubadili sura ya hali ya usalama katika maeneo tofauti duniani na hasa Mashariki ya Mbali ambako maslahi ya Marekani ni madogo, wakati tishio la Russia kwa Marekani zaidi linahusu Ulaya Magharibi, na baadhi ya nchi Ulaya Mashariki.

Ina maana kuwa China ingebidi pia iwe sehemu ya mkataba toshelevu wa kimataifa kuhusu makombora hayo.

Isitoshe kuna nchi kadhaa duniani ambazo zina makombora ya masafa ya kati hata kama bado hayana 'makucha' au 'ncha' za nyuklia lakini yanaweka hali ya usalama ya nchi za jirani katika mazingira magumu.

Mojawapo ni Iran, wakati India na Pakistan zina silaha za nyuklia, kwa hiyo kuwa na makombora kama hayo ni hali isiyoepukika, na yote hayo hayatawaliwi na mkataba huo wa kimataifa.

Bado hujaongeza nchi kama Korea Kaskazini iliyoanza kujitutumua na makombora ya masafa ya kati na baadaye marefu, kuweza kufikia ardhi ya Marekani, kabla ya Rais Donald Trump kuwaasa wanadiplomasia wake waache kuongea nao; jeshi lingetosha.

Wakati wa mtikisiko wa kimataifa kuhusu uwezekano wa Marekani kuishambulia Korea Kaskazini ili kuondoa uwezo wake wa kuifikia ardhi ya Marekani na silaha za nyuklia, hapakuwa na matumizi au majadiliano yoyote kuhusu kutumika kwa mkataba huo.

Pia, mkataba huu wa kutokuweka makombora ya masafa ya kati umbali unaoweza kuwa tishio kwa nchi yenye uhusiano wa karibu na Marekani, na pia kwa upande wa nchi yenye uhusiano wa karibu na Urusi wakati ule, inabidi uangaliwe ndani ya mkataba mpana zaidi wa NPT (Non-Proliferation Treaty) unaohusu kutokueneza uwezo wa kutengeneza silaha za nyuklia kwa nchi nyingine.

Huu ni mkataba wa jumla wa Umoja wa Mataifa (UN) ambao takriban kila nchi inatia saini, halafu watafute uwezo huo kisiri.

Ukiangalia idadi ya nchi ambazo tayari zimefikia uwezo wa kuwa na silaha za nyuklia, unakuta kuwa hakuna tena upenyo wa kuwa na mkataba kuhusu kuenea kwa silaha hizo, kwani 'hakuna siri ya watu wawili,' wakati tayari wapo watu wasiopungua 20 wenye siri ya utengenezaji wa silaha za nyuklia.

> Suala la kutumia mikataba au maazimio ya Umoja wa Mataifa halipo, kwani hakuna tena mlinzi wa maslahi ya pamoja kulinda amani ya dunia, ni mlingano wa vitisho.

Kwa mfano Pakistan ilipofanya jaribio lake la bomu la atomiki (au nyuklia, havitofautishwi kwa kina) ilisema eti ni 'bomu la Kiislamu,' kwamba kiitikadi inabidi nchi za Kiislamu nazo kuwa na uwezo wa silaha hizo, yaani kuweza kujilinda ipasavyo.

Ni wazi pia kuwa tofauti za awali (kati ya mwaka 1945 na 1960) zilizokuwa zinaigawa dunia sehemu kuu mbili zilianza kusambaratika baada ya Asia halafu Afrika kupata uhuru, zikaacha kuwa milki tu za mataifa makubwa tofauti.

Tofauti hizi kati ya Marekani na Russia kuhusu mkataba wa makombora wa masafa ya kati wa mwaka 1987 ni kielelezo cha kukwama kwa mustakabali wote wa udhibiti wa silaha za nyuklia kimataifa, kwani nchi siyo maskini au zenye utaalamu duni, zitegemee tu mataifa makubwa.

Enzi zilizopita, kusingekuwa na nchi kama Korea Kaskazini inafanya malumbano na mgongano wa moja kwa moja na Marekani bila kupitia China au Russia, jambo ambalo hivi sasa limewezekana. Kwa maana hiyo mikataba kuhusu silaha za nyuklia ingebidi zihusishe mataifa mengi, na ni jambo ambalo haliwezekani kwani hawana maeneo ya kuachiana katika udhibiti silaha.

Katika eneo la Mashariki ya Kati hivi sasa vita vinaendelea chini kwa chini kati ya Iran na Israel kupitia Syria na kwa kiasi fulani Lebanon, maeneo ambayo kimsingi yanadhibitiwa na Iran kama dola yenye nguvu eneo hilo, na yenye ushawishi mkubwa kwa jamii za madhehebu ya Shia katika ukanda huo.

Iran inataka kuweka vituo vya kijeshi vyenye uwezo wa kurusha makombora ya masafa ya kati kwa nia ya kuiteketeza Israel kuwa haina uhalali wa kuwepo kama nchi eneo hilo, hali ambayo kimsingi inaweza kusababisha vita vya nyuklia katika eneo hilo.

Na kwa vile Marekani ilishajitoa katika mkataba wa kimataifa wa kudhibiti uwezo wa Iran wa kutengeneza silaha za nyuklia, na sasa mkataba wa makombora ya masafa ya kati umesambaratika, hakuna tena wa kuizuia Iran,

Kinachoendelea huko Syria na kilichotokea Korea Kaskazini ni kielelezo cha hali halisi ya kimataifa kuhusu silaha za nyuklia, iwe ni kuenezwa kwake au ni makombora masafa ya kati kutishia uwepo au uthabiti wa usalama wa nchi jirani, endapo kuna nchi yenye silaha hizo inataka iifute katika ramani.

Kimsingi hali halisi ni kuwa inabidi kudhibiti nchi moja moja pale inapoonekana kutishia usalama wa nchi nyingine, yaani iwe ni Marekani yenyewe inayotishiwa kama kwa Korea Kaskazini, au ni Israel ambayo ni eneo muhimu kwa maslahi ya Marekani, kwani ni kama tu sehemu ya Marekani.

Suala la kutumia mikataba au maazimio ya Umoja wa Mataifa halipo, kwani hakuna tena mlinzi wa maslahi ya pamoja kulinda amani ya dunia, ni mlingano wa vitisho.

Ndiyo maana katika ushindani huu unaoendelea mbinu zinazotumiwa ni tofauti, kwa mfano Iran inataka kuwa na uwezo wa kuisumbua Israel kijeshi kwa vita ya hapa na pale, ya kuvizia, kwa mfano kwa kutumia mgambo kutoka nchi kama Lebanon na hata Syria, ambako kuna vikosi vya Iran moja kwa moja.

Ikiwa inafaulu kuleta hali ya kupungua kwa usalama nchini Israel, inaweza kutumia silaha nyingine ya kuchochea machafuko ya kidini yakijificha kuwa ni madai ya 'kurudi makwao' ya Wapalestina waliofukuzwa katika mchanganuo wa kivita wa kuundwa kwa Israel mwaka 1948.

Machafuko yakizidi huku vikundi vinatumia silaha ndogo ndogo dhidi ya raia wa Israel na taasisi za Kiyahudi, inatazamiwa Wayahudi watakata tamaa, wafungashe.

Warudi Ulaya, halafu Waarabu watawale Palestina kama nchi yao ya jadi, iliyovamiwa na Wayahudi kupitia 'ukoloni' wa Uingereza.



# Wamachinga, Jiji watunishiana misuli

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAMACHINGA wenye vibanda vya biashara kuzunguka bustani ya Jiji la Mbeya, wameanza kutunishiana misuli na viongozi wa jiji hilo baada ya kugomea amri ya kuondoka kupisha uwekezaji mpya unaotarajiwa kufanyika eneo hilo.

Wafanyabiashara hao zaidi ya 300 walihamishiwa katika eneo hilo na uongozi wa Jiji la Mbeya mwaka 2010 baada ya Soko la Uhindini walipokuwa wanafanyia shughuli zao kuteketea kwa moto.

Wakizungumza jana, machinga hao walisema hawako tayari kuondoka katika eneo hilo kwa madai wanaotakiwa kwenda hawajaandaliwa mazingira rafiki ya kufanyia shughuli zao.

**Endapo jiji hilo linataka kuwaondoa, wao wanapendekeza watafutiwe eneo lingine ndani ya Kata ya Sisimba ili kuwarahishia kazi zao na sio katika kata zingine.**

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Jacob Fungo, alisema waliwekwa katika eneo hilo kwa mkataba wa kukaa kwa muda wa miezi 38 mwaka 2010 wakisubiri soko lililoungua lijengwe upya, lakini mpaka sasa ni zaidi ya miaka nane soko hilo halijajengwa.

Alisema endapo jiji hilo linataka kuwaondoa, wao wanapendekeza watafutiwe eneo lingine ndani ya Kata ya Sisimba ili kuwarahisishia kazi zao na sio katika kata zingine.

"Hapa tuliwekwa kwa muda, lakini pia tunakopelekwa wanadai tunapelekwa kwa muda, sasa sisi tunataka waturudishe kwenye eneo letu la Uhindini ambalo ndilo soko letu la asili na hata ramani ya Jiji inaonyesha kuwa ni soko," alisema Fungo.

Naye Edward Kanjelema, alisema walitiwa na uongozi wa Jiji Desemba mwaka jana na wakaambiwa kuwa amepatikana mwekezaji wa kuwekeza katika eneo hilo na hivyo wakawaeleza kuwa wangemleta ili azungumze nao na washauriane naye namna ya kuwekeza.

Alisema wakati wanasubiria mwekezaji huyo aende katika eneo hilo kwa ajili ya kushauriana nao, imekuja amri ya kuwataka waondoke na kwenda katika masoko ya Iyunga, Uyole na Nanenane ili kumpisha mwekezaji huyo.

"Sisi hapa tupo makundi mawili, wengine ni waathirika wa ajali ya moto iliyoteketeza soko la Uhindini na wengine waliondolewa na mkuu wa wilaya kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara, sasa wameanza wanatuchanganya na sisi tunawaambia hatupo tayari kuondoka," alisema Kanjelema.

Joseph Makwamba, alisema wamekuwa wakihangaishwa kwa muda mrefu na uongozi wa Jiji, hali inayowafanya waonekane wapinzani wa serikali wakati sio kweli.

Alisema kutokana na kuhangaishwa huko waliamua kuandika barua za malalamiko kwenda kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Waziri Mkuu na Rais wakiomba wasaidiwe.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji, Dk. Amani Kilemile, alisema wameshafanya mazungumzo na Benki ya Dunia kwa ajili ya kufanya maboresho ya bustani hiyo na kuwekeza upya. Alisema kabla maboresho ya bustani hiyo, wamachinga hao wanatakiwa kuondoka ili kuepusha bughudha wakati maboresho yatakapokuwa yanafanyika.

"Wao kama hawataki kwenda kwenye masoko tuliyowaelekeza wanaweza kutafuta wenyewe maeneo ambayo ni rasmi ili wakafanye shughuli zao huko, lakini sisi tumewataka waende Airport ya zamani, Iyunga au Nanenane na masoko mengine yenye nafasi," alisema Kilemile.

Alisisitiza kuwa maeneo yote ambayo yanafanyiwa marekebisho likiwamo eneo la stendi kuu, wafanyabiashara wanatakiwa waondoke na kwamba wengine wote wamekubali isipokuwa wa City Garden.

## Waombwa kuboresha miundombinu ya shule

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, amewashukia viongozi wa chama hicho ngazi ya mashina na kata wanaoisema vibaya serikali wakidai haitekelezi baadhi ya mambo akiwataka kuacha mara moja tabia hiyo.

Mangula aliwashukia viongozi hao jijini Mbeya alipokuwa akifungua sherehe za maadhimisho ya miaka 42 ya kuzaliwa kwa CCM ambapo alisema wanatakiwa kutumia vikao halali vya chama kuishauri serikali badala ya kulaumu.

Aliwashauri viongozi hao kukaa vikao vya kila mwezi kwa mujibu wa kanuni za vikao vya chama hicho na kujadiliana kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

"Wakati tunasheherekea miaka 42 ya kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi mimi pia nasherehekea miaka 42 ya utumishi wangu ndani ya chama, namshukuru Mungu, mwaka huu tumekuja na utaratibu ambao kila kiongozi wa chama anasherehekea kwenye mkoa ambao yeye ni mlezi," alisema Mangula.

Alisema yeye ni mlezi wa chama katika mikoa ya Mbeya na Songwe hivyo akasisitiza kuwa hapendi kuona viongozi wa chama kwenye Mkoa ambao yeye ni mlezi wanakuwa sehemu ya wanaoinyooshea serikali vidole.

Aliwasisitiza viongozi wa ngazi za chini za chama kufanya vikao vya ngazi zao kila mwezi huku akifafanua kuwa maeneo ya vijijini wajumbe wanatakiwa kuwa 30 na mijini wajumbe 50.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya, Solomon Itunda, alisema utaratibu wa walezi kusheherekea kwenye mikoa yao imesaidia kuwaweka karibu viongozi mbalimbali na kutatua changamoto kwa pamoja.

Alisema Mkoa wa Mbeya utahakikisha kila kiongozi wa balozi na tawi anaitisha mikutano ya mashina na kwamba yeyote atakayekwenda kinyume atachukuliwa hatua.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akisikiliza maelezo kutoka Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Dk. Amani Kilemile, kuhusu ukarabati wa Shule ya Msingi Sisimba, jijini humo jana. Wa (pili kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika na (kulia) ni Diwani wa Sisimba, Geofrey Kajigili. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DED awafafanulia madiwani ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, amelihakikishia Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa kuwa maeneo yote ya ardhi ambayo halmashauri iliyauza kwa kufuata utaratibu, huku akiwaonya wenyeviti wa mamlaka hiyo kuacha kulalamika bila kuwa na uthibitisho.

Msangi aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Mamlaka Mji Mdogo Rujewa baada ya kuibuka malalamiko kutoka kwa wenyeviti wa vitongoji juu ya uuzaji wa eneo la serikali lililoko karibu na benki ya CRDB kwa mtu binafsi.

Alisema uuzwaji wa eneo hilo ulizingatia sheria na taratibu na kwamba kama wenyeviti hao wanahisi serikali imeuza kiholela kikao kijacho wataleta taarifa hizo kwa maandishi pamoja na nyaraka zake.

"Kamwe hatuwezi kuuza maeneo ya serikali kiholela tunayafanya wote tukikubaliana na ninyi wenyeviti ni sehemu ya makubaliano haya kwanini leo mnalalamika nawaomba kikao kijacho tuwaletee nyaraka zote za uuzaji ardhi," alisema Msangi.

Msangi aliwaasa wenyeviti hao kuwa ili wafanye vizuri hasa kwenye masuala ya ardhi ni vyema wasiwe sehemu ya matatizo na kuleta migogoro inayohusu ardhi.

Alisema baadhi ya maeneo ya vijijini wenyeviti wa vitongoji wamekuwa wakilalamikiwa katika suala la ardhi na kusababisha kuwapo kwa migogoro mingi.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mbuyuni, Bob Hamis, aliiomba serikali kutoa majibu sahihi juu ya uuzwaji wa eneo linalolalamikiwa na wenyeviti hao.

Alisema wanaamini uuzwaji wa eneo hilo haukuzingatia utaratibu unaofaa jambo ambalo limeleta sintofahamu kwao.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa, Chameta Godgod, alisema majibu ya Mkurugenzi ni kwamba eneo hilo lilishafanyiwa mchakato wa uuzaji tangu mwaka 2012.

"Kupitia baraza letu tunaomba eneo hilo lisiendelezwe mpaka mpate majibu kamili juu ya uuzaji wa eneo hilo la serikali kwa mtu binafsi," alisema mwenyekiti huyo.







Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), Margaret Sitta (katikati), akifafanua jambo wakati wa semina ya kushauriana na kujadiliana kujenga vituo kwa ajili ya wanawake wanaoathirika kijinsia jijini Dodoma jana. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Umoja huo, Susan Lyimo na Katibu, Lolensia Bukwimba. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Waziri azuia kuwekwa ndani daktari, muuguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewataka viongozi wa kisiasa kuacha tabia ya kutumia nafasi zao kuwaweka ndani (mahabusu) wauguzi na madaktari.

Mwalimu aliyasema hayo juzi alipokuwa akizindua kampeni ya 'Wauguzi sasa' jijini Dodoma.

Alisema kiongozi kumweka mahabusu muuguzi au daktari hakusaidi bali wanachotakiwa kufanya ni kuwaita na kuongea nao pale wanapoona wanakwenda kinyume cha kanuni.

**Wauguzi wengi ni wazuri sana, lakini katika wengi wabaya hawakosekani wale wenye lugha za matusi kwa wagonjwa na zile sizizo na staha wapo hivyo, basi tushirikiane katika kuwafichua hawa.**

"Muuguzi naye ni binadamu, anahitaji kuheshimiwa na kutambuliwa kazi yake, lakini hii tabia ya kuwaweka ndani haitusaidii kabisa...nashukuru Waziri wa Tamisemi, Jafo, jambo hili alishalitolea ufafanuzi," alisema Mwalimu.

Aidha, aliwataka wauguzi kufanya kazi kwa kuzingatia miongozo na maadili, kwa kuthamini heshima na utu wa wagonjwa.

"Wauguzi wengi ni wazuri sana, lakini katika wengi wabaya hawakosekani wale wenye lugha za matusi kwa wagonjwa na zile sizizo na staha wapo hivyo, basi tushirikiane katika kuwafichua hawa na tusimvumilie yeyote ambaye anaichafua kada yetu hii ya uuguzi," alisema Mwalimu.

Pia, alisema serikali itaendelea na juhudi za kuboresha mazingira ya wauguzi kwa kuhakikisha kuwa dawa na vifaa tiba vyote vinakuwapo katika maeneo yao ya kazi.



Vilevile, Waziri Mwalimu, alisema kuwa iko haja ya wizara kuwa na mtaala mmoja wa kufundishia katika vyuo vinavyotoa mafunzo ya uuguzi nchini ili kuondoa mkanganyiko ulipo sasa.

Naye Rais wa Chama cha Wauguzi na Wakunga nchini, Paul Magesa, alisema kuwa lengo ni kuhakikisha kuwa wagonjwa wanaofika katika hospitali mbalimbali nchini wanapata huduma kwa muda mfupi.

"Hivi sasa pamekuwa na changamoto ya wagonjwa kulalamikia kuwa muda mwingi wanaupoteza hospitalini kutokana na kuzungushwa muda mwingi huku na kule," alisema Magesa.

Hata hivyo, alisema kuwa kampeni hiyo ya uuguzi iliyozinduliwa inalengo la kuinua kada ya uuguzi nchini.

# Walilia fidia yao kupisha Tanesco

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa Kijiji cha Michese nje kidogo ya Jiji la Dodoma, wanaiomba serikali kuingilia kati suala la malipo yao wanayolidai Shirika la Umeme nchini (Tanesco), baada ya kuondolewa katika makazi yao ili kupisha mradi wa kuzalisha umeme kwa nguvu ya jua.

Katika mradi huo kaya zaidi ya 50 zilikumbwa katika zoezi hilo, huku wakazi wapatao 100 wanaishi kwa majirani kutokana na kukosa makazi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari kijijini hapo, wakazi hao walisema kuwa wanaiomba serikali kuingilia kati madai yao ili waweze kupata haki yao.

Mwenyekiti wa kijiji hiko, Sangali Masibe, alisema tangu mwaka 2012, walipatiwa maelekezo kuwa wasikarabati nyumba zao ambazo zitapitiwa na mradi huo, jambo ambalo linachangia wao kukosa mahali pa kuishi kutokana na nyumba zao kubomoka kwa mvua.

"Tunaomba mtusaidie tulipwe pesa zetu, hatuna fedha za kupanga nyumba na hapa tumeambia tusikarabati, lakini fedha zetu za fidia hatuzipati," alisema.

Aliongeza kuwa wanatakiwa waambiwe kama hakuna malipo wakarabati ili waendelee kukaa na familia zao.

Alifafanua zaidi kuwa kaya zaidi ya 50 zote wakazi wake wametakiwa kutoka ikiwamo mashamba yao ambayo wanayatumia katika kujipatia riziki zao.

Victoria Jeremia, mkazi wa kijiji hicho, alisema kwa sasa wamekaa hawaelewi chochote kwa kuwa mahitaji yao yamesimama.

Alisema hawana shida ya kulumbana isipokuwa wanahitaji haki yao ambayo wamekuwa wakipigwa danadana kila wakati bila kufikia mwafaka.

Akijibu malalamiko hayo, Ofisa Habari wa Tanesco mkoani Dodoma, Innocent Lupenza, alisema alithibitisha wananchi hao wanadai, lakini wanatakiwa kwenda kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi ili kujua haki zao wanazipataje.

"Nawaomba waende kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi jibu lao litapatikana ," alisema Lupenza.

# Wasaidizi wa sheria kunolewa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAASISI ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (The Law School of Tanzania) iko katika hatua za mwisho za mchakato wa kuanzisha mafunzo kwa ngazi ya cheti cha wasaidizi wa kisheria.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Habari, Elimu na Mawasiliano wa Law School, Scholastica Njozi, kwenye maonyesho ya Wiki ya Sheria yanayofanyika jijini hapa.

Alisema Law School imemaliza mchakato wa awali wa maandalizi ya mtaala na kwa sasa kinachosubiriwa ni idhini na usajili wa kozi kutoka NACTE kabla ya kuanza kutoa mafunzo hayo.

"Tunachosubiri kwa sasa ni idhini na usajili kutoka NACTE, mambo yakienda vizuri tutaanza kutoa mafunzo ya wasaidizi wa sheria kwa ngazi ya cheti (NTA level 4) na mafunzo yatakuwa kwa mwaka mmoja," alisema.

Law School inatarajia kutoa mafunzo hayo kutokana na serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kukasimu jukumu la kutoa mafunzo na kusimamia ubora wa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria nchini.

"Hii ni baada ya Bunge kupitisha Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 yenye lengo la kusimamia kwa ujumla utoaji wa msaada wa kisheria pamoja na vyombo vinavyohusika kutoa huduma hii kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za sheria nchini na kuboresha utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa jamii," alisema.

Aidha, Njozi alisema tangu kupitishwa kwa sheria hiyo, Law School imesimamia mafunzo ya kuwajengea uwezo wasaidizi wa sheria wapatao 2,400 kutoka nchi nzima ambao tayari walishapewa mafunzo hayo siku za nyuma.

"Lengo lilikuwa ni kuwajengea uwezo zaidi wa kuweza kutoa msaada wa kisheria kwa weledi na ufanisi na kwa kuzingatia sheria," alisema.



# Maandalizi ujenzi wa hospitali yaiva

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAANDALIZI ya ujenzi wa hospitali ya rufani ya Binguni Wilaya ya Kati yanaendelea vizuri baada ya eneo kupimwa na kuwekwa mipaka.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Asha Abdalla Juma, alisema hayo jana mbele ya Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, ofisini kwake wakati uongozi wa wizara ya afya ulipotakiwa kutoa ripoti.

Abdalla alisema maandalizi ya ujenzi wa Hospitali ya Binguni yanaendelea vizuri, huku akibainisha kuwa kwa sasa eneo limetambuliwa na kupimwa.

Katika hatua hiyo, alisema wamechukua hatua za awali za kupima na kuzungushia uzio kwa ajili ya kuepuka uvamizi.

Niabu Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, alisema kujengwa kwa hospitali hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar.

Alisema kujengwa kwa hospitali hiyo kwa kiasi kikubwa kutapunguza msongamano wa wagonjwa ambao walikuwa wakipata huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, mjini Unguja.

Aidha, alisema kujengwa kwa hospitali hiyo kunakwenda sambamba na ujenzi wa taasisi ya maabara ya maradhi mbalimbali katika majengo yaliyoko Binguni.

"Mikakati ya Wizara ya Afya ni kujenga Hospitali ya Binguni yenye hadhi ya rufani ambayo itakuwa na majengo ya taasisi ya utafiti wa maradhi mbalimbali," alisema.

Naye Balozi Iddi aliutaka uongozi wa Wizara ya Afya kulidhibiti eneo hilo ili kuepuka kuvamiwa na watu.

"Wizara ya Afya, watendaji mnatakiwa kuhakikisha eneo litakalojengwa hospitali ya rufani ya Binguni halivamiwi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba," alisema.

# Dk. Shein aipongeza Mahakama Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema taasisi za umma zinathamini mchango mkubwa wa serikali katika kufanikisha mageuzi ya kiutendaji, ili kufanikisha dhana ya utoaji bora wa haki katika jamii.

**Serikali katika vipindi mbalimbali na awamu zote saba, imefanya jitihada kubwa kuimarisha taasisi za umma ili kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa jamii unakua siku hadi siku.**

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar mjini Wete, Pemba jana, Dk. Shein alisema kutokana na mchango huo, shughuli za mahakama zimeimarika, hasa baada ya serikali kuteua majaji, mahakimu na makadhi wapya katika ngazi zote za mahakama Unguja na Pemba.

Alisema kwa nyakati tofauti, watendaji wa taasisi hizo wamepata mafunzo ya ndani na nje ya nchi, hivyo kujenga uwezo katika kufanikisha dhana ya serikali ya upatikanaji wa haki bora kwa jamii.

Dk. Shein pia aliwahimiza wananchi wote kuendelea kutii sheria za nchi kama Katiba inavyoelekeza, huku akiwahimiza viongozi wa dini zote zinazofuatwa na wananchi wa Zanzibar na Tanzania nzima kwa jumla kuendelea kuhubiri utii wa sheria za nchi.

Alisema kuwa serikali katika vipindi mbalimbali na awamu zote saba, imefanya jitihada kubwa kuimarisha taasisi za umma ili kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa jamii unakua siku hadi siku.

Rais pia alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya saba imefanya jitihada kubwa za kuimarisha taasisi za umma zinazosimamia haki na sheria, taasisi zinazoshughulikia huduma za jamii, elimu, afya, maji safi na salama, kilimo, miundombinu ya usafiri, utalii na michezo.

Dk. Shein alielezea kusikitishwa kwake na Jeshi la Polisi linavyoingilia vyombo vya sheria katika kupambana na rushwa.

Alisema kuwa hivi karibuni kumetokea jambo ambalo halileti picha nzuri hali iliyosababisha jeshi hilo kuanza kuwatisha wafanyakazi wa Taasisi ya Kupambana na Rushwa Zanzibar (Zaeca) na kusisitiza kuwa taasisi hiyo iachwe ifanye kazi kwa uhuru na sheria zilizowekwa.

Naye Jaji Mkuu, Omar Othman Makungu, aliipongeza serikali kwa kuanzisha mradi wa usalama na kufunga kamera za CCTV, hatua aliyosema itasaidia kuimarisha usalama wa mji pamoja na kubaini makosa mbalimbali yakiwamo ya usalama barabarani, hivyo kuipunguzia kazi mahakama.

Pia alisema Mahakama, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zinaridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kuimarisha miundombinu, upatikanaji wa vifaa na mafunzo kwa watendaji.



Viongozi na wananchi Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wakiangalia daraja la mto Bulunge, barabara kuu ya kutoka Kijiji cha Masuguru-Kerenge, jana, lililobomolewa na mvua toka mwaka jana. Sasa litajengwa upya na mkandarasi wa kampuni ya JJ Gwagisa Ltd pamoja na barabara ya kilomita moja kiwango cha lami na kilomita 3.5 kwa kiwango cha vumbi. Kushoto Mkandarasi wa kampuni hiyo, Andrew Kimonga na (wa sita kushoto) ni Meneja wa TARURA wilaya ya Muheza, Joseph Khahoza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali Zanzibar yaombwa kuajiri wataalamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetakiwa kuzipatia ufumbuzi baadhi ya changamoto ziliomo katika mpango wa ugatuzi kupatikana kwa watendaji wa kutosha katika fani mbalimbali.

Hayo yalisemwa na baadhi ya wafanyakazi wa Ofisi ya Halmashauri Mkoa wa Kusini Pemba mbele ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Haji Omar Kheir.

Juma Hamad, mfanyakazi katika sekta ya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba, alisema wanakabiliwa na uhaba wa walimu kutokana na wengi kufikia umri wa kustaafu.

Alisema hali hiyo imesababisha kuwepo kwa uhaba wa walimu wa masomo ya aina mbalimbali na wanafunzi kushindwa kufaulu vizuri.

Alisema mpango wa ugatuzi umepokewa vizuri Kusini Pemba na wananchi kushirikiana na viongozi, huku huduma muhimu zilioko katika mpango huo zikipatikana kwa walengwa.

"Mheshimiwa waziri, Mkoa wa Kusini Pemba tunatekeleza ugatuzi katika sekta tatu muhimu, lakini tunakabiliwa na uhaba wa wataalamu katika eneo la afya na elimu," alisema.

Katika sekta ya afya, baadhi ya madaktari wameitaka serikali kukamilisha ajira za wafanyakazi katika kada mbalimbali.

Maryam Hamad, msimamizi msaidizi sekta ya afya, alisema wamewasilisha maombi ya ajira kwa baadhi ya wafanyakazi wa kada muhimu katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

"Tunaomba maombi yetu ya ajira katika sekta ya afya yafikiriwe kwa sababu tunashindwa kutoa huduma za afya kwa ufanisi katika hospitali za wilaya," alisema.

Naye Waziri Kheir alisema changamoto zilizoko katika mpango wa ugatuzi wa kufikisha huduma muhimu za jamii kwenda kwa wananchi zitapatiwa ufumbuzi.

Alisema sekta tatu zimegatuliwa ambazo ni elimu ya msingi, kilimo na afya, huku lengo la serikali likiwa kuona wananchi wanapata huduma hizo kwa haraka.

"Kasoro zote zilizojitokeza katika mpango wa ugatuzi tutazifanyia kazi kikamilifu kwa ajili ya kukidhi malengo na matarajio ya wananchi wetu," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

### Uchaguzi wabunge Congo kufanyika Machi

**KINSHASA, Congo**

TUME ya Uchaguzi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), (CENI) imesema kuwa uchaguzi wa wabunge utafanyika katika maeneo ya Beni, Butembo na Yumbi Machi, 31 mwaka huu.

Uamuzi huo umeamuliwa katika mkutano wa CENI uliofanyika juzi. Uchaguzi Mkuu haukuweza kufanyika katika maeneo hayo Desemba 30, 2018.

Sababu ya kuahirishwa kwa uchaguzi huo katika maeneo ya Beni, Butembo na Yumbi ilikuwa ni mlipuko wa ugonjwa wa ebola huko Beni na Butembo, na katika eneo la Yumbi ilitokana na suala la mdororo wa usalama.

"Tume ya Uchaguzi ya Taifa imefanya kazi yake kwa kuweka ratiba kwa maeneo haya (Machi 31). Sasa, kazi kubwa itakuwa kwa wale wanaohusika na afya na vikosi vya usalama kutekeleza majukumu yao," alieleza ofisa mawasiliano wa CENI, Jean-Baptiste.

Ingawa Machi 31 iliamuliwa kwa uchaguzi wa wabunge, kikao cha CENI pia kimeamua kuwa tume mbalimbali zitatumwa katika maeneo hayo kuchunguza hali inayojiri.

Ugonjwa wa ebola tayari umeua watu 481 tangu ulipoanza Agosti mwaka jana katika eneo la Beni Mashariki mwa DRC. Ilikuwa sababu ya kuahirishwa kwa uchaguzi katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na Butembo. ***RFI***

### Mgomo waathiri wagonjwa hospitali za umma Kenya

**NAIROBI, Kenya**

MGOMO wa wauguzi ulioanza Jumatatu nchini Kenya katika majimbo 14, umewaathiri zaidi wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali za umma.

Hata baada ya Wizara ya Kazi na Wizara ya Afya kuunda jopo kazi la kutatua mgogoro huo, muungano wa wauguzi nchini humo bado unasisitiza kuwa hautashiriki mazungumzo ya aina yoyote yenye nia ya kusitisha mgomo huo, kwa kuwa unadai umechezewa sana na serikali.

Zaidi ya wauguzi 8,000 katika hospitali za umma wanaendelea kushiriki mgomo huo kuitaka serikali kuu na serikali za majimbo kutekeleza mkataba wa maafikiano unaowapa wauguzi malimbikizi ya marupurupu.

Mgogoro huo unatokana na serikali kuu na serikali za majimbo kushindwa kutoa mwongozo wa kutekeleza makubaliano ya kurejea kazini yaliyoafikiwa Novemba 2, mwaka juzi.

Katika mgomo huo, wauguzi wanalalamika kuwa hawajalipwa malimbikizo ya marupurupu ya mishahara hata baada ya kusainiwa makubaliano ya kufanya hivyo kati yake na baraza la magavana pamoja na Wizara ya Afya takribani miaka miwili iliyopita. ***VOA***

# Mawaziri Congo kulipwa mishahara hadi kifo

**KINSHASA, Congo**

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo imetetea maagizo yanayoruhusu mawaziri kulipwa mishahara na marupurupu kwa maisha yao yote.

Katika taarifa iliyotolewa juzi na serikali ilieleza kuwa malipo hayo sio ya kuwatajirisha maofisa.

Taarifa kutoka Congo zinaeleza kuwa maagizo mawili yanayoruhusu mawaziri kupokea marupurupu ya kiwango cha chini zaidi ya Dola za Marekani 2,000 yameshutumiwa vikali.

Wadau nchini huo wameeleza kuwa litakuwa ni jambo la ajabu viongozi hao kulipwa kiasi hicho cha fedha maishani mwao wakati kuna idadi kubwa ya raia nchini Congo wanaishi katika umaskini.

Serikali inayoondoka madarakani ilikuwa inawapatia mawaziri kiwango cha chini cha mshahara kuwatosheleza mahitaji yao ya kimsingi, kama chakula, makazi na huduma ya afya. Malipo hayo ni ya kuwaepusha kuishia katika umaskini.

Maagizo hayo mawili, yaliotiwa saini na Waziri Mkuu anayeondoka, Bruno Tshibala, Novemba mwaka jana yaliripotiwa katika vyombo vya habari.

Agizo la kwanza linawapa mawaziri wakuu mishahara ya kila mwezi ambayo ni asilimia 30 ya mshahara anaopokea sasa waziri mkuu, tiketi ya mara moja ya ndege kwa mwaka na marupurupu ya nyumba yenye thamani ya Dola za Marekani 5,000.

Agizo la pili linawapa mawaziri mishahara sawa na asilimia 30 ya mawaziri wa sasa na Dola za Marekani 1,000 kila mwezi kulipia makazi. Pia wanapokea tiketi ya mara moja kwa mwaka ya ndege.

Maagizo hayo yalishutumiwa vikali na watu wengi nchini Congo, hususani katika nyanja zote za kisiasa.

Mshauri wa rais wa zamani wa Congo, Joseph Kabila, alisema maagizo hayo hayaendani na mtazamo wa kiuchumi na kijamii.

Licha ya pingamizi hizo, serikali imetetea maagizo hayo na kueleza kwamba hayatozingatia mawaziri wa awamu iliopita, badala yake ni kwa mawaziri walioko kwenye serikali ya sasa na serikali zijazo.

Rais mpya wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Felix Tshisekedi, aliapishwa madarakani mwezi uliopita, akipokea 'kijiti' kutoka kwa Kabila katika ukabidhi wa kwanza wa madaraka uliofanyika kwa amani katika nchi hiyo na uliowahi kushuhudiwa katika miaka ya 60. ***BBC***



Kansela Angela Merkel wa Ujerumani (kulia), akiwa kwenye mazungumzo na mfalme wa Japan, Akihito (kushoto), nchini Japan. **PICHA ALLIANCE**

# Ujerumani na Japan ushirikiano zaidi

**TOKYO, Japan**

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merke, amefanya mazungumzo na mfalme wa Japan, Akihito kabla ya kuhitimisha ziara yake ya siku mbili nchini humo. Mataifa hayo yamekubaliana kushirikiana zaidi.

Merkel alifanya mazungumzo na mfalme Akihito jana, kabla ya kuhitimisha ziara yake ya siku mbili nchini humo, kabla ya kukutana na mwana mfalme ambaye anayetaraji kurithi kiti hicho hivi karibuni.

Kansela Merkel alikutana na mfalme huyo mkongwe wa miaka 85, aliyeamua kulivua taji lake Aprili 30, tukio ambalo ni la aina yake kuwahi kushuhudiwa tangu miaka 200 iliyopita nchini humo. Kwenye ziara hiyo, Kansela Merkel pia alikutana na mrithi wa kiti cha ufalme, Mwanamfalme Naruhito atakayekabidhiwa wadhifa huo Mei mosi inayokuja.

Merkel inakuwa ni ziara yakeya tano nchini humo ikiwa ni siku tatu tu baada ya makubaliano ya ushirikiano wa kikanda wa kiuchumi, EU-EPA ambayo ni makubwa zaidi ya biashara huru yaliyofikiwa kati ya Japan na Umoja wa Ulaya (EU) yaliyoanza kutekelezwa Februari Mosi. Makubaliano hayo yanafikia theluthi ya uchumi wa dunia. Kansela Merkel alisema kuwa hatua hiyo ni ujumbe tosha kwa dunia.

Jana, Merkel alikutana pia na Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe na kujadiliana kwa kina masuala kadhaa kuanzia uchumi hadi teknolojia.

Kwenye mkutano wa pamoja na waandishi wa habari baada ya mazungumzo hayo, Abe alisema Japan na Ujerumani zinatarajia kuongoza ukanda huo mkubwa zaidi wa kiuchumi duniani.

"Japan na Ujerumani zitakuwa vinara wa ukanda huu mkubwa zaidi wa uchumi huru, ulioanzishwa chini ya mkataba wa mashirikiano ya kiuchumi, EPA, na ulioanza kutekelezwa siku ya kwanza ya mwezi huu. Kwa mantiki hiyo, tunatakiwa kupunguza athari za Brexit kwa Umoja wa Ulaya na uchumi wa kidunia kwa ujumla," alisema Abe.

Aidha, wakuu hao wamekubaliana kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na kuhamasisha ushirikiano katika eneo la teknolojia ya juu ikiwa ni pamoja na ujasusi bandia na makubaliano ya msingi kuhusu usalama wa taarifa. ***DW***

# Mawaziri wakagua umeme wa maji

Na Mwandishi Wetu

MAWAZIRI wanaohusika na utekelezaji wa mradi wa umeme wa maji wa Rusumo (MW 80) wa Tanzania, Rwanda na Burundi wamekagua kazi ya ujenzi wa mradi huo, wilayani Ngara Mkoa wa Kagera na kutoa maelekezo mbalimbali.

Mapendekezo hayo ndiyo yatakayowezesha kasi ya utekelezaji wa mradi huo kuongezeka.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ndiye aliyewaongoza Waziri wa Nishati na Waziri Migodi wa Burundi, Come Manirakiza na Waziri wa Miundombinu wa Rwanda, Claver Gatete, katika kukagua kazi mbalimbali zinazoendelea kufanyika ukiwamo ujenzi wa eneo itakapojengwa mitambo ya kuzalishia umeme na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi.

Baada ya kukagua kazi zinazoendelea kufanyika, mawaziri hao walifanya kikao chini ya uenyekiti wa Dk. Medard Kalemani na kuiagiza Bodi ya Wakurugenzi ya mradi huo kusimamia ipasavyo kazi za ujenzi ili mradi huo ukamilike mwaka 2020 kwa mujibu wa makubaliano.

Dk. Kalemani alisema kazi ya ujenzi wa mradi huo ilianza Februari, 2017 na inapaswa kukamilika ndani ya miezi 36, hivyo bodi hiyo yenye wajumbe kutoka nchi zote ihakikishe mkandarasi anakamilisha kazi kwa wakati.

"Pia tumeiagiza bodi na wataalamu walioko katika mradi huu, wahakikishe wanashirikisha mamlaka na taasisi mbalimbali zilizopo katika maeneo ya mradi katika nchi zote tatu hasa katika masuala yanayohusu jamii zinazozunguka mradi na stahili za wafanyakazi ili kutokuwa na vikwazo katika utekelezaji," alisema Dk. Kalemani. Alisema kila nchi itapata megawati 27 na kujenga miundombinu ya usafirishaji umeme wa KV 220, ambapo kwa upande wa Tanzania, itajengwa miundombinu hiyo kutoka Rusumo kwenda Nyakanazi kwa umbali wa kilometa 98.

Aliongeza miundombinu hiyo ya usafirishaji umeme kwa upande wa Tanzania, itaingiza umeme katika gridi ya taifa kupitia njia ya umeme inayotoka Geita na kwamba, vijiji 13 vinavyopitiwa na mradi wa Rusumo vitasambaziwa nishati hiyo.

# Majaliwa: Uelewa wa sheria unachangia kupoteza haki

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi wayatumie ipasavyo maadhimisho ya Wiki ya Sheria ili waweze kupata elimu na huduma mbalimbali za kisheria.

Maadhimisho hayo yalifanyika jijini Dodoma na yalihudhuriwa na watu mbalimbali, wakiwamo wadau wa sheria, huku mgeni rasmi akiwa ni Majaliwa.

Majaliwa alisema wananchi wa mikoa mbalimbali, ukiwamo Dodoma, wanatakiwa kutumia maadhimisho hayo kwa kujitokeza kwa wingi kupata elimu na kwa wale wenye matatizo ya kisheria kuyaeleza ili yatatuliwe.

"Kwa yule ambaye hana tatizo, aje kupata elimu ya sheria, kutoa maoni au mapendekezo yake kuhusu mfumo mzima wa utoaji wa haki. Waswahili husema, elimu haina mwisho. Kwa kuwa elimu ya sheria imesogezwa hapa Dodoma, tumieni fursa hii kujifunza kadri iwezekanavyo," alisema.

Waziri Mkuu alibainisha kuwa serikali imeendelea kushirikiana na mhimili wa Mahakama katika kuhakikisha huduma bora za utoaji haki zinawafikia wananchi kwenye maeneo wanayoishi kwa wakati.

"Serikali ni mdau muhimu wa Mahakama na inafuatilia kwa karibu changamoto zote zinazoikabili pamoja na wadau wengine katika mfumo wa utoaji haki," alibainisha.

Alisema dhamira ya Mahakama kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), katika kuleta mabadiliko ya utoaji haki ni hatua nzuri na itasaidia kuboresha utoaji wa haki kwa wakati.

Aliwasihi watumishi wa Mahakama kujikita katika matumizi ya mifumo ya Tehama bila kukatishwa tamaa na changamoto zitakazojitokeza kwa kuwa mara nyingi kitu kipya chochote hakikosi changamoto za hapa na pale.

"Binafsi naunga mkono uamuzi wa Mahakama kutumia Tehama katika usajili wa mashauri, kwa kuwa unakwenda sanjari na azima ya serikali kuhakikisha Tehama inatumika vema kwenye taasisi za umma," alisema.

Aliongeza kuwa matumizi ya Tehama katika taasisi za umma yanalenga kutoa huduma bora na kuipunguzia serikali na mihimili mingine gharama za uendeshaji, hususan katika utoaji huduma kwa wananchi.

Alisema lengo la serikali ni kuona huduma bora zinawafikia wananchi kwa urahisi na pia zinapatikana kwa wakati.

Jaji Mkuu, Prof. Ibrahimu Juma, alisema kwa kipindi cha wiki nzima, maonyesho ya Wiki ya Sheria yatafanyika jijini Dodoma na kwenye Mahakama zote nchini, kuanzia ngazi ya wilaya.

Prof. Juma alisema kupitia maonyesho hayo, wananchi watakaoshiriki na kutembelea mabanda, watapata elimu na kutathmini umuhimu na hadhi ya mfumo wa kimahakama katika kustawisha maisha yao pamoja na kuwasaidia kupata haki kwa mujibu wa sheria.

"Kujikumbusha umuhimu wa mahakama kutoa haki kwa wakati, kuzingatia misingi ya maadili na mahakama kuendeleza programu za maboresho yanayolenga kupeleka huduma za utoaji haki karibu zaidi na wananchi," alisisitiza.



Baadhi ya vijana walioko katika majukwaa ya vijana, wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam wakiwa kwenye mkutano wa kupokea mrejesho wa maendeleo ya biashara uliandaliwa na taasisi ya Mpakani Tunaweza na kuwashirikisha viongozi kuanzia ngazi ya mtaa na wilaya, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wasimamishwa tuhuma kutoa lugha chafu kwa mgonjwa

Na Margaret Malisa, KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarest Ndikilo, amewasimamisha kazi watumishi wanne wa Kituo cha Afya cha Mkoani, kilichoko Kibaha, walioalamikiwa kutoa lugha chafu kwa mgonjwa. Akizungumza na waandishi wa habari akiwa mjini Bagamoyo katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo, Mhandisi Ndikilo, aliwataka watumishi wote mkoani Pwani kufanya kazi kwa weledi na kufuata taratibu na sheria za kazi.

"Nitumie fursa hii kuwataka watumishi wote wa Mkoa wa Pwani kuwa na lugha nzuri katika kuwahudumia wananchi, na endapo kuna wengine wana tabia kama hizo tutawachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwasimamisha kazi," alisema Ndikilo. Pia aliwataka wananchi kuendelea kuchangia ujenzi wa madarasa ili watoto waliofaulu na kushindwa kuendelea na kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, waende shule.

Akiwa katika Kijiji cha Kongo alizungumza na wanufaika wa miradi ya Tasaf, aliwataka watumie vizuri fedha wanazopata kwa kufungua miradi ili kujikomboa na umaskini.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

### ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute. Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii.Mawasiliano:0767574701/0758753063.www.tracdi.ac.tz

### NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU**


---

Yetu Microfinance Bank PLC

**Wekeza nasi katika akaunti maalum upate faida kubwa.**

**Muda wa uwekezaji:**
Miaka miwili

Kwa mwekezaji mwenye kiasi cha zaidi ya million 50, tafadhali piga simu 0762623062

**Unaweza kuwekeza kuanzia shilingi million moja kwa faida ya hadi 13%**

215048502

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI NA TRAILER

**SAID MOHAMED TIMBULO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 308 DJV SCANIA.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 172 CYP TRAILER.**

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**OB/RB/1235/2019.**

115047902

---

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**UPENDO PETER GEMBE** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba **T 409 CJP** na T680 CJP aina BOXER yenye chassis namba **MD2A21BZ2DWL10518** na MD2A21BZ1DWL10509,engine namba **PFZWDL17083** na **PFZWDL17118**

Yeyote atakaeiona atoe taaarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya polisi
**WMB/RB/1513/2019**

115047202

---

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PETER FRANK KEFAS GEMBE** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba **T644 CJR** aina ya TVS yenye chassis namba **MD6M14PK8D4883395** na,engine namba **0K4BD1116671**

Yeyote atakaeiona atoe taaarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

**Taarifa ya polisi**
**WMB/RB/1513/2019**

115047102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;08/2019**
Ombi la **KASSIM ABDALLAH MPONDA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **AMRI KASSIM ABDALLAH**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/01/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 08/01/2019
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115048002

---

### KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**FLORANCE MASEBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina TOYOTA HARRIER yenye namba za usajili **T 232 CCF.** Chassis Namba **SXU100033684,** Engine Namba 5S1024196.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DOM/TR/RB/171/2019.**

215047602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:230....2018**

**Mdai: SALOME MZAVA**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: TWAHA MOHAMED**

**Kwa: TWAHA MOHAMED KIHONDA - MOROGORO**

**Ombi la Mdai/Mwombaji/Msimamizi:**
**SALOME MZAVA**

**Madai ya: PESA SHILINGI 1,079,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 13 mwezi 02 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 28 mwezi 01 mwaka 2019.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

115048202

---

### NYUMBA INAUZWA

Nyumba inauzwa ipo maeneo ya tabata chan'gombe.

Ina vyumba vya kulala vitatu, kimoja ni master. Ina store, Jiko, Sebule, dining na Parking ya kutosha.

**Bei ni nafuu sana.**

**Mawasiliano: 0786058343/ 0622 096682 /0654 969280**

---


*Kwa Habari*

*Motomoto usikose*

*Gazeti lako la*

*The Guardian*

*kila siku*

---

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# Jurgen Klopp alia na mshika kibendera

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema maamuzi ya mwamuzi msaidizi yaliathiriwa na makosa ya bao la Sadio Mane dhidi ya West Ham.

Bao la Mane lilihesabiwa licha ya James Milner kuonekana kuwa ameotea.

Michail Antonio aliisawazishia West Ham kabla ya mapumziko, lakini Klopp amesema mwamuzi, Kevin Friend, hakutaka kufungua pengo zaidi katika kipindi cha pili.



"Nilisikia kwamba goli lilikuwa la kuotea, nina uhakika kwamba mwamuzi alijua hilo," alisema Klopp akiiambia BBC Sport baada ya kutoka sare ya 1-1.

"Katika hali ya 50-50 ilikuwa mpira wa adhabu ndogo kwa timu nyingine, kitu ambacho kilikuwa kigumu na hakikufanya maisha yawe rahisi."

Akizungumza na Sky Sports, kocha huyo raia wa Ujerumani aliongeza kusema: "Kama binadamu, kama ningejua nimefanya makosa makubwa kipindi cha kwanza, singetaka kuongeza makosa mengine.

"Waamuzi mara zote ni wanadamu, na nalielewa hilo, lakini sikufanya hivyo wakati wa mchezo kwa sababu sikuwa na ushahidi kama goli letu lilikuwa la kuotea."

Liverpool wangeweza kupata ushindi kupitia Divock Origi kwa shuti lake la dakika za mwisho, ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alionekana kuwa ameotea.

Kocha wa West Ham, Manuel Pellegrini pia alizungumzia maamuzi ya mwamuzi akisema, ilikuwa ni ngumu kuelewa kwa maamuzi yake.

"Bao na nafasi ya Origi lilikuwa ni kosa kubwa kwa mwamuzi msaidizi,"

# Mwili waonekana kwenye mabaki ya ndege ya Sala

**LONDON, England**

MWILI mmoja umeonekana chini ya bahari kwenye mabaki ya ndege ambayo alikuwa amepanda mchezaji Emiliano Sala na rubani, David Ibbotson.

Msako wa chini ya bahari Jumapili ulibaini mabaki ya ndege aina Piper Malibu nje kidogo ya Kisiwa cha Guernsey, takriban wiki mbili tangu ilivyopotea.

Idara ya Uchunguzi wa Ajali za Ndege ya Uingereza (AAIB), ilithibitisha Jumatatu kuonekana kwa mabaki hayo na kuwa mwili wa mtu mmoja umeonekana.

Ndege hiyo ilipotea Januari 21, mwaka huu ikiwa imembeba mshambuliaji huyo raia wa Argentina mwenye miaka 28. Sala alikuwa anatoka Ufaransa kwenda Wales baada ya kukamilisha usajili wa pauni milioni 15 kutoka Nantes kwenda Cardiff City.

"Kifaa kinachofanya uchunguzi (ROV), kimebaini mabaki hayo, na kwa masikitiko makubwa kuna mwili mmoja ambao unaonekana kwenye picha tuliyoinasa. Sasa tunachukua hatua za ziada za kuongea na familia za abiria na rubani pamoja na polisi," taarifa ya AAIB imeeleza.

AAIB pia imesema inatarajia kutoa taarifa ya awali juu ya ajali hiyo ndani ya mwezi mmoja tangu kutokea kwa ajali.

Bado maamuzi hayajafanyika iwapo mabaki hayo yaliyopo mita 63 chini ya bahari (sawa na futi 207) kuwa yatatolewa mpaka ardhini ama la.

Msako wa ndege hiyo ulisitishwa siku chache kutoka ilipotokea ajali, hata hivyo mchango wa kwenye mtandao ulioanzishwa na wakala wa Sala pamoja na familia yake ulikusanya pauni 324,000 ambazo zimetumika kufadhili msako uliogundua mabaki ya ndege hiyo.

Mito inayoaminika kutoka kwenye ndege hiyo ilipatikana ufukweni katika eneo la Surtainville, nchini Ufaransa wiki iliyopita.

Huzuni ilitanda na salamu za rambirambi kutumwa kwa wingi Jumamosi wakati Cardiff walipocheza mchezo wao wa kwanza nyumbani tangu mchezaji huyo alipopotea.

Kocha wa timu hiyo, Neil Warnock, amesema alihisi kuwa Sala alikuwa pamoja nao wakati wakiifunga Bournemouth mabao 2-0 katika mchezo wa Ligi Kuu England.

# Solskjaer
## atoa siri kubaki Man United

**MANCHESTER, England**

Ole Gunnar Solskjaer anamini yeye kocha sahihi wa Manchester United kama ambavyo anaelewa uhitaji wa kujitia majaribuni katika mashambulizi ya kushtukiza.

'Mashetani Wekundu' hao wameshinda mechi tisa na kutoka sare moja kati ya 10 kwenye mashindano yote chini ya kocha huyo wa muda, ambaye alipewa mikoba hiyo kutoka kwa Jose Mourinho aliyetimuliwa Desemba mwaka jana.

Mourinho mara nyingi alikosolewa kwa kuingiza mfumo hasi wa uchezaji hapo Old Trafford, wakati Solskjaer, ambaye ni kipenzi cha mashabiki katika miaka yake 11 akiwa United kama mchezaji, amevutia kwa kurejesha mfumo uliozoeleka klabuni hapo.

United imefunga mabao 25 katika mechi hizo 10 chini ya Solskjaer, yakiwa ni sawa na yaliyopatikana katika mechi 17 chini ya Mourinho, wakati wachezaji kama Marcus Rashford na Paul Pogba, ambao walishirikiana kupata bao la ushindi dhidi ya Leicester City Jumapili, wakifanikiwa.

Na Solskjaer, ambaye alihaha wakati akiwa Cardiff City kama kocha hivi karibuni, anaamini wale tu wanaoamini katika falsafa ya United katika kushambulia wanaweza kufanikiwa.

"Ni rahisi hapa kwa sababu ninajua vina saba [DNA] na utambulisho wa Manchester United ulivyo na wachezaji wa Manchester United walivyo," aliiambia Sky Sports.

"Ni utambulisho wa kushinda. Ni utambulisho wa kujiamini. Tunahitaji kujitia majaribuni. Tunahitaji kupata la pili, la tatu na bao la nne kwa sababu hivyo ndivyo tunavyofanya mambo Manchester United. Kama huwezi kuhimili hilo basi upo katika klabu isiyokufaa."

## HABARI MICHEZO




# MESSI, DEMBELE WAZUA HOFU BARCA

**BARCELONA, Hispania**

WAKATI Barcelona ikitarajiwa kuivaa Real Madrid kwenye mchezo wa Copa de Rey leo Jumatano, wachezaji Lionel Messi na Dembele wamezua hofu ya kuukosa mchezo huo utakaopigwa kwenye dimba la Nou Camp.

Messi ambaye ni nahodha wa timu hiyo, pamoja na Dembele kuna uwezekano mkubwa wa kuukosa mchezo huo ambao ni wa kwanza hatua ya nusu fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey'].

Dembele juzi alianza mazoezi ya kwake peke yake baada ya kukaa nje kwa wiki mbili akiuguza majeraha huku Messi akikosa kabisa kuhudhuria mazoezi kufuatia kuumia wiki iliyopita kwenye mchezo dhidi ya Valencia.

Mapema juzi kocha Ernesto Valverde alithibitisha kwamba, Messi ameumia baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kina na timu ya madaktari wa Barcelona kufuatia kuumia kwenye mchezo wa sare ya mabao 2-2 Jumamosi dhidi ya Valencia.

Barca walikuwa nyuma kwa mabao ya Kevin Gameiro na Daniel Parejo hadi Messi alipofunga mara mbili kuwaepusha na kipigo kwenye mchezo huo.

Lakini Messi alionekana kuumia misuli ya nyama za paja katika kipindi cha pili na alipata matibabu kabla ya kurudi tena uwanjani kuendelea kucheza.

"(Messi) alikuwa na tatizo dogo," alisema Valverde. Siwezi kusema kama atakosa mchezo wa Jumatano au la.

"Hadi asubuhi tutajua nini kitakachoendelea baada ya taarifa rasmi kutoka kwa timu ya madaktari. Kama yupo kwenye hali nzuri atacheza mchezo wa Jumatano."

# KAKA:
## Pogba alipanga kuondoka Man United



**MANCHESTER, England**

KAKA mkubwa wa Paul Pogba, Mathias, amesema nyota huyo wa Manchester United alipanga kuondoka klabuni hapo baada ya uhusiano wake na kocha wa zamani, Jose Mourinho kutetereka.

Akizungumza katika televisheni ya Ufaransa kwenye kipindi cha Telefoot, Mathias amesema hali kwenye uwanja huo wa Old Trafford ilikuwa ni kama sumu kwa mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi na hivyo mdogo wake huyo alijiandaa kuondoka kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

"Mambo hayakwenda vizuri chini ya Mourinho," alisema Mathias Pogba katika kipindi hicho.

"Bila shaka wakati ule alikuwa na mpango wa kuondoka, lakini sasa mambo yako vizuri. Sasa Solskjaer amemfanya kuwa mtu muhimu kwa timu, kuzungumza na mambo yamebadilika. Hicho ndicho kitu alichokuwa akikihitaji mdogo wangu."

Pogba na Mourinho walikuwa na matatizo kadhaa, hali iliyopelekea kila mmoja kuweka hisia zake hadharani. Pogba pia alikuwa akiachwa kwenye mechi kubwa na kocha huyo raia wa Ureno.

Mathias amesema mdogo wake kwa sasa anajisikia vizuri zaidi kwa kupewa uhuru na kocha mpya Ole Gunnar Solskjaer na ana nafasi ya kuonyesha kiwango chake na kipaji alichojaliwa.

Pogba amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi nane za Ligi Kuu England tangu Solskjaer alipochukua mikoba ya hapo Old Trafford.

# Bellirin akaribia kurejea Arsenal

**LONDON, England**

HABARI njema kwa kikosi cha Arsenal ni kutarajiwa kurejea dimbani kwa beki wake, Hector Bellerin ambaye aliumia mguu wake wa kushoto.

Bellerin amethibitisha kuanza kupona majeraha yake baada ya kukaa nje ya dimba takriban wiki nne.


Katika mchezo uliofanyika mwanzoni mwa Januari ambapo Arsenal waliitandika Chelsea 2-0 kwenye Uwanja wa Emirates, ulisababisha beki huyo kupata majeraha ya goti.

Baada ya kupata majeraha hayo na kusababisha kufanyiwa operesheni ya goti, beki huyo raia wa Hispania ameposti picha ikimuonyesha akiwa hospitalini na kusema kwamba anakaribia kurejea.

"Majeraha yangu yanaelekea kupona na naweza kurudi dimbani hivi karibuni," aliandika beki huyo kwenye mtandao wake wa Isntagram.



## DON ZA SOKA MAG YA ULAYA



# RAMOS AFURAHI KUBEBA JUKUMU LA RONALDO REAL

●●●'Panenka' ni namna ya kuzipiga, lakini kamwe sikutaka kumkasirikia...

**MADRID, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos ni mwenye furaha kubeba jukumu la kupiga penalti baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo.

Ramos kwa sasa ndiye aliyeshikilia jukumu la kupiga penalti Madrid baada ya Ronaldo kuachana na miamba hiyo ya La Liga na kujiunga na Juventus Julai mwaka jana.

Beki huyo tayari ameshafunga mabao 10 msimu huu na amesema ni jambo zuri kubeba jukumu hilo la Ronaldo, wakati pia akiongeza hakutaka kumkasirikia alipoamua kupiga 'Panenka' [penalti].

"Nimechukua majukumu haya baada ya Cristiano kuondoka na ni mwenye furaha kufanya hivyo," Ramos aliiambia Antena 3.

"['Panenka'] ni namna ya kuzipiga, lakini kamwe sikutaka kumkasirikia mwenzangu."

Madrid inajiandaa kwa mechi kubwa wiki chache zijazo ikiwamo ya Copa del Rey [Kombe la Mfalme] leo dhidi ya Barcelona, mchezo dhidi ya Atletico Madrid na wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax.

Ramos alisema utakuwa mwezi mkubwa kwa Madrid, ambayo ipo nafasi ya tatu kwenye La Liga na pointi nane nyuma ya Barca.

"Tunaivaa Barcelona, ambao ni vinara wa La Liga, na wapinzani wetu katika kombe," alisema.

"Pia tuna 'dabi' dhidi ya Atletico kwenye La Liga."

Madrid itashuka katika Uwanja wa Camp Nou leo kucheza mechi yake ya kwanza ya nusu fainali ya Copa del Rey.

## KWA UFUPI

### LIVERPOOL YAMPANIA INSIGNE

Liverpool imetoa ofa ya pauni milioni 61.3 kwa straika wa Napoli, Mtaliano Lorenzo Insigne, 27. ***(La Repubblica, via Sport Witness)***

### BARCA KUMSAJILI DE LIGT

Barcelona inataka kumsajili beki wa kati wa Ajax, Matthijs de Ligt, 19, katika majira ya kiangazi na itapaswa kulipa pauni milioni 65.8. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### BAYERN KUMRUDIA HUDSON-ODOI

Bayern Munich itarudi na pauni milioni 35 kutoa ofa kwa winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18, katika majira ya joto baada ya kushindwa kupata huduma ya nyota huyo wa kimataifa wa England U-19 kwenye dirisha la Januari. ***(Mail)***

### RONALDO AMTAKA RODRIGUEZ JUVE

Cristiano Ronaldo, 34, amemtaka mchezaji mwenza wa zamani katika kikosi cha Real Madrid, James Rodriguez, 27, ambaye anaichezea Bayern Munich kwa mkopo, kujiunga na Juventus. ***(Marca)***

### LIVER MAJARIBU KUMKOSA SALAH

Liverpool itajitia majaribuni ya kumkosa mshambuliaji Mmisri Mohamed Salah, 26, kama itashindwa kutwaa ubingwa wa EPL msimu huu, kwa mujibu wa straika wa zamani wa Wekundu hao wa Anfield, Emile Heskey. ***(Express)***

### RASHFORD, UNITED WATETA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na England, Marcus Rashford, 21, yupo katika mazungumzo ya mkataba mpya na klabu hiyo ambao utamfanya kulipwa mara mbili ya mshahara wake na kuwa zaidi ya pauni 150,000 kwa wiki. ***(Telegraph)***

### POCHETTINO AMGEUKIA JANSSEN

STRAIKA wa Tottenham, Mholanzi Vincent Janssen, 24, ameambiwa na kocha Mauricio Pochettino kuwa ataongezwa katika kikosi chake kitakachocheza mechi za EPL, licha ya kutojumuishwa tangu Agosti 2017. ***(Evening Standard)***

### EMERY KUPEWA PAUNI MIL. 40 TU

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery atapewa pauni milioni 40 za usajili majira ya joto, dirisha la usajili la Januari ameshindwa kusajili mchezaji wa kudumu. ***(Mirror)***

### 'MOURINHO ANGEMKIMBIZA POGBA'

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, alitaka kuondoka katika klabu hiyo wakati ikiwa chini ya kocha Jose Mourinho, kwa mujibu wa kaka wa nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Mathias. ***(Telefoot, via Mirror)***

### SCHURRLE KUIACHA FULHAM

MKATAKA wa mkopo wa miaka miwili wa mshambuliaji Andre Schurrle aliyetua Fulham akitokea Borussia Dortmund, utamalizika majira ya kiangazi - ikiwa ni mwaka mmoja mapema zaidi ya ilivyopangwa - kama 'Cottagers' hao watashuka daraja. ***(Kicker - in German)***

### ARSENAL KUSAJILI WATATU

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, anataka kusajili angalau wachezaji wapya watatu majira ya joto, ikiwa ni pamoja na beki mpya wa kushoto. ***(Mail)***

### HERTHA BERLIN YATUA LIVER

Hertha Berlin inataka kumsajili kwa mkopo kiungo wa Liverpool na Serbia, Marko Grujic, 22, mwishoni mwa msimu. ***(Liverpool Echo)***



HABARI MICHEZO

# AUSSEMS AUKUBALI USAJILI WA MAYANGA

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Simba Patrick Aussems, amesema anaufahamu uwezo wa mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Vitalis Mayanga aliyesajiliwa akitokea Ndanda FC kuchukua nafasi ya Shiza Kichuya ambaye ameuzwa Misri.

Aussems amesema anaamini mshambuliaji huyo atasaidia Simba kwenye michuano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na ile ya kimataifa wanayoshiriki.

"Nimeukubali usajili wa Mayanga, ni mchezaji mzuri ambaye naamini ataendana na kasi ya timu yetu, tumemwachia Kichuya kuondoka, hivyo ilikuwa lazima kupata mchezaji mwingine mbadala," alisema Aussems.

Alisema ataanza kumtumia baada ya kufanya mazoezi ya pamoja na wenzake kujiandaa na mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mwadui.

Simba inakabiliwa na mwezi mgumu ambapo Februari 12 itacheza na Al Alhy ukitanguliwa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mwadui, lakini pia Februari 16 ikicheza na watani zao Yanga kwenye Uwanja wa Taifa.

Mayanga, aliichezea Ndanda FC ya Mtwara kabla ya kusajiliwa na Simba kwenye dirisha dogo la usajili.



Mratibu wa hafla ya 'Mkeka na Mvinyo' kutoka Kampuni ya Real PR Solutions (RPR), Calorine Kirwanda, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hafla hiyo itakayohusisha wadau mbalimbali wa uzalishaji wa mvinyo hapa nchini pamoja na watumiaji wa kinywaji hicho itakayofanyika Februari 14, mwaka huu katika Hoteli ya Whitesands, jijini Dar es Salaam. Wengine ni pamoja na Meneja Mauzo na Masoko wa Kampuni ya TSN, Januarius Maganga (wa pili kulia), Afisa Uhusiano wa Kampuni ya GS 1, Clementine Kahamba (kushoto) pamoja na Meneja Uendeshaji wa Hoteli ya Whitesands, Ali Hilika. **MPIGAPICHA WETU**

# Valentine Dar ni 'Mkeka na Mvinyo'

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA Siku ya Wapendanao ('Valentine Day'), wadau mbalimbali wa uzalishaji wa mvinyo hapa nchini pamoja na watumiaji wa kinywaji hicho, wamejipanga kufurahia pamoja katika hafla maalum inayofahamika kama 'Mkeka na Mvinyo' itakayofanyika usiku wa Februari 14 katika Hoteli ya Whitesands jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa hafla hiyo kutoka Kampuni ya Real PR Solutions (RPR), Bi Calorine Kirwanda, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa, mbali na kuwakutanisha wadau muhimu wa kinywaji hicho, hafla hiyo inalenga kutoa fursa kwa watumiaji wa mvinyo hapa nchini kufurahia vinywaji tofauti vya aina hiyo vinavyozalishwa hapa nchini huku wakiwa wamekaa kwenye mikeka.

"Pamoja na kutoa fursa kwa watumiaji wa mvinyo siku hiyo kufurahia pamoja na wapendwa wao, usiku wa Mkeka na Mvinyo unalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kutangaza utalii na kukuza viwanda vya ndani kupitia uhamasishaji wa matumizi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ikiwamo aina tofauti ya mvinyo bora kabisa unaozalishwa hapa nchini.

"Upekee wa hafla hii unaanzia kwenye jina lake ' Mkeka na Mvinyo'. Hivyo basi itahusisha matumizi ya mikeka ambapo wageni wetu watapata fursa ya kuketi kwenye mikeka huku wakifurahia mvinyo bora unaozalishwa hapa nchini pamoja na nyama choma kadri ya matakwa yao," alisema.

Aliwataja baadhi ya wadau muhimu katika kufanikisha hafla hiyo kuwa ni pamoja na Hoteli ya Whitesands, Bodi ya Utalii Tanzania, (TTB), GS 1, pamoja na Kampuni ya Magazeti ya TSN wazalishaji wa Daily News pamoja na Habari Leo.

Kirwanda aliongeza kuwa hafla hiyo ni sehemu ya mkakati wa kampuni hiyo utakaozinduliwa hivi karibuni unaolenga kutangaza utalii wa ndani pamoja kuvumbua fursa mbalimbali za kibiashara ndani ya nchi kwa lengo la kukuza uchumi unaofahamika kwa jina la 'Domestic Tourism Promotion Initiative' (DTPI).

"Tunahitaji kuhamasisha zaidi matumizi ya bidhaa za ndani ili kukuza uchumi wetu kama taifa," aliongeza Kirwanda huku akitaja baadhi ya maeneo ambayo tiketi za hafla hiyo zinapatikana kuwa ni pamoja na Hoteli ya Whitesands na Shamo Tower Mbezi Beach.

Alisema, tofauti na mtu mmoja mmoja au kwa wale ambao watakuwa na wapendwa wao, Mkeka na Mvinyo inatoa fursa kwa mashirika na taasisi mbalimbali kufurahia pamoja katika dhana nzima ya kuonyesha upendo, shukrani na pongezi baina yao na wadau wao katika shughuli zao za kila siku huku wakifurahia mvinyo na chakula kizuri katika viunga vya Hoteli ya Whitesands.

"Ifahamike kwamba Siku ya Wapendanao sio kwa ajili ya wale wenye mahusiano ya kimapenzi tu bali pia inaweza kutumiwa na mashirika au taasisi mbalimbali lengo likiwa ni kuonyesha upendo, shukrani na pongezi kwa wafanyakazi, na wadau mbalimbali wanaoshirikiana nao katika shughuli zao za kila siku," alifafanua. Akizungumza kwenye hafla hiyo, Meneja Mauzo na Masoko wa Kampuni ya TSN, Januarius Maganga, alisema kampuni hiyo imeamua kuunga mkono mpango huo kutokana na kuguswa kwake na namna unavyolenga kuchochea harakati za masoko kwa bidhaa za ndani sambamba na kuunga mkono agenda ya serikali ya uchumi wa viwanda.

Kwa upande wake Afisa Uhusiano Mwandamizi kutoka Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Geofrey Tengeneza, alisema kupitia mpango huo mbali na kutangaza utalii wa fukwe pia utatangaza utalii wa asili kwa kuwa utahusisha mvinyo unaozalishwa hapa nchini huku watumiaji wakiwa wameketi kwenye mikeka ya asili.

## Sababu kuanguka Taarabu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KUTOFANYA vizuri kwa muziki wa Taarab asilia hapa visiwani Zanzibar, imetokana na kuongezeka kwa vikundi vingi vya muziki wa Taarab hapa nchini ambavyo vimeubadilisha muziki huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Mariam Mohmmed Hamdani, alisema zamani muziki wa Taarab ulikuwa wa aina moja na haukuwa na ushindani na hata radio nyingi za ndani na nje zilikuwa zikiupiga muziki huo asilia ikilinganishwa na sasa.

Alisema hivi sasa hapa Zanzibar kuna vikundi vingi vya Taarab ikilinganishwa na hapo awali jambo ambalo limesababisha Taarab asilia kushuka ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alisema mziki wa Taarab asilia katika miaka ya nyuma uliweza kufanya vizuri na kutamba ndani na nje ya nchi hususan katika nchi za Kiarabu na kufanikiwa kuitambulisha Zanzibar kupitia muziki huo ambao ulikuwa na wapenzi wengi.

## Karate Zanzibar sasa mwezi huu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

CHAMA Cha Karate Zanzibar kinatarajia kufanya mafunzo ya siku tatu yatakayoanza Februari 8-10, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa chama hicho, Abdalla Hussein 'Sensei Dula' alisema mafunzo hayo yatawashirikisha wanamichezo wa mchezo huo kwa rika zote wa ndani na nje ya Zanzibar.

Alisema mafunzo hayo yatatolewa na wakufunzi wapatao 10 kutoka barani Asia na Ulaya, katika Ukumbi wa Judo uliopo Amaan mjini hapa.

**"Mafunzo hayo ni ya siku tatu ambayo yata shirikisha rika zote na pia kutoka kwa jirani zetu Kenya pamoja na ndugu zetu Tanzania Bara nao watashiriki ," alisema.**

Hata hivyo, alisema lengo kuu la mafunzo hayo mbali ya kukuza uhusiano wa kitaifa na kimataifa pia yanalenga kuwaendeleza ili kufikia viwango vya juu katika mchezo wa karate.

Aidha, alisema katika mafunzo hayo zaidi ya washiriki 50 wanatarajia kushiriki.

# Michezo

Jumatano Februari 6, 2019

Nipashe




## Ramos afurahi kubeba jukumu la Ronaldo

HABARI UK 30

PATASHIKA...



Mshambuliaji wa West Ham United, Andy Carroll, katika harakati za kuunasa mpira kwa kichwa huku akiwa amemvuta jezi beki wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi usiku. **HABARI UK. 28**

# YANGA HASIRA ZOTE KWA SINGIDA UNITED

●●●Zahera atoa siri ya morali ya kuibuka na ushindi leo, Popadic apewa nafasi...

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema matokeo ya sare waliyoyapata kwenye mchezo uliopita anayaona kama siri ya ushindi katika mechi yao ya leo dhidi ya Singida United kwa kuwa yatawapa morali wachezaji wake.

Yanga inavaana na wenyeji wao hao kwenye mchezo utakaochezwa Uwanja wa Namfua huku Zahera akijaribu kusaka pointi tatu muhimu. Akizungumza na Nipashe jana, Zahera, alisema mchezo wa leo utakuwa mgumu kutokana na timu yake kukamiwa pindi inapokuwa nje ya Dar es Salaam.

"Tumesahahu matokeo yaliyopita, kwa sasa akili zetu zipo kwenye mchezo wa kesho (leo), hatutaki kuona tunapoteza tena pointi," alisema Zahera.

Alisema matokeo yoyote tofauti na ushindi yanawanyong'onyeza wachezaji wake.

"Mchezo uliopita [dhidi ya Coastal Union] waamuzi walikuwa na mapungufu..., tunacheza na Singida, lengo letu ni ushindi, wachezaji wangu wanafahamu nini cha kufanya kuhakikisha tunavuna pointi zote tatu," alisema Zahera.

"Hautakuwa mchezo mwepesi..., Singida United ni timu nzuri na watataka kupata matokeo mazuri kwenye uwanja wao wa nyumbani, tunajipanga kuwakabili," aliongeza kusema. Kwa upande wa Singida United ambayo mechi hiyo itakuwa ya kwanza kwa kocha Mserbia, Dragan Popadic kuiongoza dhidi ya Yanga kufuatia mzunguko wa kwanza kwenye Uwanja wa Taifa timu hiyo kuwa chini ya Shadrack Nsajingwa.

Hata hivyo, uongozi wa Singida United umetamba kulipa kisasi kwa Yanga leo kufuatia kushuka uwanjani ikiwa na kumkumbuku ya kipigo cha mabao 2-0 katika mzunguko wa kwanza ambayo yaliyofungwa na Amissi Tambwe.

Ofisa Habari wa Singida United, Cales Katemana alieleza kutambua wapinzani wao kutokana na kuwafuatilia muda mrefu na kwamba watatumia vema uwanja wao wa nyumbani.

"Tumejipanga kuibuka na ushindi kesho, hesabu zetu nabeba pointi tatu na kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri, tayari benchi la ufundi limefanyia kazi makosa yote hasa baada ya kutolewa kwenye SportPesa na Bandari pia hata mchezo wa Mbao FC ambao tulifungwa ni wakati wetu kuonyesha tofauti," alisema Katemana.

Baada ya mchezo huo, kesho Yanga itaanza safari ya kuelekea Tanga tayari kwa mechi yao nyingine ya ugenini dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Mkwakwani kabla ya kurejea Dar es Salaam kuanza maandalizi ya kuwakabili watani zao, Simba Februari 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa.

## Aussems aukubali usajili wa Mayanga



**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Simba Patrick Aussems, amesema anaufahamu uwezo wa mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Vitalis Mayanga aliyesajiliwa akitokea Ndanda FC kuchukua nafasi ya Shiza Kichuya ambaye ameuzwa Misri.

**UK. 31**

## Messi, Dembele hofu EL Clasico



**BARCELONA, Hispania**

WAKATI Barcelona ikitarajiwa kuivaa Real Madrid kwenye mchezo wa El Clasico ya Kombe la Mfalme ['Copa de Rey'] leo Jumatano, wachezaji Lionel Messi na Dembele wamezua hofu ya kuukosa mchezo huo utakaopigwa kwenye dimba la Nou Camp.

**UK. 29**

## Solskjaer atoa siri kubaki Man United



**MANCHESTER, England**

Ole Gunnar Solskjaer anamini yeye kocha sahihi wa Manchester United kama ambavyo anaelewa uhitaji wa kujitia majaribuni katika mashambulizi ya kushtukiza.

**UK. 28**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >